# Nipashe

Jumatatu Mei 20, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0581682
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
The Guardian digital · nipasheTZ · nipasheTZ · nipasheTZ · 0745 700710
LIKE & FOLLOW US



**FEI TOTO AFUNGUKA KUSUBIRIA OFA**

UK. 23



**Majaliwa** aagiza takwimu za sensa 2022 zitumike kutekeleza afua za wanawake

UK. 8



**Jeshi** lazuia jaribio kuipindua serikali DRC

UKURASA 19



**Suzan** Kunambi amrithi Jokate UWT

UKURASA 19



# Mapendekezo CHADEMA Tume Huru

UKURASA 2

UKURASA WA 10

## RC AAGIZA MILANGO KITUO CHA AFYA ING'OLEWE



MKUU wa Mkoa wa Shinyanga, Anamringi Macha, amebaini ubadhirifu katika ujenzi wa Kituo cha Afya Salawe wilayani Shinyanga, ikiwamo utengenezaji wa milango chini ya...

## Askofu anayedaiwa kujinyonga kuzikwa kwa taratibu za kanisa

UKURASA 2



Waziri Mkuu mstaafu, Fredrick Sumaye, akizungumza katika Mkutano Mkuu wa 29 wa Wanahisa wa Benki ya CRDB uliofanyika kwenye ukumbi wa Simba katika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa (AICC) jijini Arusha juzi.

## Sumaye aibua shangwe, vigelegele Mkutano Mkuu wa 29 wa Wanahisa wa Benki ya CRDB

UK. 4

**MICHEZO** YANGA, AZAM FAINALI YA KIBABE KOMBE LA FA UK.24

**MAONI,** UK.6

# Mapendekezo ya CHADEMA Tume Huru

**Na Elizabeth Zaya**

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kimewasilisha mapendekezo kwa Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi, kutaka marekebisho ya kanuni za uboreshaji daftari la kudumu la wapigakura ikiwa kuwapo utaratibu wa vyama kufanya kampeni ndani ya magereza.

Maoni hayo ambayo yamewasilishwa kwa Tume, wamependekeza kabla ya kuandikisha wapigakura ambao ni wafungwa na mahabusu, ifanyike sensa ya kujua idadi yao wanaotumikia adhabu ya kifungo kisichozidi miezi sita.

Kadhalika, kimependekeza ifanyike hivyo kwa mahabusu waliopo kwenye magereza yote nchini yakiwamo

makuu 12, ya wilaya 68, ya kilimo 46, kambi 40 na vyuo vya mafunzo kwa upande wa Zanzibar.

Pia kuwekwa kwa utaratibu wa vyama vya siasa kuwa na mawakala wa uandikishaji katika magereza ili kusimamia kazi hiyo ya uandikishaji wa wafungwa na mahabusu.

Kimependekeza kwamba Balozi za Tanzania nje ya nchi ziwe na vituo vya kuandikisha wapigakura ili

kuwawezesha Watanzania wanaoishi nje ya nchi kuwa na haki ya kujiandikisha kuwa wapigakura.

“Kama tumeweza kutoa haki hiyo kwa wafungwa na mahabusu, tuwape Watanzania wenzetu wanaoishi nje ya nchi haki hiyo,” ni sehemu ya mapendekezo ya chama hicho.

Mapendekezo mengine ni kutaka kuwapo na sifa mahususi za mtu kuteuliwa kuwa mratibu wa uandikishaji ngazi ya mkoa.

Kimetaka Tume iwe na jukumu la kusimamia na kuandikisha wapigakura katika Daftari la Kudumu la Wapigakura kwa ajili ya kura ya maoni na uchaguzi wa serikali za mitaa.

Aidha, kuwe na utaratibu wa kuitaka Tume kuwasiliana mara kwa mara na wadau wa uchaguzi hasa vyama vya siasa wakati wote wa kuboresha daftari hilo ikiwa ni pamoja na kutambua na kugawa vituo vya uandikishaji wa wapigakura.

Chama hicho kimetaka iongezwe kanuni kuruhusu waandishi wa habari kuwa kati ya wanaoruhusiwa

kuingia kwenye vituo vya uandikishaji na kuongeza wigo wa vitambulisho kwa kuongeza kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi.

Kimependekeza pia vyama vya siasa vipewe fursa ya kukagua daftari la awali ili kupeleka mapendekezo yao ya kuboresha daftari.



Makamu Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Zanzibar ambaye ni Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akiongoza kikao maalum cha Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya CCM Taifa jana katika ukumbi wa Ofisi Kuu ya CCM Kisiwandui, Wilaya ya Mjini Unguja, Zanzibar. **PICHA: IKULU**

# Wagonjwa 3,000 wanufaika huduma tiba, upasuaji za madaktari bingwa

**Na Ashton Balaigwa,**
MOROGORO

WAGONJWA zaidi ya 3,000 kutoka katika wilaya za Mkoa wa Morogoro wamenufaika kwa kupatiwa huduma za tiba na upasuaji kutoka kwa madaktari bingwa wa Dk. Samia Suluhu Hassan, walioweka kambi kwenye hospitali ya rufani ya mkoa huo.

Madaktari bingwa hao wamepangiwa kutoa huduma katika kambi ya Kanda ya Kati inayojumuisha mikoa ya Morogoro, Pwani, Iringa na Singida.

Akizungumza katika hitimisho ya kambi hiyo iliyofanyika katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Morogoro, Daktari Bingwa wa Upasuaji wa Mifupa kutoka Hospitali ya Tumbi, Kibaha mkoani Pwani, Dk. Amani Malima, alisema mafanikio hayo yametokana na idadi kubwa ya wagonjwa kujitokeza kupata huduma hizo.

Dk. Malima ambaye ni Mwenyekiti wa Kambi ya Kanda hiyo iliyokuwa na madaktari bingwa na bingwa bobezi zaidi 50, alisema lengo la awali katika programu hiyo ilikuwa ni kuwaona wagonjwa 2,000, lakini hadi kufikia tamati ya siku tano zilizowekwa wagonjwa 3,128 walionwa.

Alisema lengo la awali la wagonjwa watakaofikiwa, walikadiria kufanya upasuaji kwa wagonjwa 100, lakini kutokana na mwitiko mkubwa wagonjwa 109 walifanyiwa upasuaji na wote walitoka salama, wakati wagonjwa 37 walipatiwa rufani kwenda hospitali za kikanda na kitaifa.

Dk. Malima alisema, idara ya magonjwa iliyoongoza ni magonjwa yasiyoambukiza ama magonjwa ya ndani yakiwamo ya shinikizo la juu la damu, magonjwa ya kisukari na ya moyo.

Naye Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Ndani, Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Morogoro, Hadija Mahamoud, alisema idara yake ya magonjwa ya ndani ilikuwa na wagonjwa wengi akitoa mfano wa siku mbili za mwanzo ilipokea wagonjwa 649.

Dk. Hadija alimshukuru Rais kwa kuwasaidia wananchi hao ambao wamefurahi na huduma zilizotolewa na walitamani ziwe endelevu.

Baadhi ya wanufaika na huduma iliyotolewa na madaktari bingwa hao akiwamo Husna Shaibu, mkazi wa Dumila, Wilaya ya Kilosa, alishukuru huduma hiyo kutolewa mkoani Morogoro na kuwezesha wagonjwa wengi kufanyiwa uchunguzi na kupatiwa matibabu kwa gharama nafuu.

“Madaktari hawa wamewasaidia wananchi wengi ambao hawakuwa na uwezo na ninamwomba mheshimiwa Rais wetu na wabunge waendelee kutuletea huduma hizi ili sisi wananchi tunufaika kwani maradhi ni mengi na magonjwa nao ni wengi,” alisema Lukinda.

Mkazi wa Mawenzi, Manispaa ya Morogoro, Ally Said alisema huduma zilizotolewa ni nzuri, lakini muda uliopangwa ni mdogo kutokana na mwitikio wa wananchi na hiyo inaonesha kuwa Watanzania wengi wanaumwa.

Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Adam Malima, alimshukuru Rais Dk. Samia kwa kuwaleta madaktari bingwa mkoani humo na kuleta faraja kwa wananchi.

# Askofu anayedaiwa kujinyonga kuzikwa kwa taratibu za kikanisa

**Na Paul Mabeja,**
DODOMA

MWILI wa Askofu Mkuu wa Makanisa ya Methodist Tanzania (MCT), Joseph Bundala, anayedaiwa kujinyoga hadi kufa katika ofisi yake ndogo iliyopo kwenye kanisa hilo, Ipagala jijini hapo, unatarajiwa kuzikwa leo kama taratibu za uchunguzi wa kifo chake uliombwa na familia zitakamilika.

Aidha, Makamu Askofu Mkuu wa Kanisa hilo, Samwel Nyanza, ametangaza kufungwa kwa kanisa la MCT, Ipangala kwa siku 40, ambako tukio hilo lilitokea.

Akizungumza kwenye ibada maalumu iliyofanyika kwenye Kanisa la MCT Ihumwa, Makamu Askofu Mkuu Nyanza, alisema kanisa linatarajia kumzika kiongozi huyo kwa taratibu za kikanisa.

“Tangu jana yameibuka mambo mengi sana watu wanahoji kwa hili lililotokea sisi tunafanyaje na tunafahamu kuwa kuua na kujiua ni dhambi, lakini jana (juzi) tumejadiliana sana na tumeona tutamzika kwa mujibu wa taratibu zote za kanisa hayo mengine tunamwachia yeye na Mungu wake,” alisema Askofu Nyanza.

Askofu huyo aliwataka waumini wa kanisa hilo kuwa watulivu katika kipindi hiki kigumu wanachopitia kwa kuwa kila jambo linalotokea ni mpango wa Mungu.

“Huu unaweza kuwa ni mpango wa Mungu anataka kutukumbusha kuna mahali tumekosea hivyo kifo hiki kiwe sehemu ya sisi kulijenga kanisa upya, lakini kama kanisa inatupasa tuingie kwenye toba tumwombe sana Mungu atusimamie.

“Na kama tutashikana basi katika hili tutatoboa, lakini kama tutazubaa tutashindwa moja kwa moja na nimekuwa nikipokea ujumbe wa simu kutoka sehemu mbalimbali kuna ambao wanatupa pole, lakini wapo ambao hawatutakii mema hivyo tunapaswa kuwa imara zaidi ya wakati mwingine ili kulijenga kanisa letu,” alisema.

Kadhalika, aliwataka waumi kuwaombea viongozi wao wa dini ili kuondokana na tatizo la afya ya akili ambalo kwa kiasi kikubwa ndilo linachangia watu kufikia uamuzi mbaya kama huo.

“Afya ya akili ndiyo inaweza kufanya hiki kutokana na mizigo ya mambo ambayo viongozi wa dini wamebeba kutoka kwa waumini wao unakuta watu wana ugomvi unaletwa kanisani, mtu ana njaa linaletwa kanisani na mambo mengine kama hayo,” alisema.

Kuhusu kufungwa kwa kanisa la Ipagala, alisema waumini wataendelea kusali, lakini watafanya ibada zao nje hadi siku 40 zitakapoisha ndipo watali-weka wakfu na kuanza kutumika tena.

Katibu Mkuu wa Kanisa hilo, Askofu Allen Sisso, alisema ratiba ya mazishi itatolewa baada ya taratibu za kitabibu ambazo zinaendelea kufanywa na familia kuhusu uchunguzi wa nini hasa kimemuua kiongozi huyo wa kiroho.

“Watu wanaongea mambo mengi sana lakini sisi kama kanisa bado hatujatoa kauli yetu, tunasubiri uchunguzi ambao unafanywa na familia majibu ya kitabibu yatakayotoka ndipo na sisi tutatoa tamko letu kuhusu kifo cha Askofu wetu mkuu,” alisema Askofu Sisso.

Kaimu Kamanda wa Polisi mkoani Dodoma, Alchelaus Mutalemwa, akizungumzia tukio hilo Mei 17, mwaka huu, alisema Jeshi la Polisi linachunguza tukio hilo la Askofu huyo ambaye ni mkazi wa Ihumwa jijini hapa.

“Tukio hilo liligundulika Mei 16, 2024 majira ya saa moja usiku katika mtaa wa Meriwa, Dodoma ndani ya ofisi yake iliyopo katika kanisa hilo.”

Alisema uchunguzi wa awali katika eneo la tukio, umekutwa ujumbe unaoeleza sababu za kujinyonga ni madeni na mgogoro uliopo katika uendeshaji wa shule binafsi.

Aidha, dada wa marehemu, Veronica Alexandra alisema wanataka uchunguzi wa tukio hilo kwa kuwa Mei 16, aliwasiliana na kaka yake na kumwambia anapokea simu za vitisho na kwamba akili yake imefika mwisho na baadaye jioni alipokea taarifa za kifo chake.

# TRA: Hatua tunazochukua kabla ya kufunga akaunti

**Na Salome Kitomari**

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA), imetoa hatua tatu zinazochukuliwa kabla ya kufunga akaunti ya mdeni anayedaiwa kodi mbalimbali.

Aidha, imewakumbusha walipakodi kutekeleza wajibu wao wa kisheria wa kulipa kodi kwa hiari na wakati, ili kuepuka usumbufu na migogoro isiyo ya lazima.

Kwa mujibu wa taarifa kwa umma iliyotolewa jana na idara ya elimu kwa mlipakodi na mawasiliano ya TRA, hatua ya kuzuia akaunti ya mlipokodi ni ya mwisho kabisa ambayo hufanyika baada ya mlipakodi kutotimiza matakwa ya sheria ya kulipa kodi, kuvunja mkataba wa makubaliano aliyoingia na TRA ya kulipa kodi kwa awamu au kukaidi wito wa kufika ofisini.

Hatua ambayo huchukuliwa ni; kumwandikia mlipakodi hati ya madai (demand note) ambapo mlipakodi hupewa muda wa kutosha wa kulipa deni lake la kodi au kufika katika ofisi inayomhudumia kwa ajili ya majadiliano ya namna ya kulipa kodi husika.

Ya pili, mlipakodi asipotekeleza hatua ya kwanza, hatua ya pili ni kumwandikia barua ya kumkumbusha kutimiza wajibu wake wa kulipa kodi na kumtaka alipe kodi anayodaiwa au afike kwa majadiliano.

Ya tatu, mlipakodi asipotekeleza hatua zote, Kifungu cha 67 cha Sheria ya Usimamizi wa Kodi inampa mamlaka Kamishana wa TRA kutoa hati ya uwakala wa ulipaji kodi ambayo hupelekwa kwa mtu au taasisi inayomiliki fedha au mali za mlipakodi ambayo hutumika kama wakala wa mlipakodi na kutakiwa kulipa deni hilo la kodi kwa niaba yake.

Taarifa hiyo ilisema kuwa TRA hutumia njia mbalimbali za kisheria ili kukusanya mapato na madeni ya kodi zikiwamo kuwakumbusha na kuwaita wote wenye madeni ya kodi kukaa nao mezani kwa ajili ya kujadili namna ya kulipa kodi zao, ambayo huishia kwa kuingia mikataba ya kulipa madeni hayo kwa awamu.

"Kwa taarifa hii, TRA inawasihi walipakodi wote kuhakikisha wanalipa kodi kwa hiari na wakati, wale wenye changamoto za madeni ya kodi kufika katika ofisi za TRA zinazowahudumia kwa lengo la kujadili namna ya kutatua changamoto hizo.

Aidha, taarifa hiyo imesisitiza kuwa TRA hutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa sheria ambayo ni kukadiria, kukusanya na kuhasibu mapato yote ya serikali, kusimamia kwa makini na ufanisi sheria zote za kodi, kuishauri serikali kuhusu sera za mapato ya Taifa.

Pia kudhibiti udanganyifu na ukwepaji kodi na kuinua kiwango cha uwajibikaji wa kulipa kodi kwa hiari na kwamba hutekelezwa kwa kuzingatia misingi ya weledi, uwajibikaji na uadilifu.

# Mkuu Mweka apewa baraka za kitume na Papa Francis

**Na Salome Kitomari**

PAPA Francis ametoa baraka za kitume kwa Mkuu wa Chuo cha Usimamizi wa Wanyamapori Mweka, Profesa Jafari Kideghesho, kutokana na juhudi zake kusaidia huduma za kikanisa kwenye eneo hilo.

Kwa mujibu wa cheti cha pongezi kilichotolewa na kusainiwa na Papa Francis mwishoni mwa wiki; "Kupitia maombezi ya Bikira Maria aliyebarikiwa, Baba Mtakatifu anamwombea wingi wa neema za Mungu ziwe juu ya Profesa Kideghesho."

Kwa mujibu wa taarifa kwa umma iliyotolewa na Chuo cha Mweka na Ofisa Mkuu wa Uhusiano kwa Umma, Ernest Emmanueli: "Heshima hii inaonyesha namna Papa alivyotambua mchango mkubwa wa Profesa Kideghesho sio tu kwenye usimamizi wa wanyamapori barani Afrika, lakini kusaidia masuala ya kijamii kwenye jumuiya za Tanzania," alisema.

"Baraka ya kitume inatumika kama ishara ya kuthamini kujitolea kwa Profesa Kideghesho katika kazi yake na kujitolea kwake kuleta matokeo chanya kwenye ulimwengu," ilisema taarifa hiyo.

Akizungumza na Nipashe kuhusu hatua hiyo ambayo ni yenye manufaa kwake na Tanzania kwa ujumla, Profesa Kideghesho alisema chuo kimekuwa karibu na jamii ya eneo hilo.

Aidha, Profesa Kideghesho aliwashukuru wenyeji wa eneo hilo ambao wanakiri kuwa chini ya uongozo wake ushirikiano na jamii inayozunguka chuo hicho umeimarika.

Profesa Kideghesho ameshakuwa mkufunzi katika Chuo Kikuu cha Kilimo SUA mkoani Morogoro, Naibu Mkurugenzi wa Idara ya Wanyamapori katika Wizara ya Maliasili na Utalii na sasa ni Mkuu wa Chuo cha Usimamizi wa Wanyamapori Mweka, akiwa ameshachapisha machapisho ya kisayansi zaidi ya 40 kuhusu wanyamapori kwenye majarida ya kimataifa na vitabu mbalimbali.




MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA

**TAARIFA KWA UMMA**
**KUHUSU KUWAKUMBUSHA WALIPAKODI KUTEKELEZA WAJIBU WA KULIPA KODI KWA MUJIBU WA SHERIA**

**Dar es salaam, 18 Mei, 2024:**

Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), inapenda kuwakumbusha walipakodi kutekeleza wajibu wao wa kisheria wa kulipa kodi kwa hiari na wakati, ili kuepuka usumbufu na migogoro isiyo ya lazima.

Ifahamike kwamba, TRA hutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa sheria ambayo ni kukadiria, kukusanya na kuhasibu mapato yote ya serikali, kusimamia kwa makini na ufanisi sheria zote za kodi, kuishauri Serikali kuhusu sera za mapato ya Taifa, kudhibiti udanganyifu na ukwepaji kodi na kuinua kiwango cha uwajibikaji wa kulipa kodi kwa hiari. Majukumu yote haya hutekelezwa kwa kuzingatia misingi ya Weledi, Uwajibikaji na Uadilifu.

Mamlaka ya Mapato Tanzania hutumia njia mbalimbali za kisheria ili kukusanya mapato na madeni ya kodi zikiwemo kuwakumbusha na kuwaita wote wenye madeni ya kodi kukaa nao mezani kwa ajili ya kujadili namna ya kulipa kodi zao. Njia hii, huishia kwa kuingia mikataba ya kulipa madeni hayo kwa awamu.

Hatua ya kuzuia akaunti ya mlipakodi ni ya mwisho kabisa ambayo hufanyika baada ya mlipakodi kutotimiza matakwa ya sheria ya kulipa kodi, kuvunja mkataba wa makubaliano aliyoingia na TRA ya kulipa kodi kwa awamu au kukaidi wito wa kufika ofisini. Hatua zinazochukuliwa kabla ya kuzuia akaunti ya mlipakodi ni pamoja na: -

1. Ni kumuandikia mlipakodi Hati ya Madai (Demand Notice) ambapo mlipakodi hupewa muda wa kutosha wa kulipa deni lake la kodi au kufika katika ofisi inayomhudumia kwa ajili ya majadiliano ya namna ya kulipa kodi husika.

2. Mlipakodi asipotekeleza hatua ya kwanza, hatua ya pili hufuata ambayo ni kumuandikia barua ya kumkumbusha kutimiza wajibu wake wa kulipa kodi na kumtaka alipe kodi anayodaiwa au afike ofisini kwa majadiliano.

3. Mlipakodi asipotekeleza hatua zote tajawa hapo juu, Kifungu cha 67 cha Sheria ya Usimamizi wa Kodi (Tax Administration Act) inampa mamlaka Kamishna wa TRA kutoa hati ya uwakala wa ulipaji kodi (Agency Notice) ambayo hupelekwa kwa mtu au taasisi inayomiliki fedha au mali za mlipakodi ambayo hutumika kama wakala wa mlipakodi na kutakiwa kulipa deni hilo la kodi kwa niaba yake.

Kwa taarifa hii, TRA inawasihi walipakodi wote kuhakikisha wanalipa kodi kwa hiari na wakati, wale wenye changamoto za madeni ya kodi kufika katika ofisi za TRA zinazowahudumia kwa lengo la kujadili namna ya kutatua changamoto hizo.

***"Pamoja Tunajenga Taifa Letu"***

**Imetolewa na;**
**IDARA YA ELIMU KWA MLIPAKODI NA MAWASILIANO**

TANGAZO

# Sumaye aibua shangwe, vigelegele Mkutano Mkuu wa 29 wa Wanahisa wa Benki ya CRDB



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi (katikati), akipata maelezo kutoka kwa Meneja Mafunzo na Usimamizi wa Programu ya IMBEJU, Joshua Mwakalobo, wakati alipowasili katika Semina ya Wanahisa wa Benki ya CRDB iliyofanyika Ukumbi wa Mikutano wa Kimataifa wa Arusha (AICC). Kushoto kwake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela na Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi Benki ya CRDB, Dk. Ally Hussein Laay.

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

WAZIRI Mkuu mstaafu, Frederick Sumaye ameonesha kuguswa na umahiri wa Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela, baada ya kufanya mageuzi makubwa ya kiutendaji ndani ya benki hiyo tokea alipokabidhiwa kijiti na aliyekuwa Mkurugenzi Mtendaji wa benki hiyo, Dk. Charles Kimei.

Sumaye aliyaeleza hayo wakati akitoa maoni yake katika Mkutano Mkuu wa 29 wa Wanahisa wa Benki ya CRDB baada ya kuwasilishwa kwa Taarifa ya Ripoti ya Wakurugenzi na Taarifa ya Hesabu zilizokaguliwa na gawio kwa mwaka 2023 ambapo utendaji wa benki hiyo umeonekana kuendelea kuimarika, huku thamani ya uwekezaji wa wanahisa ikiendelea kukua mwaka hadi mwaka.

Taarifa ya fedha iliyowasilishwa na Ofisa Mkuu wa Fedha wa Benki hiyo, Fredrick Nshekanabo, inaonyesha mizania ya Benki ya CRDB na kampuni zake tanzu imeendelea kuimarika kufikia Sh. trilioni 13.3 mwaka 2023 ikiwa ni ukuaji wa asilimia 121 tokea Nsekela aliposhika hatamu mwaka 2018.

Taarifa hiyo pia inaonesha ukuaji mkubwa katika viashiria mbalimbali vya kiutendaji ambapo Faida Baaada ya Kodi imeongezeka kwa takribani asilimia 560 kufikia Sh. bilioni 422.8 mwaka jana, jambo ambalo limepelekea kuongezeka gawio kwa hisa kutoka Sh. 5 mwaka 2018 hadi Sh. 50 mwaka 2023 sawa na ukuaji wa asilimia 900.

Akichangia katika ripoti hiyo ambayo pia imeonesha ukuaji mkubwa wa Kundi la Benki ya CRDB ambapo kampuni tanzu mpya tatu zimeanzishwa chini ya uongozi wa Nsekela ikiwamo ile ya DRC, CRDB Bank Foundation, CRDB Insurance Company Ltd, Sumaye aliibua hoja katika mkutano huo ya kuiomba Benki Kuu ya Tanzania (BoT) kubadili kanuni zinazomtaka Mkurugenzi Mtendaji wa benki nchini atumikie kwa kipindi kisichozidi miaka 10.

Sumaye alisema kuwa Nsekela ameonesha uwezo mkubwa, hata kuifanya benki hiyo kuweka rekodi ya faida ambayo haikuwahi kufikiwa huko nyuma.

"Mzee Kimei (Mkurugenzi Mtendaji wa zamani wa CRDB) aliitoa mbali sana benki hii na kuifikisha pale alipoipokea Abdulmajid," Sumaye alisema na kuelezea zaidi hoja yake kwamba:

"Niliwahi kumwambia jambo hili Profesa (Florens) Luoga (Gavana mstaafu wa BoT ambaye alikuwa miongoni mwa wageni waalikwa katika mkutano huo) -- benki ni taasisi nyeti, tatizo dogo tu linaweza kuwa na athari kubwa mno.

"Kwa benki kubwa kama CRDB na NMB, Mkurugenzi Mtendaji akiwa na vision (dira) nzuri, aachwe atekeleze maono yake. Ningependa sana vision (dira) hii ya Mkurugenzi Mtendaji wa CRDB, aachwe aitekeleze," Sumaye akasisitiza.

Ni hoja iliyoibua shangwe kwa wanahisa ukumbini, Waziri Mkuu mstaafu Sumaye akieleza kwa kutumia mfano kwamba benki hizo mbili tajwa zinashikilia uchumi wa nchi.

"Ninajua kuna kitu BoT cha miaka 10. Ninafikiri pawapo rukhsa kwa baadhi ya benki viongozi wake wapewe muda zaidi kutekeleza maono yao," alisema Sumaye na kuibua shangwe zaidi ukumbini, wanahisa wakikatisha maelezo yake kwa furaha. Katika mkutano huo pia alikuwepo mwakilishi wa Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania (BOT).

Sumaye, aliyekuwa Waziri Mkuu wa Tanzania kuanzia Novemba 28, 1995 hadi Desemba 30, 2005 katika uongozi wa Rais wa Awamu ya Tatu, Benjamin Mkapa, alisema ni muhimu kuwakumbatia viongozi wenye maono mazuri kwa ustawi wa benki na uchumi wa nchi kwa ujumla.

Pamoja na hilo, Sumaye pia alipongeza jitihada za Benki ya CRDB katika kupanua wigo wake wa utoaji huduma katika masoko ya ndani na nje ya nchi huku akisema kuingia katika DRC kuna fungua fursa nyingi za kiuchumi kwa wafanyabiashara wa Tanzania. Aidha alishauri kuchukua tahadhari katika utekelezaji mkakati wake wa kujitanua zaidi.

Sumaye pia alipongeza Benki ya CRDB kwa kuwa na mtazamo chanya dhidi ya maendeleo ya teknolojia. Alieleza mzizi wa hoja yake juu ya teknolojia unatokana na darasa kwenye semina mojawapo, akisema:

"Ninawapongeza (CRDB) kwa mtazamo mlionao kwenye teknolojia. Angalieni uwekezaji katika matawi utakuwa na tija miaka ijayo? Tunapaswa kuangalia manufaa ya muda mrefu. Kama kweli kuna mahali wananchi hawajui huduma za mtandaoni, tuweke majengo machache na tutumie zaidi mawakala."

Yakirejewa mageuzi ya uchumi nchini, Sumaye ndiye aliyekuwa Mtendaji Mkuu wa Shughuli za Serikali - Waziri Mkuu, wakati wa kutekeleza mageuzi ya sekta ya fedha nchini (soko la fedha za kigeni, Sheria ya Fedha sambamba na Sheria ya Benki).

Ni kipindi ambacho ulifanyika ubinafsishaji Benki ya Ushirika na Maendeleo Vijijini hadi kuwapo Benki ya CRDB. Hali kadhalika, kutoka kuvunjwa Benki ya Maendeleo ya Biashara ambayo ilizaa NMB.

Muundo wa sasa wa benki zilizopo nchini unatokana na mageuzi ya ubinafishaji uliofanywa na Serikali ya Awamu ya Tatu, ukisimamiwa na Tume ya Rais ya Kurekebisha Mashirika ya Umma (PSRC).

Katika mkutano huo, Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Nsekela, alisema mkakati mpya wa biashara umekuwa muhimu kwa mafanikio ya benki, ukifanya kazi kama ramani ya kuboresha utendaji kazi.

Nsekela pia alisema kuwa Benki ya CRDB imewekeza kwa kiasi kikubwa katika kukuza ujumuishi wa kifedha, kwa wajasiriamali na wafanyabiashara. Kupitia mpango wa IMBEJU, taasisi ya CRDB Bank Foundation imeboresha uwezeshaji kwa vijana na wanawake. Zaidi ya hayo, benki imeunda ushirikiano wa kimkakati ili kufadhili vyema miradi ya maendeleo nchini.

Nsekela alielezea mipango ya siku za usoni ya Benki ya CRDB na kampuni zake, akisisitiza kuongeza mchango wa kampuni tanzu zilizoanzishwa, kuboresha huduma kwa wateja na kuwekeza zaidi katika ubunifu wa kidijiti.

Vilevile, alisema benki hiyo itaendelea kuongeza usimamizi mkubwa katika vihatarishi, na kuhakikisha inaendana na mabadiliko ya usimamizi na kuhakikisha utawala bora.

Wakati wa kutambulishwa rasmi katika Benki ya CRDB Oktoba 10, 2018, Nsekela alitaja vipaumbele vyake ambavyo ni: Uboreshaji mifumo ya huduma; kuongeza weledi na umahiri wa wafanyakazi; kuwekeza katika teknolojia ya kisasa na kukuza biashara katika nyanja zote. Vipaumbele ambavyo vimeleta matokeo makubwa katika utendaji wa benki hiyo.

| MWAKA | PAT (SH. BIL) |
|---|---|
| 2018 | 64.1 |
| 2019 | 120.1 |
| 2020 | 165.2 |
| 2021 | 268.2 |
| 2022 | 351.4 |
| 2023 | 422.8 |

CHANZO: CRDB, Mei 18, 2024

Akiunga mkono hoja ya Waziri Mkuu mstaafu Fredrick Sumaye, aliyekuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Benki hiyo ambaye sasa ni Mbunge wa Vunjo (CCM), Dk. Charles Kimei amesema Nsekela ameweza kuvivaa viatu vyake na kupitiliza kutokana na ukuaji mkubwa ambao Benki ya CRDB imeushuhudia katika kipindi chake cha uongozi.

# TFS inavyoifanya sekta ya nyuki kuwa na mchango mkubwa katika uchumi wa Taifa

**Na Mwandishi Wetu**

Nyuki ni jamii ya wadudu ambao huishi maisha ya kijamaa, niwadudu wenye jozi mbili za mabawa mepesi yenye mishipa laini. Mwili wa nyuki umegawanyika katika sehemu kuu tatu ambazo ni kichwa, kifua na tumbo/fumbati. Tofauti na wadudu wengine nyuki hutengeneza na kuhifadhi asali kwenye kiota chake (yaani masega).

Kuna takriban aina elfu ishirini (20,000) tofauti za nyuki wanaouma duniani. Nyuki hawa wanatofautiana kwa maumbile, ukubwa na tabia lakini wote wanashabihiana katika tabia moja kuu ya kutembelea maua ili kukusanya mbochi (maji matamu yanayotengeneza asali) na chavua (unga unaopatikana kwenye maua) kwa ajili ya chakula chao.

Nyuki wanaouma wanaopatikana Tanzania wamegawanyika katika makundi matatu kutegemeana na mahali wanakoishi. Wapo wanaopatikana katika maeneo ya mwambao: Apis Mellifera litorea ambao wana umbo dogo na ni wakali sana; Apis Mellifera scutellata wana umbo la wastani, ni wakali kiasi na hutoa asali kwa wingi, wanaptikana maeneo ya tambarare na Apis Mellifera monticola - wana umbo kubwa, ni wapole sana, wanapatikana maeneo ya milimani.

Nyuki wasiouma - Huishi ndani ya matundu ya miti, chini ya matawi makubwa ya miti, kwenye vichuguu vya mchwa na hata chini ya mapaa ya nyumba. Uzalishaji wao wa asali ni mdogo ukulinganisha na nyuki wanaouma. Asali ya nyuki hawa inaaminika kuwa na uwezo mkubwa wa kutibu maradhi mbalimbali kuliko ya wale wanaouma.

**KUNDI LA NYUKI**

Kundi la nyuki lina jinsia mbili, yaani nyuki jike na nyuki dume na lina aina tatu za nyuki ambao ni vibarua, malkia na dume.

Nyuki vibarua (Worker bee): Nyuki vibarua ndio watendaji wakuu wa kazi zote muhimu kwa ustawi wa kundi la nyuki lililokamilika. Hawa ni nyuki wa kike ambao huunda idadi kubwa katika kundi ambao hufanya kazi ya kukusanya mbonci (nectar) na chabua (pollen) kutoka kwenye maua, kujenga masega, kulea majana, na kutunza mazingira ya mizinga.

Nyuki wa Kiume (Drones): Idadi yao ni ndogo katika kundi ukilinganisha na ya kike na hawana uwezo wa kuvuna mbochi na chavua, ambao kazi yao kuu ni kuzalisha mbegu kwa kumfikia na kumjilia malkia, na kwamba hawana uwezo wa kujikinga wenyewe na hivyo hutegemea kundi kwa chakula.

Malkia (Queen Bee) ni malkia ni nyuki mmoja pekee katika kundi ambaye majukumu yake ni kuzalisha mayai na kuongoza kundi. Nyuki malkiahuzalisha kemikali inayoitwa "pheromone" ambayo inawaongoza nyuki wengine kudumisha utaratibu wa kundi.

**UCHAVUSHAJI**

Tendo la kuchavusha mimea linalofanywa na nyuki linawezesha uendelevu wa uhai wa viumbe vingine wakiwemo binadamu. Nyuki wanajulikana kama kiumbe kinachofanya kazi ya kuchavusha mimea kwa ufanisi mkubwa zaidi.

Kuelekea maadhimisho ya Siku ya Nyuki Duniani, Watanzania wamashauriwa kutambua umuhimu wa nyuki kwa kulinda makazi ya nyuki, kudhibiti matumizi ya dawa za wadudu na kuhamasisha ufugaji wa nyuki kibiashara ili kufanikisha malengo ya maendeleo ya taifa na kujenga maendeleo ya taifa na mustakbal bora kwa vizazi vijavyo.

Siku hii huadhimishwa tarehe 20 Mei ya kila mwaka, ambapo kaulimbiu ya mwaka huu ni "Shirikisha Vijana na Nyuki" ambayo kauli mbiu hii inasisitiza umuhimu wa



*Mitambo ya kuchakata asali katika kiwanda cha TFS kilichopo wilaya ya Manyoni*

kushirikisha vijana katika juhudi za ufugaji nyuki na uhifadhi wa viumbe wachavushaji wengine, wakiwatambua kama walinzi wa mazingira yetu ya sasa na baadaye.

Kamishna wa Uhifadhi wa Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS), Prof. Dos Santos Silayo alisema kuwa jamii inapaswa kutambua umuhimu wa nyuki katika kudumisha afya ya ikolojia, ustawi wa kilimo na kuleta maendeleo endelevu hivyo ni vyema kuchukua hatua za kulinda ustawi wa maisha ya Nyuki hao.

"Nyuki si tu wazalishaji wa asali bali pia ni wachavushaji muhimu ambao mchango wao ni mkubwa na unahitajika sana katika uzalishaji wa chakula na utunzaji wa mazingira yetu. Ni wakati wa kuchukua hatua za kuhakikisha tunalinda makazi yao, kudhibiti matumizi ya dawa za kuulia wadudu, na kuhamasisha ufugaji wa nyuki kwa njia endelevu,"alisema.

Kwa mujibu wa Prof. Silayo, jamii inaweza kufanikisha malengo ya maendeleo ya Taifa na kujenga mustakbal bora kwa vizazi vijavyo hivyo kuungana kwa pamoja kuwa walinzi wa nyuki na kuleta mabadiliko chanya katika jamii zetu.

Alisema kuwa tafiti zilizofanywa ndani na nje ya nchi zinaonesha kuwa takriban asilimia 80 ya mimea ya chakula duniani huchavushwa na nyuki kwani nyuki wanachavusha mazao ya chakula na biashara na mimea mbalimbali na ni muhimu katika mnyororo wa chakula na bioanuwai.

"Pamoja na faida hizo nyuki anatoa mazao kama vile asali, nta, chavua, maziwa ya nyuki, gundi ya nyuki na sumu ya nyuki ambazo pia ni malighafi ya viwandani kwa ajili ya kutengeneza bidhaa nyingine," aliongeza Prof. Silayo.

Prof. Silayo alisema kuwa kwa bahati mbaya, idadi ya nyuki duniani kote inapungua kutokana na sababu mbalimbali kama kupoteza makazi yake kunakosababishwa na uharibifu wa mazingira hivyo kutokana na changamoto hiyo serikali kupitia TFS imeendelea kuweka mazingira wezeshi ya kuwalinda nyuki pamoja na kuhamasisha ufugaji wa nyuki kibiashara.

Akielezea umuhimu wa siku ya Nyuki Duniani, Prof. Silayo alisema kuwa Nyuki na wadudu wengine wachavushaji ni muhimu kwa uwepo wetu hapa duniani, wanadumisha kilimo na bioanuai ulimwenguni kote kwani kuna zaidi ya spishi 20,000 za nyuki na wadudu wengine wachavushaji, wanakabiliwa na changamoto kutokana na shughuli za kibinadamu, kama vile upotevu wa makazi, matumizi ya dawa za kuua wadudu, na mabadiliko ya tabianchi.

Alisema kuwa nyuki wanazidi kuwa hatarini japokuwa ni wazi kuwa mchango wao katika uchavushaji wa mimea ni muhimu kwa mstakbal wa ustawi na uwepo wa dunia hivyo TFS imeweka jitihada mbalimbali kukabiliana na changamoto hiyo ikiwemo uhifadhi wa mazingira, kuelimisha jamii, kusimamia matumizi ya dawa za wadudu, kuhamasisha ufugaji wa nyuki, utafiti na ufuatiliaji .

Hata hivyo, Prof. Silayo alisema kuwa TFS inafanya juhudi mbalimbali katika kuboresha Sekta ya Ufugaji Nyuki nchini ambapo baadhi ya hatua hizo ni kuendeleza misitu, kutoa elimu na mafunzo na kusaidia vikundi vya wafugaji nyuki nchini.

Aliongeza kuwa pia TFS inaweza kusaidia katika utafutaji wa masoko ya mazao ya nyuki kwa njia mbalimbali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali kama Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TANTRADE) na sekta binafsi.

"Hii inajumuisha kuwezesha ushiriki wa wadau kwenye maonesho ya biashara kama Sabasaba na maonesho ya wakulima ya Nanenane, vyama vya wafanyabiashara, na wauzaji wa malighafi.

Vilevile, kuandaa na kutekeleza mpango wa kudhibti mabaki ya kemikali (Chemical Residue Monitoring Plan) katika asali. Mpango huo hutekelezwa kwa kukusanya na kufanya uchambuzi wa sampuli za asali kila mwaka. Uchambuzi wa asali unaonesha asali ya Tanzania imeendelea kukidhi viwango vya ubora katika masoko ya nje ya nchi. Hii ni kutokana na kutokuwa na mabaki ya kemikali.

kigezo cha kutokuwa na mabaki ya kemikali kinatumiwa na nchi za Umoja wa Ulaya (European Union) kudhibiti usafirishaji wa asali kwenda nje ya nchi. Hivyo TFS ni mhusika mkuu nchini katika kuhakikisha asali ya Tanzania inakidhi vigezo vya afya ya walaji," alisema.

Alisema japokuwa Sekta ya Ufugaji Nyuki ni ndogo ina umuhimu mkubwa katika kutimiza malengo ya maendeleo ya Taifa kwa njia kadhaa, ikiwepo kuinua kipato cha wakulima na wafugaji kwani ufugaji wa nyuki ni shughuli inayoweza kutoa fursa za kujipatia kipato kwa wakulima na wafugaji wadogo.

"Pia kwa kutoa bidhaa kama asali, nta, gundi ya nyuki (propolis), na maziwa ya nyuki, sekta hii inaweza kusaidia kuongeza mapato ya familia na kuboresha maisha ya wafugaji na kuongeza uhakika wa chakula. Nyuki ni sehemu muhimu ya mfumo ikolojia na hufanya kazi kama walinzi wa mazingira kwa kusaidia katika uchavushaji wa mimea na kuhifadhi bioanuwai,"alisema Prof. Silayo.

Aidha, alisema kukuza Sekta ya Ufigaji Nyuki, kunaweza kuchangia katika uhifadhi wa mazingira na kudumisha mfumo ikolojia wenye afya, kukuza Sekta ya Utalii ambapo nyuki wanaweza kuwa kivutio kwa watalii wanaovutiwa na utamaduni wa ufugaji nyuki, kutembelea mashamba ya nyuki, na kujifunza juu ya faida za mazao ya nyuki na bidhaa zake, hivyo kusaidia katika kuongeza mapato kupitia utalii wa ndani na wa kimataifa.

Kama mtoa huduma wa misitu nchini, TFS inafanya jitihada kusaidia katika kukuza Sekta ya Ufugaji Nyuki na kusaidia wakulima na wafugaji wa nyuki kujikwamua kutoka kwenye umaskini. Baadhi ya jitihada hizo ni pamoja na: elimu na mafunzo, kuwezesha upatikanaji wa rasilimali, kuendeleza masoko, na kutekeleza miradi ya maendeleo.



Sehemu ya mizinga ya kufugua nyuki ya TFS iliyopo Msingisi, Gairo mkoani Morogoro.



Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Wachezaji kuweni makini na mikataba mipya

**LIGI** Kuu Tanzania Bara msimu wa 2023/2024 unaenda ukingoni, sasa zimebaki mechi tatu kwa kila timu kutamatisha msimu huu na kuanza kujiandaa na msimu ujao.

Kumalizika kwa msimu mmoja ni mwanzo wa maandalizi ya msimu mpya kwa wachezaji, mabenchi ya ufundi na hata viongozi wa klabu.

Kila unapoanza msimu mpya ni kipindi cha wachezaji kuongeza mikataba yao kwa wale ambao wanaimaliza, lakini ndio kipindi cha usajili kwa wachezaji wapya, kiufupi ni kipindi cha uhamisho wa wachezaji na hata makocha.

Ni kipindi cha kuvuna kwa wachezaji, kipindi cha kuona thamani ya kipaji na uwezo wa kucheza soka kwa kila mchezaji alichozawadiwa na Mwenyezi Mungu.

Kwa wachezaji hiki ni kipindi ambacho wanatakiwa kuwa makini zaidi kwenye kufanya uamuzi wa kujiunga na timu nyingine kwa ajili ya kuendeleza kipaji chao.

Ni kipindi ambacho kama mchezaji hatokuwa makini kuna mambo mawili yanaweza yakamkuta, kwanza anaweza akajiunga na timu ambayo hana uhakika wa kupata muda wa kucheza na kujikuta anatumia muda mwingi akiwa benchi, kuna uwezekano mkubwa wa kushusha kiwango cha uchezaji au kuua kabisa kipaji.

Wapo wachezaji wengi ambao hawaangalii mustakabali wa kipaji chake, anachoangalia ni kiasi gani anaingiza kwenye uhamisho kuhamia timu mpya.

Hapa lazima tuwakumbushe wachezaji hususani wachezaji wazawa, umakini mkubwa unatakiwa katika kuingia mikataba mipya au kuongeza ile ya zamani ili kukwepa migogoro ya kimkataba.

Soka la sasa linahitaji weledi mkubwa katika kufanya uamuzi kwa wachezaji linapokuja suala la mikataba mipya.

Nipashe tunawashauri wachezaji hasa wazawa kutumia wataalamu hususani wanasheria katika kuingia mikataba ya kujiunga na timu nyingine au kuongeza mikataba wanapocheza sasa.

Kwa nini tunasema hivyo, kumekuwa na migogoro mingi kati ya wachezaji na klabu linapokuja suala la mikataba, tunashauri wasisaini mikataba bila kuwa na uwelewa wa vifungu vilivyoko, ndio maana tunashauri wawatumie wanasheria.

Ni vizuri kuwa na uwelewa wa kile unachotaka kukisaini kama makubaliano ya uhamisho, kujua haki za mchezaji na wajibu wake kwa mwajiri, hii itasaidia mchezaji kuwa huru na kazi yake.


Tumeshuhudia nchini wachezaji wakiingia kwenye migogoro na klabu zao pale mikataba yao inapoisha au wanapotaka kuingia mikataba mipya.

Jambo pekee kwa wachezaji wetu kuepuka migogoro ya kimkataba ni kuwatumia watu sahihi kwenye kuielewa mikataba yao kwa sababu ni ukweli usiopingika mikataba mingi inaandikwa kwa lugha ya Kiingereza.

Lugha hiyo imekuwa changamoto kwa baadhi ya wachezaji wetu hasa wale wazawa, sio mbaya kama mchezaji atamshirikisha mtu wake wa karibu na mwenye uwelewa wa lugha.

Tunawakumbusha wachezaji hiki ndio kipindi cha kupiga pesa na kuona thamani ya kipaji chao walichojaliwa na Mungu, wanapaswa kuwa makini kwenye kuongeza mikataba au kusaini mikataba mipya ya kujiunga na timu nyingine.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Adam Fungamwango

## Muungwana Lazima Nilonge

# Wachezaji wazawa msimu huu wametisha Ligi Kuu

**NAWEZA** kusema baada ya misimu takriban mitatu au minne hivi, msimu huu wachezaji wengi wa kitanzania wameonekana kufanya vyema kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara.

Japo si kwa kiwango kinachotakiwa, lakini angalau msimu huu wachezaji wazawa wameonekana kupigana vikumbo na wale wa kigeni kiasi kwamba hata klabu kubwa za Simba, Yanga na Azam, zinaweza kufanya usajili wa wachezaji wengi wa hapa kuliko misimu mingi iliyopita.

Wachezaji wazawa wa Simba, Yanga na Azam wameonekana kuamka, wamepambana vya kutosha kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara.

Ukisoma au kusikiliza tetesi za usajili wa wachezaji Ligi Kuu kabla hata ligi haijamalizika, inaonyesha hivyo, Simba na Yanga zinaonekana kutaka kujiimarisha zikianza kutaka kusajili wachezaji wazawa, kitu ambacho misimu michache nyuma haikuwa hivyo.

Klabu hizo zilikuwa zinapigana vikumbo kusaka wachezaji wa kimataifa kutoka nje ya nchi, huku soko la ndani likiwa ni kwa zile zinaitwa au kujiita klabu ndogo.

Ilikuwa inatia huzuni kila unaposoma habari za usajili, Simba, Yanga na Azam zikiwa zinawania wachezaji kutoka nje tu, wa hapa kama wakibahatika ni mmoja au wawili tu.

Matokeo yake, wachezaji wa Kibongo walionekana kuzunguka kwenye klabu zingine tu.

Hii haikuwa kwa bahati mbaya, kwani viwango vyao havikuwa vinawashawishi hata mashabiki wa soka achilia mbali viongozi wa klabu.

Leo hii kuna wachezaji wengi wazawa walioonyesha viwango vya juu msimu huu kama Mohamed Ibrahim 'Bacca', Nickson Kibabage, Mudathir Yahaya, Aboubakar Salum 'Sure Boy' na wengine wa Yanga, pia wamo Ladack Chasambi, Edwin Balua, Hussein Abel, Saleh Karabaka wa Simba, Feisal Salum, Ayoub Lyanga, Abdul Suleiman Sopu wa Azam FC.

Tukienda kwenye klabu zingine ambao wameanza kuzishawishi hata klabu kubwa kuwasajili ni, Yusuph Kagoma na Aziz Andambwile wa Singida Fountain Gate, Lameck Lawi wa Coastal Union, Zabona Mayombya wa Prisons, hao ni kwa uchache, lakini wapo wengi.

Ndiyo maana utaona safari hii, klabu kubwa macho yao ni kusajili kwanza wachezaji wa ndani, halafu wa nje baadaye.

Miaka michache iliyopita ilionekana kuwa wachezaji wa Kitanzania waliopo Simba na Yanga ni bora zaidi kuliko walio kwenye klabu zingine, hivyo bora wabaki nao hao kuliko kusajili wengine.

Pamoja na yote hayo, shukrani za pekee ziwaendee wachezaji wa kigeni kutoka nje, ambao kwa kiasi kikubwa wamekuja kuwaamsha wazawa ambao kuna kipindi ilionekana kama wamebweteka.

Walionekana kama hawazisaidii timu zao na kuonekana mizigo kwa waajiri wao.

Mchezaji analipwa mshahara na posho, lakini hataki mazoezi, hana nidhamu, analewa na kufanya anasa kiasi kwamba hata uchezaji wake unakuwa wa kusuasua, leo anacheza vizuri kesho anavurunda.

Wachezaji wa nje ndiyo wanaoonekana kuwakumbusha wazawa kuwa mpira ni kazi kama kazi zingine, haifai kuufanyia masihara, kwa sababu mtu anaendesha maisha kutokana na mchezo huo.

Kilichotufelisha ni kwamba zamani soka lilikuwa la ridhaa, wachezaji hawakuwa wanalipwa mishahara zaidi ya posho tu, hata lilipoingia soka la kulipwa, bado akili za wachezaji wetu ziliendelea kubaki kule kule.

Matokeo yake wageni wanakuja nchini na kuvuna pesa nyingi, kutokana na uwezo na viwango vyao, kujituma, nidhamu, hivyo kupendwa na mashabiki pamoja na viongozi wao kwa kile wanachotoa kwa klabu.

Nawapongeza sana wachezaji walioanza kujitambua na kujituma kiasi cha kuonekana na kuwa lulu, ambao ujio wa wageni haukuwafanya kuona kama wanazibiwa nafasi za kucheza kwenye klabu zao, bali changamoto kwao ili kujitambua.

Nalipongeza pia Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF), pamoja na Bodi ya Ligi kwa kuziba masikio ya wale waliokuwa wanapinga uwezo wa wachezaji wengi na kigeni, wakiomba wapunguzwe.

TFF na Bodi zilikataa zikidai wachezaji hao wanaleta chachu kwa wazawa. Na kweli hili tumeliona, wamekuwa walimu wazuri kiasi kwamba sasa wachezaji wengi wa wazawa wamekuwa na soko kuelekea msimu ujao wa ligi tofauti na misimu kadhaa nyuma.

# TANGAZO

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI

## TANGAZO LA MWALIKO WA WAANGALIZI WA NDANI WA UANDIKISHAJI WA WAPIGA KURA

Kwa mujibu wa kanuni ya 46(1) ya Kanuni za Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura za Mwaka 2024, Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi inaalika Asasi na Taasisi zenye nia ya kuangalia zoezi la uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura. Uboreshaji huo utaanza kufanyika kuanzia mwezi Julai, 2024 kwa kuzingatia ratiba itakayotolewa na Tume.

Kupitia tangazo hili, Tume inakaribisha maombi kutoka kwa taasisi na asasi mbalimbali nchini ambazo zinahitaji kuangalia zoezi la uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura. Maombi hayo yawasilishwe kupitia anuani (link) ifuatayo: **https://ams.inec.go.tz**

**Barua ya maombi itatakiwa kuainisha mambo yafuatayo: -**

i. Anuani kamili ya taasisi au asasi husika;
ii. Mahali ambapo taasisi au asasi husika inafanyia kazi (Physical address);
iii. Shughuli ambazo zinafanywa na taasisi au asasi husika kwa mujibu wa hati ya usajili;
iv. Sehemu ambazo taasisi au asasi inaomba kwenda kuangalia uandikishaji;
v. Idadi ya watu ambao taasisi au asasi itawatumia katika zoezi hilo pamoja na majina na taarifa zao binafsi;
vi. Majina na namba za simu za viongozi watatu wa taasisi au asasi;
vii. Ikiwa taasisi au asasi ya ndani inahusisha viongozi ambao si raia wa Tanzania, viongozi wawili ni lazima wawe watanzania;
viii. Kuambatisha nakala au kivuli cha hati ya usajili wa taasisi au asasi husika; na
ix. Kuambatisha nakala au kivuli cha katiba ya taasisi au asasi husika.

Maombi yatakayozingatiwa ni yale yatakayowasilishwa kupitia anuani (link) ifuatayo: **https://ams.inec.go.tz**

Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 30 Mei, 2024.
Tume haitahusika na utoaji wa rasilimali fedha au rasilimali nyingine kwa ajili ya kugharamia zoezi la uangalizi kwa taasisi au asasi zitakazopewa kibali.

Imetolewa leo tarehe 17 Mei, 2024 na:

**Kailima, R. K**
**MKURUGENZI WA UCHAGUZI**

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI

## TANGAZO LA MWALIKO KWA TAASISI NA ASASI ZA KIRAIA ZENYE NIA YA KUTOA ELIMU YA MPIGA KURA WAKATI WA UBORESHAJI WA DAFTARI LA KUDUMU LA WAPIGA KURA MWAKA 2024

Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi inatarajia kufanya uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura Mwaka 2024. Uboreshaji huo utaanza tarehe 01 Julai, 2024 katika Mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora. Ratiba ya mikoa mingine itatangazwa kadri Tume itakavyokuwa inaendelea na zoezi.

Kwa mujibu wa kifungu cha 10(1)(g) na (h) cha Sheria ya Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi Na. 2 ya Mwaka 2024, Tume ina wajibu wa kutoa elimu ya mpiga kura nchini, kuratibu na kusimamia taasisi na asasi za kiraia zinazotoa elimu hiyo.

Hivyo, kupitia tangazo hili, Tume inakaribisha maombi kutoka taasisi na asasi za kiraia nchini zenye nia ya kutoa elimu ya mpiga kura katika uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura 2024 kama ilivyoainishwa kwenye jedwali.

Taasisi na asasi za kiraia zenye nia ya kutoa elimu ya mpiga kura zinatakiwa kuwasilisha maombi yao katika mfumo wa kusajili watazamaji, asasi za kiraia na vyombo vya habari (Accreditation Management System - AMS) unaopatikana katika anwani ya **https://ams.inec.go.tz**

**Maombi hayo yatapokelewa kuanzia tarehe 17 hadi 30 Mei, 2024.**
Taasisi au asasi ya kiraia yenye nia ya kutoa elimu ya mpiga kura inatakiwa kukidhi vigezo vifuatavyo:-

i. iwe imesajiliwa kwa mujibu wa Sheria za Tanzania;
ii. iwe imetuma maombi kupitia mfumo wa Accreditation Management System (AMS) kupitia anwani ya **https://ams.inec.go.tz**
iii. iwe imefanya kazi nchini kwa kipindi kisichopungua miezi sita tangu kusajiliwa kwake;
iv. ikiwa taasisi au asasi ya kiraia inahusisha watendaji wa kimataifa, miongoni mwa watendaji wake wakuu, wawili ambao taarifa zao zitawasilishwa wanapaswa wawe Watanzania;
v. katika utendaji wake, iwe haijahusishwa na uchochezi au kuvuruga amani;
vi. iwe na uzoefu wa kutoa elimu ya mpiga kura; na
vii. iwe tayari kujigharamia katika kutoa elimu ya mpiga kura.

Aidha, taasisi au asasi ya kiraia itakapowasilisha maombi katika mfumo, inatakiwa kutekeleza yafuatayo:-

i. kuambatisha nakala au kivuli cha cheti cha usajili;
ii. kuambatisha nakala au kivuli cha katiba ya taasisi au asasi husika;
iii. kujaza majina matatu ya viongozi wa juu wa taasisi au asasi husika;
iv. kujaza anwani kamili ya makazi na namba za simu za ofisi na za viongozi wake;
v. kuainisha vyanzo vya fedha zitakazotumika katika utelekelezaji wa jukumu la kutoa elimu ya mpiga kura;
vi. kuambatisha ratiba itakayoonesha tarehe na mahali elimu ya mpiga kura itakapotolewa katika halmashauri husika; na
vii. kuorodhesha katika mfumo watendaji watakaotoa elimu ya mpiga kura walioteuliwa na taasisi au asasi iliyopewa kibali

Tume haitahusika na utoaji wa rasilimali fedha au rasilimali nyingine kwa ajili ya kugharamia zoezi la utoaji wa elimu ya mpiga kura kwa taasisi au asasi za kiraia zitakazopewa kibali.

Limetolewa leo tarehe 17 Mei, 2024 na:

**Kailima, R. K**
**MKURUGENZI WA UCHAGUZI**

# Majaliwa aagiza takwimu za sensa 2022 zitumike kutekeleza afua za wanawake

## •Utaratibu mpya mikopo ya 10% waja

Na Mwandishi Wetu

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa amewataka wadau wanaotekeleza afua mbalimbali za wanawake watumie taarifa na takwimu za Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022 katika kuandaa mipango na mikakati ya uwezeshaji wanawake nchini.

Majaliwa pia amewataka wadau hao kuandaa mipango yao kwa kuzingatia vipaumbele vya serikali.

"Hii ni namna bora ya kuharakisha ustawi na maendeleo ya wanawake," Majaliwa alisema juzi wakati wa utoaji Tuzo ya Malkia wa Nguvu iliyofanyika jijini Mwanza.

Alisema kuwa kuanzia Julai mwaka huu, serikali itatoa utaratibu wa namna ya uendeshaji na utoaji mikopo kwa makundi ya wanawake, vijana na wenye ulemavu ili kuwawezesha kujikwamua kiuchumi.

"Nitoe rai kwa wanawake wote na makundi ya vijana na watu wenye ulemavu wazingatie utaratibu utakaotolewa na niwakumbushe kuwa fedha inayotolewa ni mikopo, si ufadhili, hivyo wanufaika wote wawajibike kuirejesha," alisisitiza.

Waziri Mkuu alisema serikali inayoongozwa na Rais Samia Suluhu Hassan, imeendelea kutoa kipaumbele katika masuala ya uwezeshaji kiuchumi kwa makundi maalum ya wanajamii, likiwamo kundi la wanawake.

Alisema serikali kwa mwaka 2023/24 imetenga Sh. bilioni 18.5 kwa ajili ya kutoa mikopo hiyo kwa riba ya asilimia saba na kufanya makubaliano na Benki ya NMB yatakayowezesha wafanyabiashara ndogo, wakiwamo wanawake, kupata mikopo yenye riba nafuu.

"Nina furaha sana kwa kuwa hamasa inayotokana na ushiriki wa Tuzo ya Malkia wa Nguvu imeendelea kuvuta wanawake wengi zaidi na kuwafanya waongeze ubora wa shughuli wanazofanya sambamba na kukuza biashara zao," Majaliwa alisema.

Alisema anafahamu kuwa moja ya malengo ya Mradi wa Malkia wa Nguvu ni kuimarisha fursa za ajira na kuwa kichocheo muhimu cha uzalishaji ajira mpya.

"Ninawapongeza sana kwa kuchangia jitihada za serikali katika kukabiliana na changamoto ya ukosefu wa ajira kwa vijana," alisema Majaliwa na kuitaja kaulimbiu ya tuzo hizo kwa mwaka huu ya "Weka Tuweke" inaleta hamasa kwa wanawake kufanya shughuli za uwekezaji na kutoa wito kwa wanawake wote kutumia kikamilifu fursa mbalimbali zilizomo nchini.

Alisema zipo fursa nyingi, zikiwamo za uchumi wa buluu na uchumi wa kidijiti ambazo zikitumiwa kikamilifu zinaweza kuwa na manufaa makubwa kwa wanawake.

Kuhusu uchumi wa kidijiti, Waziri Mkuu alisema amefarijika kwa kuwa kuna ongezeko kubwa la ushiriki wa wanawake wanaofanya biashara kupitia mitandao ya kijamii mathalani, Instagram, WhatsApp, Telegram na Tiktok.

Awali, Mwenyekiti wa Kamati ya Tuzo za Malkia wa Nguvu, Liliane Masuka, alisema mradi huo unalenga kukuza na kuongeza fursa za biashara zinazoendeshwa na wanawake ili kuleta mabadiliko chanya katika jamii.



Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Said Mtanda (wa tatu kulia), akipata maelezo ya mradi wa hoteli ya nyota tano kutoka kwa Mhandisi Helmes Pantaleo ambaye ni Meneja Miradi wa NSSF. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# RC Mwanza asema azma kuona mradi hoteli nyota tano unajengwa na NSSF unakamilika

**Na Mwandishi Wetu,** MWANZA

MKUU wa Mkoa wa Mwanza, Said Mtanda, amesema ni azma ya serikali kuona miradi ya kimkakati ukiwamo wa hoteli ya nyota tano inayojengwa na Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) jijini Mwanza inakamilika.

Mtanda alisema hayo mwishoni mwa wiki wakati alipofanya ziara ya kikazi kukagua miradi ya kimkakati.

"Nawapongeza NSSF kwa kazi nzuri na ubunifu mkubwa wa miradi ya kimkakati wanayoitekeleza sehemu mbalimbali nchini, nawaomba waendelee kuongeza kasi ya utekelezaji ili ile azma ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kuona miradi mbalimbali ya kimkakati inakamilika kama ilivyokusudiwa.

Alisema mradi wa NSSF wa hoteli ya nyota tano wa jijini Mwanza, utakapokamilika utaongeza thamani katika jiji hilo na kuhakikisha Serikali ya Mkoa itaendelea kutoa ushirikiano kwa NSSF ili mradi huo unakamilika na kuanza kutumika kama ilivyokusudiwa.

Awali, akizungumza kwa niaba ya Mkurugenzi Mkuu wa NSSF, Kaimu Mkurugenzi wa Uwekezaji, Mapesi Maagi, alisema uwekezaji wa mradi huo ni moja kati ya majukumu manne ya mfuko ambayo ni kuandikisha wanachama kutoka sekta binafsi na sekta isiyo rasmi, kukusanya michango, kuwekeza na kulipa mafao.

Maagi alimesema uwekezaji wa hoteli hiyo utakapokamilika utachochea maendeleo ya Mkoa wa Mwanza na Kanda ya Ziwa kwa ujumla kwa kuinua shughuli za kiuchumi hususan utalii hasa ikizingatiwa kuwa Mkoa wa Mwanza umepakana na Hifadhi ya Taifa ya Serengeti ambayo ipo karibu na mkoa huo.

Naye Meneja wa NSSF Mkoa wa Mwanza, Emmanuel Kahensa, alimshukuru Mkuu wa Mkoa kwa kufanya ziara hiyo ya kikazi katika mradi huo wa hoteli ya nyota tano.

Akitoa taarifa, Mhandisi Helmes Pantaleo ambaye ni Meneja Miradi wa NSSF ameelezea utekelezaji wa mradi na changamoto zote ambazo zilikuwa ni kikwazo zimetatuliwa. Mhandisi Pantaleo alisema utekelezaji unaendelea na unatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwaka huu na kuanza kazi mwezi Machi 2025.

# Wagonjwa kutoka nje ya nchi wamiminika kutibiwa JKCI

Na Joseph Mwendapole

MATIBABU ya moyo katika Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI) yanazidi kuvutia mataifa ya nje. Ndani ya kipindi cha miezi mitatu imepokea na kuwapa matibabu wagonjwa 365 kutoka nchi mbalimbali.

Hayo yalibainishwa mwishoni mwa wiki na Mkurugenzi Mtendaji wa JKCI, Dk. Peter Kisenge, alipozungumzia ujio wa wataalamu wa afya kutoka Burundi waliotembelea kwa lengo la kuangalia namna ya kushirikiana katika matibabu ya moyo.

Alisema JKCI sasa inavutia nchi nyingi kutaka kujifunza kutokana na uwekezaji wa kisasa uliofanywa na serikali pamoja na kuleta wagonjwa wao nchini.

Dk. Kisenge alisema nchi nyingi za Afrika zikitaka kuanzisha hospitali za moyo zimekuwa zinafanya ziara katika taasisi hiyo kujifunza na kupata uzoefu ili nazo ziweze kufanikiwa ikiwa ni sehemu ya mkakati wa serikali wa tiba utalii.

"Wataalamu hawa kutoka Burundi wamekuja hapa kujionea nini tunafanya, pia kuweka uhusiano nasi ili waanze kuwaleta wagonjwa kutoka Burundi kuja kutibiwa JKCI.

"Tumekuwa tunatembelewa na wataalamu kutoka nchi mbalimbali kujifunza, ikiwamo Somalia, Sierra Leone, Kenya na Burundi, alisema Dk. Kisenge.

Alisema dhana ya tiba utalii katika taasisi hiyo imeongezeka kwa kasi na kwa kipindi cha miezi mitatu wameona wagonjwa 365 kutoka nje ya nchi.

"Tumekuwa na wigo mkubwa wa kutoa huduma za kibingwa za magonjwa ya moyo, hivyo kupelekea kupata idadi kubwa ya wagonjwa kutoka nchi mbalimbali za Afrika, pia kutembelewa na wataalamu wa afya kutoka nje ya nchi ili waweze kujifunza hapa kwetu," alisema.

Dk. Kisenge alisema kupitia wagonjwa wanaotoka nje ya nchi uchumi wa nchi na wa mtu mmoja mmoja unaokua kwa kuwa wanapokuwa nchini wanajihusisha na shughuli tofauti zikiwamo za malazi, utalii na zinginezo.

Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Moyo kutoka Burundi, Constantin Nyamuzangula, alisema Tanzania imepiga hatua kubwa katika eneo la matibabu ya magonjwa ya moyo.

Alisema kupitia ziara hiyo wamejifunza kuwa JKCI inafanya upasuaji wa moyo wa aina karibuni zote. Kwao Burundi hawajaanza kufanya upasuaji wa moyo wa aina nyingi.

"Tumetembelea maeneo mbalimbali ya taasisi hii, wanaona wagonjwa wengi sana, mazingira ya hospitali pia ni mazuri, mtu akiwa hapa ni kama yupo eneo linalojihusisha na mambo mengine na si hospitali," alisema bingwa huyo.

## HABARI KASKAZINI



## DC awapa salamu 'mchwa' fedha za serikali

**NA Steven William,** MUHEZA

SERIKALI wilayani Muheza mkoani Tanga imetoa onyo la kuwachukulia hatua yeyote atakayechezea fedha za serikali au kuzembea kutekeleza miradi.

Agizo hilo limetolewa juzi na Mkuu wa Wilaya ya Muheza, Tanga, Zainab Abdallah katika kikao kazi na watumishi, kilicholenga kujadili miradi inayotekelezwa na Halmashauri ya Wilaya ya Muheza katika kipindi cha uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan.

Alisema kuwa watakaobainika kuhujumu miradi katika uongozi wa Rais Samia Suluhu hata kama watakuwa wamehamishwa kituo cha kazi watarudishwa kujibu hoja za serikali wilayani hapa.

Alisema kuwa juzi wamefanya kikao kazi cha kujadili miradi inayotekelezwa na Halmashauri ya Wilaya ya Muheza kwa miaka mitatu ya Rais Samia Suluhu.

Alisema kuwa katika kikao hicho kilichodumu mpaka saa 4:30 usiku wamewweka mikakati na maazimio ambayo yanaenda kuwa mwarobaini wa changamoto ya Wilaya ya Muheza.

Zainab alisema kuwa moja ya mikakati hiyo ni ya kutokukamilisha miradi kwa wakati, miradi kuwa chini ya viwango, fedha kuisha na miradi kutokukamilika, fedha za miradi kukaa muda mrefu kwenye akaunti bila ya kutumika.

Katibu Tawala wa Wilaya ya Muheza, Mohamed Mfaki, alisema kuwa kazi iliyobaki hivi sasa ni kuhakikisha miradi ya maendeleo inasimamiwa na kukamilika kwa haraka pamoja na kusimamia vizuri matumizi ya fedha za serikali.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Muheza, Dk. Jumaa Mhina, alisema kuwa kwa kushirikiana na timu yake ya watumishi amesikia na anakwenda kuyatekeleza maagizo hayo.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Muheza, Erasto Mhina, alisema kuwa kwa niaba ya madiwani wenzake wamejipanga kusimamia miradi katika kata zao ili iweze kukamilika kwa wakati pamoja na fedha za serikali kuhakikisha zinatumika vizuri.

# Mwanafunzi MoCU abuni mbolea kiboko ya wadudu

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

MWANAFUNZI wa Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi (MoCU), Justine Opola, amebuni mbolea ya asili, ambayo harufu yake hairuhusu mdudu kukaa kwenye mazao.

Mwanafunzi huyo wa shahada ya kwanza ya uchumi, ameibuka na ubunifu huo wa mbolea maarufu ya 'Opola' inayozalishwa kwa kutumia uchafu unaotokana na shughuli za binadamu, wanyama na mchanganyiko wa mimea tofauti.

Akizungumza juzi chuoni hapo, wakati wa maonyesho ya ubunifu wa stadi za kazi kwa wanafunzi, mwanafunzi huyo alisema mbolea hiyo, licha ya kuwa suluhisho kwenye soko la ndani la kimataifa, kushindana na vyakula vinavyozalishwa kwa kutumia mbolea za kemikali, ni rafiki kwa binadamu, kwa sababu haitumii sumu.

"Ukinyunyiza kwenye mmea, mdudu hawezi akastahimili kukaa kwenye mmea husika. Wizara ya Kilimo, tayari imeshatoa maelekezo kwa chuo, mbolea yangu ichukuliwe na kupelekwa kwenye mamlaka husika kama TPHPA (Mamlaka ya Afya ya Mimea na Viuatilifu) kwa ajili ya uhakiki na kutafutiwa hati miliki ya wazo langu," alisema.

Kaimu Makamu Mkuu wa Chuo hicho cha MoCU, Prof. Freddy Kilima, alisema kwa kuwa suala la ajira ni changamoto kwa wahitimu wengi nchini, serikali kupitia Rais Samia Suluhu Hassan, imekuwa akisisitiza umuhimu wa vijana kutafuta fursa mbalimbali zilizoko katika mazingira yao, kujiajiri pamoja na kutengeneza ajira kwa vijana wengine, chuo hicho kimekuwa kikifanya hivyo kwa miaka 12 sasa.

"Chuo kina wanafunzi ambao kwenye programu mbalimbali ambazo zimekuwa zinawajengea uwezo katika tasnia mbalimbali kubuni huduma zinazoweza kutatua changamoto mbalimbali katika jamii. Jambo hili linaendana na mpango wa serikali wa kukuza sekta binafsi na kuhamasisha ubunifu, kukuza ajira na kutatua changamoto mbalimbali, hasa ikiwamo ile ya ufinyu wa ajira kwenye sekta rasmi," alisema.

Aliongeza: "Katika tukio hili zaidi ya wanafunzi 100 kutoka programu mbalimbali wako wanaonyesha huduma na bidhaa mbalimbali walizobuni wenyewe kutokana na utashi walionao na kijasiriamali pamoja na ujuzi ambao wameupata darasani."

Alisema: "Miongoni mwa wanafunzi hawa wako wanaonyesha biashara na vipaji, utengenezaji wa bidhaa mbalimbali, uchoraji, utengenezaji wa mifumo, umahiri katika fani walizobobea, mfano ushirika na nyinginezo, kuigiza na vichekesho, muziki na maeneo mengine yaliyokatika mtambuka huo."

Mkurugenzi wa Kampuni za Marenga Investment, Joseph Kimoso, aliwafunda wabunifu hao, akiwataka kutosubiri miujiza au njia ya mkato ili kupata manufaa ya kiuchumi.

"Ukisoma kivivu utafaulu kivivu na utapoteza kabisa ile talanta uliyonayo. Nafurahi kuona watoto wadogo walivyo na bidii katika ubunifu. Tusiwaache wakae muda mrefu kwenye mambo yasiyo na tija katika uchumi. Wako watu wana GPA kubwa lakini ni wavivu na hujui wameipataje, hii inashangaza. Usipotoka huko na ukafanya kazi kwa bidii na nguvu zote labda sasa usubiri miujiza," alisema.

Zaidi aliongeza: "Naomba msiishi kwa kusubiri miujiza, fanyeni kazi za ubunifu mtajiinua kichumi, huko kwenye miujiza ni kujidanganya na kuchekewesha ndoto zao kiuchumi."


## Jinsi Ya Kununua Magazeti Ya Nipashe na The Guardian katika tovuti ya www.ippmedia.com au epaper.ippmedia.com

**Kupitia tovuti ya epaper.ippmedia.com:**

1. Utafungua tovuti ya **epaper.ippmedia.com** utachagua toleo unalotaka kununua aidha **Nipashe** au **The Guardian** kwa kuclick Read
2. Itakuletea ukurasa mwingine unaotakiwa kujaza taarifa zako na kifurushi unachotaka kujiunga. Kisha unabonyeza **"subscribe"**
3. Itakupeleka katika ukurasa wa malipo ambapo unaweza kulipa kwa **kadi ya benki** malipo kwa **mtandao wa simu** unaoutumia baada ya kujaza kwa usahihi taarifa zako na anuani
4. Kwa **namba ya simu** unachagua mtandao wa simu unatumia ambapo utaandika namba yako na kutick box la kukubali terms and conditions ndio uende **"pay via mobile"**. Itakuletea maelekezo namna ya kulipa kwa simu kulingana na mtandao unaotumia.
5. **Kwa benki** unaweka taarifa za kadi yako ndio uruhusu muamala ukatwe katika account yako baada ya kukubali terms and conditions. Ndipo utaingia katika account yako na kusoma toleo ulilolilipia
6. Malipo yakikamilika, utapokea email na message kuwa pesa imepokelewa hivyo utaingia kwa account yako na kuanza kusoma yale matoleo umeyalipia


**Na kwa tovuti ya www.ippmedia.com**

7. Unafungua website yako ya **www.ippmedia.com** upande wa kulia utaona **"E-Paper"** utabonyea na kuafuatisha hatua zote 1-6



Kwa mawasiliano zaidi Tupigie: 0677 020 701 | Subscription: 0625 174 714 | Barua pepe: customerrelations@guardian.co.tz

Nipashe The Guardian



# RC aagiza milango kituo cha afya ing'olewe

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MKUU wa Mkoa wa Shinyanga, Anamringi Macha, amebaini ubadhirifu katika ujenzi wa Kituo cha Afya Salawe wilayani Shinyanga, ikiwamo utengenezaji wa milango chini ya kiwango na matumizi makubwa ya fedha katika ujenzi wake.

Kituo hicho kinatajwa kutumia zaidi ya Sh.bilioni 1.2 na bado hakijakamilika, huku vituo vingine vikipatiwa Sh.milioni 500 hadi kukamilika na kuanza kutoa huduma.

Macha alibaini hayo juzi wakati wa ukaguzi wa maendeleo ya upanuzi wa kituo hicho na kukikuta katika hali mbaya, huku milango ikiwa imetengenezwa chini ya kiwango na kumwagiza mkandarasi kuirudia upya.

"Mradi haupo vizuri, hakuna umakini yaani zimetumika Sh. bilioni 1.2 na hakuna kinachoendelea, mradi kama umetelekezwa, milango haina ubora, halafu mnasema mnampongeza Rais Samia kwa kutoa fedha nyingi, mnampongeza Rais kwenye mambo ya ovyo hivi," alisema Macha.

Aliongeza: "Fedha zote hizi ambazo zimetumika kwenye ujenzi wa kituo hiki cha afya kingekuwa tayari kimeanza kutoa huduma kwa wananchi, mngetoa kipaumbele kwenye majengo muhimu ikiwamo la Wagonjwa wa Nje (OPD), maabara na sehemu ya kuhifadhi maiti, lakini mmejenga holela bila mipango na kama kuna pesa zimeliwa tutazitafuta tu," alisisitiza.

Aidha, aliagiza mafundi waliotengeneza milango pamoja na kupaka rangi kwenye ujenzi wa kituo hicho wafike kwa Mkuu wa Wilaya kwa hiari yao ili wahojiwe na kufanya marekebisho haraka ikiwamo kung'oa milango hiyo.

Naye Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, Kisena Mabuba, alisema mikakati ya halmashauri ambayo wameweka ili kukamilisha majengo muhimu ya kuanza kutoa huduma, wameshatenga Sh.milioni 50 ambazo watazitoa mwezi huu.

Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, Dk. Nuru Yunge, akisoma taarifa ya ujenzi wa upanuzi wa kituo hicho alisema ulianza mwaka 2021/2022 na fedha iliyotumika ni Sh. bilioni 1.2 na bado hakijaanza kutoa huduma na fedha imekwisha.

Alitaja mikakati ya halmashauri ili kukamilisha ujenzi huo na kuanza kutoa huduma za matibabu, kwamba katika mwaka 2023/24 wametenga Sh.milioni 25 kupitia mapato ya ndani na mwaka 2024/25 wametenga tena Sh.milioni 15.



Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Anamringi Macha, akikagua ujenzi wa upanuzi wa Kituo cha Afya Salawe wilayani Shinyanga juzi, alikuta milango ikiwa imetengenezwa chini ya kiwango na kuagiza ifanyiwe marekebisho ya haraka, ujenzi huo hadi sasa umeshatumia Sh.bilioni 1.2. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Wenye ulemavu wataka fursa sawa katika ajira

**Na Vitus Audax,** MWANZA

WATU wenye ulemavu mkoani Mwanza wameiomba serikali pamoja na sekta binafsi kufuata sheria za kazi katika kutoa fursa sawa za ajira kwa kila mtu, pasipo kuangalia hali yake bali kwa kufuata ujuzi alionao.

Walitoa ombi hilo kwa nyakati tofauti wakati wa Kongamano la Shirikisho la Watu Wenye Ulemavu Tanzania (SHIVYAWATA) Wilaya ya Nyamagana.

Mmoja wa kundi hilo, Janeth Mahile alisema idadi kubwa ya wenye ulemavu wamekuwa wakikosa fursa kutokana na hali walizonazo.

Mwenyekiti wa SHIVYAWATA Wilaya ya Nyamagana, Hamza Nyamakurura, alisema licha ya serikali kuweka juhudi katika uboreshaji sekta mbalimbali ikiwamo miundombinu rafiki kwao pamoja na elimu, bado upo kuna uhitaji zaidi wa kutoa ajira shindanishi kwa wenye ujuzi na taaluma husika.

Alisema hawataki kuwa ombaomba mitaani bali wanachohitaji ni ajira zinapotangazwa ibainishwe ni wenye ulemavu wangapi wanahitajika ili kuwasaidia wao kujiinua kiuchumi na kudhibiti hali duni kwao.

Hivyo, aliiomba serikali katika miundombinu ya kiuchumi inayotekelezwa nchini yakiwamo masoko kuhakikisha wanapata fursa pia za maeneo ya biashara kama zinavyotolewa kwa wengine ili wajiinue kiuchumi.

Akifungua kongamano hilo, Mkuu wa Wilaya ya Ilemela, Hassan Masala, alisema serikali inatambua uhitaji wa watu wenye ulemavu katika kupata fursa za ajira na jitihada mbalimbali za kuhakikisha wanapata fursa sawa.

"Tumewapa pia kipaumbele katika hatua za kuomba ajira ambapo mwenye ulemavu anayekidhi vigezo anatakiwa kuweka aina ya ulemavu wake ili kuiwezesha kumtambua na kumchukua wa kwanza," alisema Masala.

Aidha, alisema tatizo lililopo kwa sasa ni hali ya watu hao kutokufuata utaratibu huo, hali inayoifanya serikali ishindwe kuwatambua kama sehemu ya waombaji wenye ulemavu.

Mkurugenzi Msaidizi wa Sera na Mipango kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu, Godfrey Chambo, alizitaka sekta binafsi kutekeleza Sheria ya Watu Wenye Ulemavu Namba 9 ya Mwaka 2010 inayomtaka kila mwajiri kuhakikisha anaajiri watu watatu wenye ulemavu kati ya waajiriwa 20.

## Ufaransa yatenga bil.211/- uimarishaji majiji matatu

**Na Vitus Audax,** MWANZA

SHIRIKA la Maendeleo la Ufaransa (AFD) kwa kushirikiana na wadau wengine wamesema wanaendelea na utekelezaji wa programu ya uimarishaji usafi pamoja na uchumi kwa wajasiriamali katika majiji matatu nchini kwa gharama ya Sh. bilioni 211.6.

Programu hiyo iitwayo 'sasa towards smarter city' inatekelezwa katika majiji ya Mwanza, Tanga pamoja na Kisiwa cha Pemba inaendeshwa kwa kipindi cha miaka sita kuanzia 2021 hadi 2026, huku ikitarajiwa kuinua uchumi wa wafanyabiashara katika maeneo husika.

Akizungumza mwishoni wa wiki mkoani hapa katika ufunguzi wa Wiki ya Ubunifu Duniani uliofanyika kimkoa wilayani Ilemela, Meneja mradi wa Enabel, Kikolo Mwakasungula alisema utekelezaji wa programu hiyo unalenga zaidi kuyapangilia na kuyaweka safi majiji husika.

Alisema kwa Jiji la Mwanza unatarajia kuboresha baadhi ya masoko ya chakula likiwemo la Buhongwa ambalo litajengwa upya na kupangiliwa kukabiliana na hali ya uchafu.

Alisema soko lingine ni Buswelu pamoja na ukarabati wa Soko la Kimataifa la Samaki la Kirumba kwa lengo la kuhakikisha ubora wa chakula, kudhibiti uchafuzi pamoja na kusaidia wafanyabiashara kufanya kazi katika mazingira salama.

"Tulibaini kuwa Mwanza kuna ng'ombe wengi ambao wanahudumia Tanzania na baadhi ya mataifa jirani, hivyo tutajenga na kurekebisha machinjio yakiwemo yale ya Nyakato ili kazi hiyo ifanyike katika maeneo salama," alisema.

Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Said Mtanda akifungua maadhimisho hayo aliliagiza Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO), kushirikiana na wadau hao kuhakikisha wanatekeleza majukumu yao.

"Nchi zaidi ya 26 za ulaya zimeungana kuhakikisha zinalisaidia Jiji letu linakuwa janja, hivyo serikali itashirikiana nao kikamilifu kupitia SIDO katika kubaini taasisi za wajasiriamali zisizo wababaishaji ili kufanikisha malengo," alisema Mtanda.

Meneja wa SIDO Mkoa wa Mwanza, Bakari Songwe alisema kupitia programu hiyo wamepewa jukumu la kuandaa taasisi 100 za wajasiriamali zitakazozalisha ajira 400.

**Alisema kwa Jiji la Mwanza unatarajia kuboresha baadhi ya masoko ya chakula likiwemo la Buhongwa ambalo litajengwa upya na kupangiliwa kukabiliana na hali ya uchafu.**

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM

# HOTUBA YA WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM, MHE. DKT. DOROTHY O. GWAJIMA (MB), KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2024/25.



Mhe. Dkt. Dorothy Gwajima (Mb)
Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum



Mhe. Mwanaidi Ali Khamis (Mb)
Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wanawake na Makundi Maalum



Dkt. Seif Abdallah Shekalaghe
Katibu Mkuu wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum



Amon Anastaz Mpanju
Naibu katibu Mkuu wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum

# HOTUBA YA WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM, MHE. DKT. DOROTHY O. GWAJIMA (MB), KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2024/25.

## A. UTANGULIZI

*Mheshimiwa Spika,* kufuatia taarifa iliyowasilishwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii ndani ya Bunge lako Tukufu, ambayo imechambua Bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, ninaomba kutoa hoja kwamba sasa Bunge lako likubali kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum **(Fungu 53)** kwa mwaka 2023/24 na Vipaumbele vya Wizara kwa mwaka 2024/25. Aidha, ninaliomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Kawaida pamoja na Miradi ya Maendeleo ya Wizara kwa mwaka 2024/25.

*Mheshimiwa Spika,* awali ya yote napenda kumshukuru Menyezi Mungu kwa kunijalia afya njema na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu ili kuwasilisha hotuba yangu siku ya leo. Pia, nitumie fursa hii kumshukuru sana **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan,** Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kuendelea kutuongoza vyema kwa mafanikio makubwa katika nyanja mbalimbali kwa kipindi hiki cha miaka

mitatu ya uongozi wake. Kipekee niendelee kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kuniamini kuiongoza Wizara hii. Natambua kuwa Mheshimiwa Rais ana matarajio makubwa ya kuona hali ya usawa wa kijinsia hapa nchini inaimarika na utoaji wa huduma za maendeleo na ustawi wa jamii unafanyika kwa kasi kubwa na ufanisi. Ninamuahidi kwamba nitaendelea kutimiza majukumu yangu kwa weledi mkubwa ili kuhakikisha kwamba matarajio yake yanafikiwa kikamilifu.

***Mheshimiwa Spika,*** pia, napenda kumpongeza na kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuwa mstari wa mbele katika jitihada za kuboresha huduma za maendeleo na ustawi wa jamii, kuhimiza usawa wa kijinsia, uwezeshaji wanawake kiuchumi pamoja na kuzingatia haki za wazee, wanawake, wanaume na watoto katika jamii. Hivyo, Wizara yangu itaendelea kutekeleza kikamilifu maelekezo anayoyatoa mara kwa mara.

***Mheshimiwa Spika,*** nitumie fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake mahiri uliowezesha kuleta tija na ufanisi katika utendaji na kuimarisha huduma zinazotolewa katika Sekta ya Maendeleo na Ustawi ya Jamii. Aidha, ninampongeza kwa hotuba yake aliyoiwasilisha kwenye Bunge lako Tukufu tarehe 15 Aprili, 2024 ambayo imetoa mwelekeo wa majukumu yatakayotekelezwa na Serikali katika mwaka 2024/25.

***Mheshimiwa Spika***, kwa namna ya kipekee naomba nimpongeze Mheshimiwa Dotto Mashaka Biteko (Mb), Naibu Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Waziri wa Nishati kwa kuaminiwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuteuliwa kuwa Naibu Waziri Mkuu. Aidha, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum inaahidi kuendelea kumpa ushirikiano katika utekelezaji wa majukumu yake.

*Mheshimiwa Spika,* ninapenda kukupongeza wewe binafsi kwa uongozi wako mahiri na weledi wa kuendelea kuliongoza Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, ninampongeza **Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu (Mb),** Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uchapakazi wake uliotukuka. Mwenyezi Mungu awajalie utashi, weledi na ufanisi mkubwa katika kuliongoza Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

*Mheshimiwa Spika,* vilevile, nawapongeza **Mheshimiwa Dkt. Joseph Mhagama (Mb)**, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria na **Mheshimiwa Deo Mwanyika (Mb)**, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo kwa kuchaguliwa kuwa Wenyeviti wa Bunge. Nawatakia majukumu mema katika kuliongoza Bunge.

*Mheshimiwa Spika,* Kipekee namshukuru na kumpongeza **Mheshimiwa Mwanaidi Ali Khamis (Mb),** Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kwa ushirikiano mkubwa anaonipa katika kutekeleza majukumu yangu ya kila siku.

*Mheshimiwa Spika,* nitumie nafasi hii, kumshukuru **Mheshimiwa Angellah Kairuki (Mb),** Waziri wa Wizara ya Maliasili na Utalii ambaye pia ni Mwenyekiti wa Kamati ya Ushauri ya Utekelezaji wa Jukwaa la Kizazi Chenye Usawa kwa jitihada zake za dhati katika kufikia kizazi chenye usawa nchini. Chini ya uenyekiti wake, Kamati imeweza kusimamia utekelezaji wa Programu ya Kizazi Chenye Usawa (Tanzania Generation Equality Programme - TGEP, 2021- 2026) inayoainisha afua muhimu zitakazo tekelezwa na Wizara za Kisekta na kuhakikisha kuwa hakuna mtu anayeachwa nyuma katika maendeleo na ujenzi wa Taifa letu.

*Mheshimiwa Spika,* ninapenda kuwashukuru Mawaziri wenzangu kwa ushirikiano wanaonipatia ambao unaiwezesha Wizara yangu kuendelea kuimarisha na kuboresha utoaji wa huduma za maendeleo na ustawi wa jamii. Wizara itaendelea kushirikiana nao na kuhakikisha tunatimiza dhamira ya **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan,** Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya kuhakikisha mafanikio katika Nyanja za Maendeleo na Ustawi wa Jamii yanafikiwa.

*Mheshimiwa Spika*, Kipekee ninapenda kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii, chini ya **Mwenyekiti Mheshimiwa Fatma Hassan Toufiq (Mb)** na **Makamu wake, Mheshimiwa Riziki Said Lulida (Mb)** kwa ushauri na maelekezo waliyoyatoa wakati wa maandalizi ya Bajeti hii. Vilevile, ninawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa

ushirikiano mzuri wanaotupatia wenye lengo la kuboresha huduma za ustawi na maendeleo ya jamii.

*Mheshimiwa Spika*, naomba kutoa pole kwa Serikali na Chama cha Mapinduzi kufuatia kifo cha cha **Ndugu, Ally Hassan Mwinyi** aliyekuwa Rais wa awamu ya Pili wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Ndugu **Edward Ngoyai Lowassa** Waziri Mkuu Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, nitoa pole kwako, Spika na Waheshimiwa Wabunge wa Bunge lako Tukufu kwa kuondokewa na wapendwa wetu **Mheshimiwa Francis Leonard Mtega** aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Mbarali na **Mheshimiwa Ahmed Yahaya Abdul-wakil** aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Kwahani Zanzibar.

*Mheshimiwa Spika*, napenda pia kutoa pole kwa wakazi wa Wilaya ya Hanang' pamoja na wananchi wa Mkoa wa Manyara kwa ujumla kufuatia maporomoko ya matope yaliyotokea Desemba 3, 2023 kutokana na mvua kubwa na kusababisha vifo, majeruhi, upotevu wa mali na makazi. Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu wote mahali pema peponi. Amina.

*Mheshimiwa Spika,* baada ya kutoa maelezo ya awali, ninapenda sasa kutoa maelezo kuhusu utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2023/24, Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi pamoja na Maombi ya Fedha kwa ajili ya kutekeleza Vipaumbele vya Wizara kwa mwaka 2024/25.

## B. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA WIZARA KWA MWAKA 2023/24

*Mheshimiwa Spika,* Wizara imeendelea kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia Sera, Mpango Mkakati pamoja na Makubaliano ya Kitaifa na Kimataifa yenye lengo la kuimarisha utoaji wa huduma za maendeleo na ustawi wa jamii nchini. Sera hizo ni pamoja na Sera ya Maendeleo ya Jamii (1996); Sera ya Taifa ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (2001); Sera ya Taifa ya Wazee (2003), Sera ya Maendeleo ya Mtoto (2008) na Sera ya Taifa ya Jinsia na Maendeleo ya Wanawake (2023). Vilevile, katika kuandaa mpango na bajeti, Wizara imezingatia Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2020, Dira ya Taifa ya Maendeleo (2025), Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/22 - 2025/26), Malengo ya Maendeleo Endelevu (Sustainable Development Goals, 2030); na Agenda ya Afrika Tuitakayo (2063). Aidha, Wizara inatekeleza majukumu yake kwa kuzingatia Ahadi za Nchi katika Jukwaa la Kizazi Chenye Usawa (Generation Equality Forum – GEF, 2021 – 2026).

*Mheshimiwa Spika,* katika mwaka 2023/24, Wizara ilipanga kutekeleza vipaumbele mbalimbali vyenye lengo la kuboresha utoaji wa huduma za maendeleo na ustawi wa jamii katika maeneo yafuatayo: -

i) Kuratibu afua za kukuza usawa wa kijinsia na uwezeshaji wanawake kiuchumi (Generation Equality Forum - GEF);
ii) Kuratibu utekelezaji wa Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto (MTAKUWWA);
iii) Kutekeleza Mpango wa Taifa wa Kuhamasisha na Kusimamia Maendeleo Ngazi ya Msingi wa mwaka 2022/23 - 2025/26 (Bottom Up);
iv) Kukuza ari ya jamii kushiriki katika kupanga na kutekeleza miradi ya maendeleo;
v) Kutambua na kuratibu Makundi Maalum wakiwemo wafanyabiashara ndogondogo ili kuboresha mazingira ya biashara zao;
vi) Kuboresha mazingira ya kufundisha na kujifunzia katika Taasisi ya Ustawi wa Jamii, Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru na Vyuo vya Maendeleo ya Jamii;
vii) Kuratibu utoaji wa huduma za msingi kwa watu wenye mahitaji maalum ikiwemo huduma za msaada wa kisaikolojia kwa manusura wa majanga mbalimbali na makundi mengine yenye uhitaji katika jamii;
viii) Kuratibu na kuwezesha upatikanaji wa haki za watoto na huduma za ustawi wa jamii kwa wazee;
ix) Kuimarisha mifumo ya malezi, ulinzi na maendeleo ya watoto na familia; na
x) Kuimarisha utendaji kazi wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ili mchango na ushiriki wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika maendeleo ya taifa uweze kutambulika na kuwa na tija kwa Jamii.

*Mheshimiwa Spika,* katika mwaka 2023/24, Wizara ilipanga kukusanya kiasi cha **Shilingi 8,500,000,000.00** kutoka kwenye ada za wanafunzi, uuzaji wa Mitaala ya kufundishia fani za Maendeleo ya Jamii na Ustawi wa Jamii pamoja na malipo ya hosteli katika vyuo nane (8). Vyanzo vingine ni mapato ya ada ya

usajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, ada za mwaka na faini kwa mujibu wa Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Sura ya 56 pamoja na marekebisho yake na mapato mengineyo. Hadi kufikia mwezi Aprili 2024, Wizara imefanikiwa kukusanya kiasi cha **Shilingi 3,184,370,155.50** sawa na asilimia **37.46** ya makadirio ya mapato kama inavyoonesha katika ***Jedwali Na. 1*** **ukurasa wa 9.**

*Mheshimiwa Spika,* kutofikiwa kwa lengo la Makusanyo ya Mapato kunatokana na sababu zifuatazo; wanafunzi kutoripoti wote kama ilivyokadiriwa; Kumekuwa na upungufu wa wanafunzi 1,691 ambao hawajaripoti kutoka katika makadirio ya 7,190; Kutokukamilika kwa malipo ya Ada ya Malazi kwa wanafunzi vyuoni, Kuchelewa kuanza kwa utaratibu wa usajili na utambuzi wa wafanyabiashara ndogondogo ambao ulianza mwezi Machi, 2024 na hadi sasa tumeweza kukusanya kiasu cha shilingi 64,284,000 kati ya Shillingi Billioni moja. Aidha, umefutaji wa usajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali 14 kutokana na ukiukwaji wa Sheria na Kanuni na Miongozo inayosimamia shughuli za Mashirika hayo, imechangia kupunguza mapato.

*Mheshimiwa Spika,* Wizara inafanya jitihada kuhakikisha makusanyo yote yaliobaki yanakusanywa katika kipimdi kilichobakia ili kuweza kuongeza makadirio ya makusanyo yaliokadiriwa kwa mwaka 2023/2024.

*Mheshimiwa Spika,* katika mwaka 2023/24, Wizara iliidhinishiwa na Bunge lako Tukufu kiasi cha **Shilingi 74,223,193,000.00.** Kati ya fedha hizo, **Shilingi 43,664,963,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ambapo **Shilingi 26,577,510,000.00** ni fedha za Matumizi Mengineyo (OC) na **Shilingi 17,087,453,000.00** ni kwa ajili ya Mishahara. Aidha, kiasi cha **Shilingi 30,558,230,000.00** kilikuwa ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ambapo **Shilingi 26,800,000,000.00** ni fedha za ndani na **Shilingi 3,758,230,000.00** ni fedha za nje.

*Mheshimiwa Spika,* Hadi kufikia mwezi Aprili, 2024, Wizara imepokea jumla ya **Shilingi 30,114,668,978.89** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida sawa na asilimia 68.97. Kati ya Fedha zilizopokelewa, **Shilingi 15,640,771,358.89** ni Matumizi Mengineyo na Shilingi **Shilingi 14,473,897,620.00** ni Mishahara. Aidha, hadi kufikia Aprili, 2024, Wizara imepokea Fedha za Maendeleo **Shilingi 4,949,880,000.00** sawa na asilimia 16.20. **Shilingi 4,883,800,000.00** ni Fedha za Ndani na **Shilingi 66,080,000.00** ni Fedha za Nje, kama inavyoonesha katika Jedwali Na. 2 **lililopo ukurasa wa 11.**





C. UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA (FUNGU 53)

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2023/24, utekelezaji wa majukumu ya Wizara ulilenga kuimarisha ushiriki wa jamii katika shughuli za maendeleo, utambuzi na uratibu wa Makundi maalumu, kuimarisha upatikanaji wa haki na maendeleo ya mtoto, kuboresha huduma za ustawi wa jamii, kuleta usawa wa kijinsia na uwezeshaji wa wanawake kiuchumi, kuratibu utekelezaji wenye ufanisi wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na kuratibu utekelezaji wa Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto (MTAKUWWA) na Uratibu wa utekelezaji wa majukumu haya ulifanywa na Wizara kwa kushirikiana na Taasisi zake pamoja na wadau mbalimbali.

**ENEO LA 1: MAENDELEO YA JAMII**

***Mheshimiwa Spika,*** Dhana ya Maendeleo ya jamii ni kuwashirikisha wananchi kujiletea maendeleo yao wenyewe kwa kutumia rasilimali zilizopo na kwa kuzingatia mahitaji na vipaumbele vyao, ambapo maafisa maendeleo ya jamii hushirikiana nao kwa kuwapatia utaalamu wa namna ya kufanikisha shughuli za maendeleo yao. Kupitia dhana hii, Wizara imeendelea kutekeleza programu ya Amsha Ari ya Jamii na Mpango wa Taifa wa kuhamasisha na Kusimamia Maendeleo Ngazi ya Msingi ambao ulianza 2022/23 kwa ushirikiano wa jamii na Wataalam wa Maendeleo ya Jamii kutoka katika Halmashauri zote nchini. Wataalamu wa Maendeleo ya Jamii wameendelea kutoa mchango wao wa utaalam katika kutekeleza Sera ya Maendeleo ya Jamii kwa kupitia Programu ya Kuamsha Ari ya Jamii ambayo inalenga kukuza moyo wa uzalendo, kufanya kazi kwa bidii ili kujiletea maendeleo ikiwemo kampeni ya kitaifa ya ujenzi wa Makazi Bora.

***Mheshimiwa Spika***, Wizara kwa kushirkiana na Wizara za Kisekta, imeendelea kutekeleza Kampeni endelevu ya Ujenzi wa Nyumba Bora zenye gharama nafuu katika maeneo yenye makazi duni inayotumia mifumo ya asili ya kusaidiana miongoni mwa jamii. Mafaniko ya zoezi hili yanategemea ari ya wananchi, uongozi bora na juhudi za Wataalamu wa Maendeleo ya Jamii. Kupitia kampeni hiyo, idadi ya nyumba bora imeongezeka kutoka nyumba 5,732 kwa 2022/23 hadi 11,883 kufikia Aprili, 2024, sawa na ongezeko la nyumba 6,151.

***Nitumie fursa hii kuishukuru Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Miongozo ya Kisera na OR-TAMISEMI kwa kusimamia utekelezaji wa Kampeni hii kupitia maafisa maendeleo ya Jamii.***

***Mheshimiwa Spika,*** miradi mingine iliyotekelezwa kupitia kampeni ya Amsha Ari, ni utekelezaji wa ukamilishaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo katika Mikoa yote ya Tanzania Bara. Miradi hiyo ni Pamoja na ile ya Afya na Elimu ambapo jumla ya miradi 29,641 imetekelezwa, ikiwemo ukamilishaji wa ujenzi wa vituo vya kutolea huduma za afya 6,761 (Zahanati 5,887 na Vituo vya afya 874), ujenzi wa madarasa ya shule za msingi na madarasa ya awali 17,986 na madarasa ya shule za sekondari 4,894 kama ilivyotajwa na Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa (Mb), Waziri wa OR TAMISEMI wakati akiwasilisha Bungeni mkadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2024/25. Ni dhahiri, uwepo wa Maafisa Maendeleo ya Jamii wa kutosha utaongeza kasi na ari ya wananchi kushiriki na kumiliki shughuli za maendeleo. Shukrani kwa Mhe Rais kwa kuongeza ajira 762 za Maafisa Maendeleo ya Jamii mwaka 2023/24 hivyo, kuwezesha kufikia idadi ya maafisa 3,675 (69.4%) kati ya 5296 wanaohitajika jambo litakalochochea zaidi uwajibikaji ngazi ya msingi.

***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na OR-TAMISEMI, Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru pamoja na Chama cha Wataalam wa Maendeleo ya Jamii Tanzania (Community Development Professional Association of Tanzania - CODEPATA) ilifanya kongamano la wataalam wa Maendeleo ya Jamii lililofanyika katika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Arusha (Arusha International Conference Center - AICC) tarehe 20 – 22 Novemba, 2023. Kongamano lililenga kufanya tathimini ya mchango wa maendeleo ya jamii katika kuchochea na kukuza ari ya jamii kujiletea maendeleo endelevu pamoja na kubadilishana uzoefu na mbinu mpya zinazotumika katika kukabiliana na changamoto za jamii na kuwafanya wananchi kuwa kitovu cha maendeleo; kupokea na kujadili mifano mizuri ya kuwezesha wananchi; kujenga uwezo wa washiriki kupitia mada mbalimbali zinazohusiana na maendeleo ya jamii. Aidha, Kaulimbiu iliyoongoza kongamo hilo ni "Sekta ya Maendeleo ya Jamii: Msingi Imara wa Uwezeshaji wa Wananchi." Kongamano hilo pia lilikua ni kuadhimisha miaka 60 ya Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru na jumla ya Wataalam 700 walishiriki.

***Mheshimiwa Spika,*** Wizara yangu pia ina jukumu la kuzalisha wataalamu wa wanaotekeleza afua za maendeleao ya jamii na ustawi wa jamii, ili kuweza kuongeza idadi ya wataalamu hawa katika sekta hii. Wizara imefanya mapitio ya Mitaala inayotumika kutoa mafunzo ya taaluma kwa ngazi ya Astashahada hadi Stashahada. Mitaala hiyo imeandaliwa ikilenga kuwapa Wahitimu maarifa na ujuzi unaoakisi mahitaji ya soko la Ajira, Mahitaji ya Sekta na mabadiliko ya Sayansi na Teknolojia. Na hadi kufikia Aprili 2024, jumla ya Vyuo 67 (12 vya Serikali na 55 binafsi) vinavyotoa Mafunzo ya Programu ya Maendeleo ya Jamii nchini, ambapo Vyuo vyote vinavyotoa kozi ya maendeleo ya jamii, Pamoja na ufundi kwa kutumia mitaala hii iliyoboroshwa.

***Mheshimiwa Spika,*** Napenda kutoa shukrani za dhati kwa Mhe Rais, kwa kutupatia fedha za kuboresha miundombinu ya vyuo hivyo. Hali hii imetuwezesha kuongeza idadi ya udahili wa wanafunzi kutoka wanafunzi 5,255 (Me 2,089 na Ke 3,166) mwaka 2022/23, hadi wanafunzi 5,499 (Me 1,966 na Ke 3,533) kwa mwaka 2023/24 sawa na ongezeko la wanafunzi 244 ambayo ongezeko la asilimia 4.6. Aidha, mwaka 2022/23, wanafunzi 4,978 (Me 1,875 na Ke 3,103) walihitimu katika Vyuo vya Maendeleo ya Jamii ikilinganishwa na wanafunzi 4,710 waliohitimu mwaka 2021/22 sawa na ongezeko la asilimia 5 ya wahitimu.

***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia vyuo vyake inatekeleza programu ya uanagenzi kwa wanafunzi waliohitimu mafunzo katika Vyuo vyetu. Wahitimu hawa huunganishwa na Makampuni, Mashirika na Taasisi mbalimbali kwa lengo la kuwapa ujuzi na stadi mbalimbali zitakazowawezsha kukabiliana na changamoto za soko la ajira. Maeneo waliopatiwa ujuzi ni Pamoja na Ujenzi wa miradi ya maji, Material Testing, Road Construction na Building construction. Katika mwaka wa fedha 2023/24 jumla ya wanafunzi 2,200 walijiunga na program hiyo ambapo, kati yao wanafunzi 1,104 sawa na asilimia 50.2 walifanikiwa kuhitimu mafunzo. Aidha, wanafunzi 1,096 sawa na asilimia 49.8 wanaendelea na mafunzo hayo. Kutokana na umuhimu wa program hii, Wizara inaendelea kuhimiza wanafunzi/wahitimu wa Vyuo Jamii kujiunga na progamu hii ili kupanua fursa ya kuajirika, kujiajiri na kuajiri wengine. Pia, Katika mwaka wa fedha 2023/24 bunifu mbalimbali zinazolenga kutatua changamoto za kijamii ziliibuliwa. Bunifu hizo zimeainishwa kwenye **Ukurasa…….**

**ENEO LA 2: KUTAMBUA NA KURATIBU WA SHUGHULI ZA KIUCHUMI ZA MAKUNDI MAALUM**

Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kutambua, kuratibu na kusimamia mipango mbalimbali ya kuwezesha na kuendeleza Makundi Maalum katika mambo mbalimbali zikiwemo shughuli za kiuchumi. Makundi yanayolengwa ni wafanyabiashara ndogondogo wote wakiwemo Machinga, Mama/Baba Lishe, Waendesha Bodaboda na Bajaji. Makundi haya yanakabiliwa na changamoto mbalimbali zikiwemo kutofikia fursa za kiuchumi kama kupata mikopo kutoka kwenye taasisi za fedha. Kupata maeneo wezeshi ya kufanyia biashara zao, kuwepo kwa ofisi zao rasmi kuwawezesha kukutana na kuratibu masuala yao wenyewe.

***Mheshimiwa Spika,*** katika kuwaondolea changamoto hizo. Serikali imefanya yafuatayo; Kukamilisha Mpango wa kutoa mikopo kwa kundi hili kupitia taasisi za kifedha ambapo tarehe 06 Mei 2024 Wizara imeingia mkataba wa makubaliano na benki ya NMB ambayo itatoa mikopo kwa wafanya biashara hawa kwa mujibu wa mwongozo ulioandaliwa na pande zote mbili. Kupitia makubaliano haya, na kwa mwaka wa 2023/2024 serikali itaipatia benki ya NMB kiasi cha shilingi bilioni 18.5 kwa ajili kwa ya kutoa mikopo yenye riba nafuu ya (7%).

***Mheshimiwa Spika***, ili kuwezesha zoezi la utambuzi na usajili kutekelezwa kwa urahisi nchi nzima, Wizara imekamilisha mafunzo kwa wataalamu wa maendeleo ya jamii, maafisa biashara na maafisa TEHAMA wapatao 660 kutoka ngazi za Mikoa, Halmashauri, Miji, Manispaa na Majiji Tanzania Bara. Na tayari zoezi la utambuzi na usajili limeanza Machi, 2024 na linaendelea katika Halmashauri zote nchini kupitia Maafisa hao na tayari hadi kufikia Aprili 2024, wafanyabiashara ndogondogo 11,003 (Me 4,079 na Ke 6,924) wamesajiliwa kwenye mfumo huo wakisubiriwa kukamilisha hatua ya malipo ya shilingi elfu ishirini (20,000) na baada ya hapo atapatiwa kitambulisho kitakachomuwezesha kutambuliwa wakati wa kwenda kuomba mkopo.

***Mheshimiwa Spika,*** Eneo lingine muhimu la kuwezesha kundi hili kiuchumi ni kuwapatia maeneo rasmi ya kufanyia biashara ili kuwaondolea usumbufu na bughudha kwa kuweka mazingira wezeshi ya kupata wateja. Wizara kwa kushirikiana na OR – TAMISEMI imeendelea kuboresha mazingira ya kufanyia biashara kwa wafanyabiashara ndogondogo. Taarifa kutoka OR – TAMISEMI inaonesha kuwa, hadi kufikia Aprili, 2024 jumla ya masoko 367 yamejengwa na kuboreshwa katika maeneo mbalimbali nchini. Uwepo wa masoko hayo yamewezesha jumla ya wafanyabiashara ndogondogo 136,041 kuendesha biashara zao katika mazingira rafiki. Masoko 16 kati ya masoko hayo yamejengwa na kuboreshwa kwa fedha zilizotolewa na Mheshimiwa Rais, Shilingi Bilion 5. Masoko hayo 16 kama yalivyoainishwa kwenye Jedwali Na.4 Ukurasa wa.......

**ENEO LA 3: HAKI NA MAENDELEO YA MTOTO**

***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inalo jukumu la kusimamia na kuratibu maendeleo ya mtoto Pamoja na upatikanaji wa haki za msingi kwa mtoto kama zilivyoainishwa katika Mikataba ya Kimataifa, Kikanda na Kitaifa, Sera ya Maendeleo ya Mtoto ya mwaka 2008 na Sheria ya Mtoto Na. 21 ya mwaka 2009 pamoja na marekebisho yake ya mwaka 2019.

***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na Wizara za kisekta pamoja wadau wa maendeleo imeendelea kutekeleza afua mbalimbali zinazolenga kuimarisha mifumo kwa kufanya marekebisho ya kisheria na kanuni. Marekebisho ya sheria na kanuni hizo ni pamoja na Sheria ya Mtoto-Sura 13, Sheria ya Ushahidi, Sura ya 6 na Sheria ya Makosa Mtandao - Sura ya 443 kwa lengo la kumlinda mtoto nje na ndani ya Mtandao. Wizara pia imerekebisha Kanuni ya Kusimamia Vituo vya Kulea Watoto Wachanga na Wadogo Mchana, Kanuni za Makao ya Watoto, na Kanuni za Kuasili na Malezi ya Kambo ili kuhakikisha mazingira ya malezi ya mtoto wa Kitanzania ni salama kwa makuzi stahiki.

***Mheshimiwa Spika,*** hali kadhalika Wizara kwa sasa inashirikiana na Wizara nyingine za Kisekta kuhakikisha inapitia sheria ya kumlinda mtoto njiti. Lengo la marekebisho ya sheria hii ni kumuongezea muda mama aliyejifungua mtoto njiti ili kuweza kupata muda stahiki na wa kutosha wa kumhudumia mtoto vizuri tofauti na sheria zilivyo kwa sasa.

***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ilizindua Kampeni ya Kitaifa ya Ulinzi na Usalama wa Mtoto Mtandaoni tarehe 10 Februari, 2024 Jijini Dodoma ambapo wadau zaidi ya 460 walishiriki. Lengo la kampeni hiyo ni kuelimisha watoto, wazazi, walezi, walimu, viongozi wa dini, viongozi wa Taasisi zisizo za Serikali, Wizara za kisekta, na jamii kuhusu kuwalinda watoto dhidi ya vitendo vya ukatili mitandaoni pamoja ukatili wa aina nyingine.

***Mheshimiwa Spika,*** katika siku za hivi karibuni tumeshuhudia aina nyingine ya ukatili wa watoto kupitia Tasnia ya Sanaa ambapo watoto wanashirikishwa kwenye matamasha ya usiku wakihusishwa katika michezo na shughuli za maonesho ya mitindo, sherehe za harusi na shughuli nyingine za starehe hasa nyakati za usiku hali ambayo inachangia mmomomyoko wa maadili na pia ni kinyume cha Sheria ya Mtoto kifungu cha 158(1)(b).

***Mheshimiwa Spika,*** Katika kukabiliana na suala zima la mmomonyoko wa maadili, Serikali imeunda Kamati Maalum inayojumuisha Wizara yangu pamoja na Wizara nyingine za Kisekta, na Taasisi za Serikali zilizo chini ya Wizara hizi. Lengo la kamati hii, ni kubaini vyanzo vya mmomomyoko wa maadili kwa ujumla ukiwemo ule wa watoto, kutambua ukubwa wa tatizo na kuandaa mpango kazi wa kutekeleza ili kuzuia na kumaliza tatizo hili. Aidha, mbinu mbalimbali zitatumika katika kukabiliana na tatizo hili na Taarifa ya utekelezaji itakuwa inatolewa.

***Mheshimiwa Spika,*** suala la kukabiliana na ukatili dhidi ya watoto ni jukumu la kila mmoja wetu, katika kutimiza azma hiyo, Wizara inashirikiana na vikundi mbalimbali vya kijamii kwa hiari vikiwemo SMAUJATA (Mashujaa wa Maendeleo na Ustawi wa Jamii), SAWATA (Sauti ya Watoto Tanzania), Malezi Bora Network, FAGDI (Foundation for Ambassodors Gender Development Initiatives) na vingine kadhaa, kupitia Kampeni ya Wizara kwa ushirikiano na SMAUJATA yenye lengo la kuelimisha watoto na jamii katika kukabiliana na vitendo vya ukatili hadi kufikia Aprili, 2024 jumla ya wananchi 10,525 wamejiunga na kikundi hiki katika mikoa 26 ya Tanzania Bara na matokeo mojawapo ni jumla ya matukio 799 ya ukatili dhidi ya watoto yameibuliwa kuwasilishwa kwenye mamlaka za kusimamia sheria kwa hatua zaidi.

***Mheshimiwa Spika,*** Hadi kufikia Aprili 2024, jumla ya vituo 3,862 vya kulelea watoto wadogo mchana vimesajiliwa vyenye jumla ya watoto 397,935 (Me 175,517 Ke 222,418) na vituo vya Kijamii 206 (vikiwemo 30 vya mfano) vyenye jumla ya watoto 11,675 (Me 4,833 na Ke 6,842), ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2022/2023 ambapo kulikuwa na jumla ya vituo 3,033 na vya kijamii 200 vilivyokuwa na jumla ya watoto 184,606 (Me 86,832 na Ke 97,774), na hivyo kuwa na ongezeko la vituo 829 sawa na asilimia 21.5 na ongezeko la watoto 225,003 sawa na asilimia 55. Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba, Tanzania ni miongoni mwa nchi za mwanzo katika





Afrika zilizoandaa Programu Jumuishi ya Taifa ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto mwaka 2021 baada tu ya mwongozo wa kimataifa kutoka mwaka 2018. Kutokana na utayari huo na mafanikio yaliyopatikana katika kuratibu utekelezaji wa programu hii, Tanzania ilipewa Heshima ya kuandaa mkutano wa Kimataifa wa Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto kwa Nchi za Ukanda wa Afrika Mashariki uliofanyika kuanzia tarehe 11 hadi 14 Machi, 2024 Jijini Dar Es Salaam na ulihudhuriwa na jumla ya washiriki 1,300 kutoka, Nchi za Afrika Mashariki, Bara la Afrika, Amerika, Ulaya na Asia.

Mh*eshimiwa Spika* Hadi kufikia Aprili, 2024 jumla ya Vijana balehe 983,487 (wavulana 261,293, Wasichana 722,194) walipatiwa huduma za upimaji wa VVU na kati ya hao waliopatikana na maambukizi walikuwa 6,154 sawa na asilimia 8.5 ya vijana balehe walioopima, ambapo Wavulana walikuwa 772 sawa na asilimia 12.5, na Wasichana 5,382 sawa na asilimia 87.5. Waathirika wote waliunganishwa na huduma za matibabu (CTC). Aidha, Jumla ya Vijana 8,380,871 (wavulana 5,394,334 na Wasichana 2,986,537) walipata elimu ya Afya ya Uzazi kwa lengo la kuwakinga na mimba za utotoni na athari nyingine zinazotokana na uzazi usio salama.

*Mheshimiwa Spika,* Katika kukabiliana na mila na Suala la kukabiliana na mila na desturi zenye madhara kwa Watoto na jamii. Wizara imeendelea kuratibu utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Kutokomeza Ukeketaji wa mwaka 2020/21-2024/25 wenye lengo la kutokomeza vitendo vya ukeketaji kwa watoto wa kike na wanawake nchini. Takwimu zinaonesha kupungua kwa vitendo vya ukeketaji nchini kutoka asilimia 10 kwa mwaka 2015/2016 hadi asilimia 8 kwa mwaka 2022/2023. Ingawa bado baadhi ya mikoa kiwango cha ukeketaji ni kikubwa mfano, Arusha (43%), Manyara (43%), Mara (28%), Singida (20%), Tanga (19%), Dodoma (18%), Iringa (12%), Morogoro (10%), Kilimanjaro (9%), Njombe (7%), Pwani (5%) na Mbeya (3%). Mikoa mingine, ukeketaji upo chini ya asilimia 1. Wizara inaendelea na utekelezaji wa Mkakati huo ili kufikia lengo la kupunguza vitendo vya ukeketaji hadi asilimia 5 ifikapo mwaka 2025.

**ENEO LA 4: HUDUMA ZA USTAWI WA JAMII**

*Mheshimiwa Spika,* Wizara ina jukumu la kusimamia, kuratibu na kutoa huduma za Ustawi wa Jamii hapa nchini zikiwemo: haki, matunzo na ulinzi kwa wazee; watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi; watoto wanaoishi na kufanya kazi mitaani; watoto walio katika mkinzano na sheria; huduma kwa waathirika wa ukatili wa kijinsia na waathirika wa usafirishaji haramu wa binadamu; huduma za msaada wa kisaikolojia na kijamii. Majukumu haya yanatekelezwa na wataalam wa Ustawi wa Jamii kwa mujibu wa Sera, Sheria, Kanuni na Miongozo mahsusi inayoongoza utoaji wa huduma za Ustawi wa Jamii.

*Mheshimiwa Spika,* Wizara imeendelea kusimamia na kuratibu utambuzi na utoaji wa huduma kwa watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi nchini wakiwemo watoto waliotelekezwa, wanaoishi na kufanya kazi mitaani, wanaotoka katika kaya masikini, wanaolelewa na wazee wasio na uwezo, watoto wanaojilea wenyewe, Watoto yatima, na wale wanaokinzana na sheria pamoja na watoto waliozaliwa nje ya ndoa na watoto walio katika familia zenye migogoro. Hadi Aprili, 2024, jumla ya watoto 708,957 (Me 340,661, Ke 368,296) wanaoishi katika mazingira hatarishi wametambuliwa katika Halmashauri zote nchini na kupatiwa huduma kuendana na mahitaji yao. Watoto 275,058 (Me 127,667, Ke 147,391) kati ya hao wamesaidiwa na Serikali kwa kushirikiana na wadau kupata vyeti vya kuzaliwa. Kaya za watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi 457,450 (Me 141,507, Ke 315,943) zimesaidiwa kupata Bima za afya. Aidha watoto wengine wamesaidiwa kupata chakula, malazi, mavazi, elimu, matibabu, lishe, dawa za kufubaza VVU/UKIMWI, afya ya uzazi, ulinzi, msaada wa kisaikolojia na kijamii, marekebisho ya tabia, kuunganishwa na familia na mafunzo ya ufundi na stadi za maisha.

*Mheshimiwa Spika,* Wizara inajukumu la kutoa huduma za mahabusu kwa watoto kwenye mahabusu tano (5) za watoto za Mbeya, Kilimanjaro, Tanga, Arusha na Dar es Salaam. Watoto hawa ni wale walio katika mkinzano na sheria. Hadi kufikia Aprili, 2024, jumla ya watoto 381 (Me 361 na Ke 20) waliopo katika mahabusu hizi walipatiwa huduma za msingi zikiwemo chakula, malazi, mavazi, matibabu, elimu, stadi za Maisha na marekebisho ya tabia. Aidha, kati ya hao, jumla ya watoto 92 (Me 89 na Ke 3) waliohukumiwa kwa makosa mbalimbali wanaendelea kuhudumiwa katika Shule ya Maadilisho ya Irambo Mkoani Mbeya. Shule hii inatoa pia marekebisho ya tabia na elimu ya msingi na stadi za maisha kwa watoto ili wanapokamilisha hukumu zao waweze kujitegemea na kuwa raia wema.

*Mheshimiwa Spika,* Wizara imeendelea kuratibu huduma za Ustawi wa Jamii katika Mahakama za Watoto 133 nchini ambapo katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Aprili, 2024, mashauri 4,462 yalipokelewa yakijumuisha mashauri 1,034 ya matunzo (maintenance), 952 ya uangalizi wa mtoto (custody), 882 ya kuona watoto (access), 680 watoto waliokinzana na sheria, 13 ya kuasili, 7 ya vinasaba (DNA order), 22 ya uthibitisho wa baba (parentage), 872 ya Huduma za afya ya akili, msaada wa kisaikolojia na kijamii (Mental Health and Pyscho-social support - MHPS). Jumla ya mashauri 3,984 kati ya yote yaliopokelewa yalisikilizwa na kufungwa na mashauri 478 yaliobaki bado yanaendelea kusikilizwa.

*Mheshimiwa Spika,* huduma za malezi ya kambo na kuasili zimeendelea kutolewa kwa watoto walio katika mazingira hatarishi kwa kuhakikisha kuwa watoto wanalelewa katika ngazi ya familia kulingana na Sheria ya Mtoto, Sura ya 13. Wizara imeendelea kutoa elimu kwa umma kupitia vyombo vya habari, vipeperushi na matangazo juu ya umuhimu wa malezi ya watoto ngazi ya familia kupitia huduma ya malezi ya kambo na kuasili. Kutokana na jitihada hizi, idadi ya watoto waliopata malezi mbadala imeongezeka ambapo hadi kufikia Aprili 2024, jumla ya watoto 133 walipata malezi mbadala wakiwemo 74 malezi ya kambo, na 59 wameasiliwa, ukilinganisha idadi ya Watoto 75 (41 malezi ya Kambo na 34 waliasiliwa) mwaka 2022/23 sawa na ongezeko la asilimia 43.6.

*Mheshimiwa Spika*, Wizara imeendelea kusimamia na kuratibu utoaji wa huduma za msingi kwenye makao ya watoto ikiwemo usajili, malazi, chakula, malezi, matunzo, ulinzi, afya, elimu, msaada wa kisaikolojia na kijamii, mafunzo ya ufundi na stadi za maisha kwa watoto walio katika mazingira hatarishi nchini. Aidha, hadi kufikia Aprili 2024, leseni 35 za usajili wa Makao ya Watoto zimetolewa kwa watu binafsi na taasisi za dini na kufanya jumla ya makao yaliyosajiliwa kufikia 368 yenye Watoto 13,945 (Me 7,007 na Ke 6,938) ikilinganishwa na jumla ya Makao 333 mwezi Aprili 2023 ambapo jumla ya wahudumiwa ilikuwa watoto 12,077 (Me 6,050, Ke 6,027). Jitihada zinaenddela kuboresha Makao ya Taifa ya Watoto Kikombo (Dodoma) na Kurasini (Dar es Salaam).

*Mheshimiwa Spika,* Wizara inaendelea na uratibu wa afua za kupambana na wimbi la watoto wanaoishi na kufanya kazi mitaani nchini ambapo kwa kipindi cha Julai 2023 hadi Aprili 2024 jumla ya watoto 8,372 (Me 4,218, Ke 4,154) wametambuliwa katika Halmashauri zote nchini na kupatiwa huduma stahiki ikiwemo kuwapatia hifadhi ya muda kwenye Makao ya Kulelea Watoto kwa ajili ya kuwaandaa kuunganishwa na familia zao au kuwezeshwa kujitegemea katika **jamii. Nitumie fursa hii kuwaomba Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya kupitia**

**Kamati za Ulinzi wa Wanawake na Watoto kudhibiti tatizo la watoto wa mitaani kwa kuzisimamia Halmashauri zote kufanya tathmini ya kaya zilizo katika mazingira hatarishi na kuziwekea mkakati wa kuwasidia ili tuzuie watoto kutorokea mitaani, kwa sababu tatizo hili linaanzia katika mikoa na wilaya zetu.**

*Mheshimiwa Spika,* Wizara inaendelea kuratibu huduma ya msaada wa simu bila malipo Namba 116 (Child Helpline) kwa ajili ya jamii kutoa taarifa za vitendo vya ukatili dhidi ya Watoto ama kupata elimu juu ya masuala ya Watoto. Aidha huduma nyingine ni ile ya huduma kwa mteja inayotolewa na Wizara kupitia kituo cha huduma kwa mteja kilichopo Dodoma. Mteja anapiga simu za bure (0262160250, 0734986503, 0766400168 na 076960830) kwa ajili

ya kuwasilisha changamoto zao moja kwa moja kwa wizara na kusaidia kuwaunganisha na huduma pamoja na wataalam katika sekta mbalimbali.

*Mheshimiwa Spika,* Kupitia Programu Jumuishi ya Malezi na Makuzi (PJT MMAM), elimu ya malezi na makuzi kwa wazazi, walezi na jamii imeendelea kutolewa kupitia vyombo vya habari na mikutano ya hadhara katika ngazi zote kwa kushirikiana na wadau mbalimbali. Katika kufanikisha hili, Wizara imevitambua vyuo 63 vya mafunzo ya Malezi ya Watoto nchini pamoja na kutoa mafunzo kazini kwa walezi wa watoto wadogo na wachanga mchana. Jumla ya walezi 12,547 (Me 3,623 Ke 8,924) wameshiriki katika mafunzo ya kuongeza ufanisi wa huduma za uchangamshi wa awali na ulinzi kwa watoto.

*Mheshimiwa Spika,* Wizara kwa kushirikiana na wadau inaratibu na kutoa huduma ya msaada wa Akili na Kisaikolojia kwa makundi mbalimbali yanayokabiliwa na changamoto mbalimbali za kimaisha katika jamii yetu. Wizara imeendelea kuratibu utoaji wa huduma ya msaada wa kisaikolojia kwenye jamii katika Halmashauri zote nchini. Hadi kufikia Aprili 2024, Jumla ya watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi 284,308 (Me 183,124 na Ke 101,184), wazee wasiojiweza 245 (Ke 145 na Me 100) na waathirika wa matukio ya ukatili 2,682 (watoto 1,944 na watu wazima 738) wamepatiwa huduma hii. Aidha, katika kipindi hicho huduma hii pia imetolewa kwa wahanga wa vitendo vya ukatili 13,926 (ke 7,142 na watoto 6,784). Pamoja na wahanga wa vitendo vya ukatili na usafirishaji haramu wa binadamu 452 (Me 05, Ke 447).

*Mheshimiwa Spika,* Wizara imeratibu utoaji wa huduma kwa jamii ya waathirika wa maporomoko ya matope yaliyotokea katika Wilaya ya Hanang', Mkoani Manyara ambapo jumla ya waathirika 9,016 walipatiwa huduma ya Akili na Saikolojia ikiwa ni pamoja kuwatoa hofu na kuwapa utulivu; kufanya tathmini ya mahitaji ya waathirika kwa mtu mmoja mmoja; familia na jamii na kuwapa huduma stahiki kulingana na mahitaji. Aidha, huduma kama za Afya, kutambua wazazi wa kuaminika (Fit Persons) kwa watoto waliofiwa na wazazi wao, kwa ajili ya kuhakikishia usalama wao na kutoa malezi ya muda kwa watoto hao. Vilevile, waathirika wapao 690, kutoka kaya 140 waliokuwepo katika kambi za muda na ambao walipoteza makazi yao, waliunganishwa na ndugu na jamaa zao ili kuweza kupata hifadhi ya makazi na huduma nyingine.

*Mheshimiwa Spika,* Huduma ya Akili na Kisaikolojia imetolewa pia katika jamii ambazo zimeathirika na ugonjwa wa kipindupindu ambapo watu 79,513 (Me 38,142 na Ke 41,371) katika mikoa ya Simiyu, Dar es Salaam, Mwanza, Shinyanga, Kagera, Morogoro, Manyara, Katavi, Kigoma, Rukwa na Dodoma. Aidha, Wizara pia kwa kushirikiana na Wizara za Kisekta na wadau imeendelea kutoa huduma kwa waathirika 8,920 wa mafuriko katika Wilaya za Rufiji, Kibiti, Nsimbo, Mbeya Jiji na Mlimba.

*Mheshimiwa Spika,* Huduma ya Usuluhishi wa Migogoro ya Ndoa na Familia ni moja ya Majukumu ya Wizara yangu. Ikumbukwe kuwa utulivu wa Ndoa na Familia ni msingi mkubwa ustawi wa familia na jamii kwa jumla, kwani huzuia athari nyingi zikiwemo Ukatili, Watoto wa mtaani na kuvunjika kwa Ndoa. Katika kuhakikisha kuna ustawi na utulivu wa familia, Wizara kupitia maafisa Ustawi wa Jamii, imeendelea kuratibu huduma za usuluhishi wa migogoro ya ndoa na familia kupitia Baraza la Usuluhishi wa Ndoa la Kamishna wa Ustawi wa Jamii lililopo Makao Makuu ya Wizara, Mabaraza ya Kata, Mabaraza ya Jumuiya, Ofisi za Ustawi wa Jamii, wasaidizi wa msaada wa kisheria na Kampeni mbalimbali. Hadi kufikia Aprili 2024, mashauri yaliyoshughulikiwa yalikuwa 31,380 ikilinganishwa mashauri 28,773 yaliyoshughulikiwa mwaka 2022/2023 ikiwa na ongezeko la mashauri 2,607 sawa na asilimia 8.3. **Naomba nitoe wito kwa viongozi wa dini zote kuendelea kutoa mafunzo kwa**

**wanandoa wanaofunga ndoa na kwa vijana kupitia mikusanyiko ya vijana katika madhehebu yao, ili kuwaandaa kubeba majukumu ya ndoa na kujiandaa kwa majukumu hayo kabla ya kuingia katika ndoa.**

*Mheshimiwa Spika,* Katika kuhakikisha huduma za Msingi zinatolewa kwa Wazee na watu wasiojiweza, Wizara imeendelea kutoa huduma za chakula, malazi, mavazi, matibabu na msaada wa kisaikolojia na kijamii kwa wazee na watu wasiojiweza katika makazi 13 ya wazee yanayomilikiwa na Serikali, Pamoja wazee wanaoishi katika jamii. Wazee hawa hutambuliwa kupitia Ofisi za Ustawi wa Jamii zilizopo kwenye Halmashauri zote nchni. Hadi kufikia Aprili 2024, wazee wasiojiweza 240 (Ke 95 na Me 145) walihudumiwa katika makazi ya wazee ya Kibirizi (26), Njoro (18), Kolandoto (18), Bukumbi (27), Ipuli (24), Fungafunga (21),

Mwanzange (14), Misufini (18), Nunge (18), Nyabange (14), Kilima (19), Sukamahela (16), Magugu (7). Pia, Wizara imeendelea kusimamia na kuratibu huduma za msingi zinazotolewa kwa wazee kwenye makazi ya wazee ya Taasisi Binafsi 15 yenye jumla ya wazee 268 (me 150, ke 118) katika mikoa ya Dar es Salaam, Morogoro, Kagera, Shinyanga, Arusha, Tanga, Dodoma na Lindi.

*Mheshimiwa Spika,* Hadi kufikia Aprili 2024, jumla ya wazee 574,321 (Me 214,739, Ke 359,582) ambapo kati yao wazee

wasiojiweza 365,284 (Me 145,829, Ke 219,455) sawa na asilimia 63.6 ya wazee wote waliofanyiwa tathmini, wamepatiwa vitambulisho maalum kwa ajili ya msamaha wa matibabu. Vilevile, kampeni ya "MPISHE MZEE KWANZA" inaendelea kwenye vituo vya kutolea huduma za afya kuanzia ngazi ya zahanati hadi hospital ya taifa ili kutoa kipaumbele na kuhakikisha wazee wanapata huduma za afya kwa wakati ambapo kwa kipindi cha Julai 2023 hadi Aprili 2024 kulikua jumla ya madirisha 1,066 ya huduma kwa wazee nchini kote ikilinganishwa na madirisha 629 yaliokuwepo mwaka 2022/2023 ikiwa na ongezeko la madirisha 437 sawa na asilimia 69.48.

*Mheshimiwa Spika,* Wizara ipo katika hatua za Mwisho za kukamilisha mabadiliko ya sera ya wazee ambapo miongoni mwa maboresho yatakayozingatiwa ni pamoja na Kuwa na umuhimu wa jamii kujiandaa kabla ya uzee, huduma wa afya ya akili na kisaikolojia kwa wazee, miundombinu na mazingira wezeshe kwa wazee, na wawezeshwaji wa wazee kwenye mabadiliko ya Teknolojia kama TEHAMA.

*Mheshimiwa Spika,* Wizara yangu bado inakabiliwa na changamoto ya upungufu wa Maafisa Ustawi wa Jamii 17,485 ambayo ni sawa na asilimia 94.6 ya Maafisa wanaotakiwa kuanzia ngazi ya mkoa mpaka ngazi ya Kijiji/Mtaa kama inavyoonesha katika Jedwali Na.5 ukurasa wa 56. Naomba kutaarifu Bunge lako kwamba serikali imetoa kibali cha kuajiri Maasifa **Ustawi wa Jamii 350 na mchakato wa ajira umeshaanza. Nichukue fursa hii kumshuruku Mhe Rais kwa kutoa kibali cha ajira, aidha napenda kumshukuru waziri wa utumishi Mhe Simbachawene kwa ufuatiliaji wake hadi kufanikisha suala hili.**

**ENEO LA 5: MAENDELEO YA JINSIA NA UWEZESHAJI WANAWAKE**

*Mheshimiwa Spika,* Katika eneo la maendeleo ya Jinsia na Uwezeshaji wanawake, Wizara ina jukumu la kuhakikisha kuna usawa wa jinsia katika jamii yetu na kwamba Wanawake wanawezeshwa kiuchumi ili kuweza kuchangia katika shughuli za kiuchumi na maendeleo ya familia na nchi kwa ujumla.

Katika kufanikisha hili, Wizara, inatekeleza Programu ya Kitaifa ya Kizazi Chenye Usawa 2021/22 – 2025/26 (Generation Equality Forum Commitments- GEF) ambapo Mheshimiwa **Dkt. Samia Suluhu Hassan,** Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni Kinara wa utekelezaji wa eneo la Haki na Usawa wa Kiuchumi.

*Mheshimiwa spika,* Moja ya Mkakati wa Kumkomboa Mwanamke ambao unazingatiwa katika Programu ya kizazi chenye usawa, ni kuhakikisha anapata muda wa Kushiriki katika Shughuli za Kiuchumi ili kuchangia maendelea ya familia na nchi kwa ujumla. Katika kufanikisha hili; Wizara imetilia mkazo utekelezaji wa afua ambazo zinalenga kumpa muda zaidi mwanamke zikiwemo, Matumizi ya Nishati Safi. Hadi kufikia Aprili 2024, jumla ya wananchi 1,228,248 wanatumia nishati safi ya kupikia. Katika idadi hiyo, wanawake jumla ya 102,000 wasiokuwa na uwezo walipatiwa majiko ya gesi bure ikiwa ni jitihada za Mhe Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kuwezesha wanawake kutumia nishati safi ya kupikia akiwa kinara wa utekelezaji wa Programu ya kukuza matumizi ya nishati safi ya kupikia kwa Barani Afrika.

*Mheshimiwa Spika,* katika kuonyesha dhamira ya serikali katika kukuza usawa wa kijinsia, serikali kupitia Wizara yangu ilizindua Sera ya Taifa ya Jinsia na Maendeleo ya Wanawake ya mwaka 2023 mnamo tarehe 8 Machi, 2024 wakati wa kilele cha Maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani, Wilayani Chamwino, Mkoa wa Dodoma. Mapitio na maboresho ya Sera hiyo, yamezingatia masuala mabadiliko ya Tabia Nchi, ushirikishwaji wa wanaume katika jitihada za kuleta usawa wa kijinsia na matumizi ya teknolojia katika uzalishaji na mawasiliano na Ukatili mtandaoni wakati wa Uchaguzi. Masuala haya yote yamewekewa matamko na mikakati ya utekelezaji, na kwa kuwa hii Sera Mama ya masuala ya jinsia nchini, utekelezaji wake utachochea jamii na wadau kuendeleza mafanikio yaliyopo katika utatuzi wa changamoto za wanawake na wanaume ili kuwa na Taifa la Kizazi Chenye Usawa. Aidha nalishukuru Bunge lako tukufu, Wizara za kisekta na wadau wote ambao wamechangia katika kufanikisha kukamilika kwa sera.

*Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi*

*Mheshimiwa spika,* Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeendelea kutoa mafunzo ya ujasiriamali na uendeshaji wa biashara kwa wanawake wajasiriamali. Kuanzia Julai 2023 hadi kufikia Aprili 2024, jumla ya wanawake 2,222,000 wamepatiwa mafunzo ya ujasiriamali katika nyanja za elimu ya fedha, matumizi ya teknolojia, masoko, mnyororo wa thamani na uongozi bora. Aidha, katika kipindi cha mwaka 2023 hadi Aprili, 2024, mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 748 imetolewa kupitia Mifuko na Programu za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ambapo jumla ya walengwa 6,064,957 wamenufaika na mikopo hiyo; kati yao wanawake ni 3,288,186 sawa na asilimia 54 na wanaume 2,776,771, sawa na asilimia 46.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kushirikiana na Sekta ya mifugo na uvuvi, 1,023 wamekopeshwa boti za kisasa za uvuvi na wanawake 446 wamekopeshwa vizimba vya kisasa vya kufugia Samaki. Mikopo yote hii haina riba. Aidha, Wanawake 24 wamepatiwa mafunzo yanayohusu ututoleshaji wa vifaranga vya kuku, na wanawake 38 wamewezeshwa kuwa wazalishaji wa vitotoleshi. Katika mrengo huu huu wa kuwawezesha wanawake, Wizara imefanikisha upatikanaji wa mashine 250 za ututoleshaji vifaranga vya kuku na vyerehani 425 vyenye thamani ya Shilingi Milioni 79 kutoka Serikali ya Watu wa China ambavyo vitasambazwa kwa wanawake nchini. Jitihada hizi zimewezesha wanawake kuongeza ari miongoni mwao na kuongea fursa ya kujiajiri katika sekta ya uvuvi, mifugo na ushonaji.

*Uanzishwaji wa Majukwaa ya Uwezeshaji Kiuchumi*

*Mheshimiwa Spika*, Uanzishaji wa majukwaa haya ni fursa kwa wanawake kuweza kukutana na kujadili masuala mbalimbali wanayokabiliana nayo katika shughuli zao za kujikwamua kiuchumi pamoja na kuweka mikakati ya ufumbuzi. Aidha, Majukwaa haya yameongeza kazi zenye staha kwa wanawake katika sekta rasmi na sekta isiyo rasmi. Katika kuhakikisha idadi ya majukwaa haya yanaongezeka, Wizara imeendelea kuratibu uanzishwaji na uendeshaji wa Majukwaa haya. Hadi kufikia Aprili, 2024, jumla ya majukwaa 3,391 yameanzishwa yakijumuisha majukwaa ngazi ya mkoa ni 26, Halmashauri 152 kati ya 184, kata 1,354 kati ya 3,957 na Mitaa/ Vijiji 1,859 kati ya vijiji 12,348. Aidha, Wizara katika kuboresha utendaji kazi wa Majukwaa inakamilisha Mapitio ya Mwongozo wa Uundaji na Uratibu wa majukwaa ya Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi, ili kuyafanya yawe na ufanisi zaidi.

*Mheshimiwa Spika,* sambamba na uanzishaji wa majukwaa haya, Wizara imeendelea kuratibu ushiriki wa wanawake kwenye Maonyesho mbalimbali ya biashara. Maonesho haya huwapatia fursa wanawake kushiriki na kutangaza bidhaa zao ili kupata masoko ya ndani na nje ya nchi, Pamoja na kuongeza wigo wa mtandao wa mawasiliano na mnyororo wa thamani wa bidhaa zao. Hadi kufikia Aprili, 2024 Wizara iliwezesha ushiriki wa wanawake 336 katika maonyesho ya Sabasaba yaliyofanyika jijini Dar es salaam na wanawake 1,880 katika maonyesho ya Nanenane yaliyofanyikia Jijini Mbeya.

*Mheshimiwa Spika,* Wizara kwa kushirikiana na shirika lisilo la kiserikali (WiLDAF) imeratibu Kampeni ya Siku 16 za Kupinga Ukatili wa Kijinsia katika mikoa yote nchini, ambapo kilele cha kampeni hii ilifanyika Mkoa wa Mara 10, Dsemba 2023. Lengo la Kampeni hii ni kuongeza jitihada za jamii kukabiliana na vitendo vya ukatili wa kijinsia ambapo Kaulimbiu ya Mwaka huu ilikuwa **"Wekeza: Kuzuia Vitendo vya Ukatili"**. Aidha, wizara ilianda matamasha yaliyolenga kutoa elimu na uelewa juu ya fursa za kiuchumi, Athari za ukatili. Kampeni zote ziliongozwa na kauli mbiu **"Zijue Fursa, Imarisha Uchumi, Kataa Ukatili, Kazi Iendelee" (ZIFIUKUKI)**. Kupitia Matamasha haya jumla ya wananchi 45,895 (Me 21,830 na Ke 24,065) kwa mikoa hii miwili walipata huduma mbalimbali zikiwemo huduma ya msaada wa kisheria, kisaikolojia, elimu ya masuala ya jinsia, na biashara na huduma za afya.

*Mheshimiwa Spika*, Kupitia Mwongozo wa Uanzishwaji wa Madawati ya Jinsia, Wizara imeendelea kuratibu uanzishwaji wa madawati ya jinsia katika Taasisi za Elimu ya Juu na Maeneo ya umma. Sambamba na uanzishwaji wa madawati haya, Wizara imeendelea kutoa mafunzo kwa Wakuu wa Vyuo pamoja na Waratibu wa Madawati haya ili kuwapa uelewa na uwezo wa kuyaratibu na hatimae kutokomeza ukatili katika maeneo yao. Hadi kufikia Aprili, 2024 jumla ya Madawati 612 yameanzishwa na kati ya hayo, 296 (48.4%) ni madawati ya jinsia. *Mheshimiwa Spika,* Uingizwaji wa masuala ya Jinsia ni kipaumbele ambacho Wizara imeendelea kusimamia ili kuwa na Sera, Mipango, Programu, Mikakati, Miongozo na Bajeti za Wizara za Kisekta na Sekta binafsi zenye mrengo wa Kijinsia. Katika kutekeleza hilo, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais Utumishi zimezindua Mwongozo wa Ujumuishaji wa Jinsia katika Utumishi wa Umma wa Julai 2023, ambao unaimarisha utekelezaji wa masuala ya Jinsia katika utumishi wa Umma. Vilevile, Wizara kwa kushirikiana na jeshi la Magereza Nchini imewezesha kuandaliwa kwa Mkakati wa uingizwaji wa masuala ya Jinsia ya Jeshi hilo unaozingatia pia kundi la wafungwa wanaohudumiwa.

*Mheshimiwa Spika,* Wizara imeshiriki Mikutano ya Kimataifa na Kikanda kwa ajili ya kutekeleza masuala ya Jinsia na Uwezeshaji Wanawake ambayo nchi yetu imeridhia. Kwa kipindi cha Julai, 2023 hadi Aprili, 2024 Wizara ilishiriki Mkutano wa Women Deliver uliofanyika Nchini Rwanda Kigali Julai, 2023. Pia Tulishiriki katika Mkutano wa 13 wa Mawaziri wanaoshughulikia masuala ya wanawake wa nchi wanachama wa Jumuiya ya Madola (JYM) – The 13th Commonwealth Women's Affairs Ministerial Meeting (CWAMM) uliofanyika Agosti, 2023, Jijini Nassau, Bahamas.

Wizara imeshiriki katika Mkutano wa Mapitio kipindi cha kati cha utekelezaji wa Programu ya kizazi chenye Usawa (GEF Mid-Point Review) uliofanyika Jijini New York Marekani Septemba, 2023 Ambapo Nilimuwakilisha Mhe Rais, ambae alialikwa kama Mgeni Mahsusi. Aidha kuanzia tarehe 11 – 22 Machi 2024, Wizara tulishiriki Mkutano wa 68 wa Kamisheni ya Hali ya Wanawake Duniani uliofanyika Jijini New York, Marekani, ambapo Mhe Spika wewe binafsi ulishiriki Pamoja nasi kwa nafasi yako ya Rais wa Mabunge ya Dunia (International Parliamentary Unit)

*Mheshimiwa Spika,* Wakati Ninapohitimisha katika eneo hili la usawa wa kijinsia na Uwezeshaji wanawake kiuchumi, Napenda kulitaarifu Bunge lako tukufu kwamba, Jitihada za Mhe Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzaniaa, Dr Samia Suluhu Hassan, imeiweka Nchi yetu katika nafasi nzuri Kimataifa katika utekelezaji wa usawa wa jinsia kwa vitendo katika nyanja zote. Hivyo, Bunge lako tukufu, Watumishi wote, wadau wa Maendeleo, jamii kwa ujumla, na kwa upekee WANAWAKE WOTE hatuna budi Kumpongeza na kumuunga mkono katika jitihada hizi kwa kuendelea kujenga uelewa na fursa kwa mafanikio zaidi hapa nchini.

**ENEO LA 6: URATIBU WA MASHIRIKA YASIYO YA KISERIKALI.**

*Mheshimiwa Spika,* Wizara inaendelea na usajili, uratibu na ufuatiliaji wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kwa kuzingatia Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Sura Na. 56. Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Aprili, 2024 Wizara imesajili jumla ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali 1,028. Kati ya hayo, Mashirika ya Kimataifa ni 43, Kitaifa ni 937, Kimkoa ni 29 na Kiwilaya Mashirika 19. Idadi hii inafanya jumla ya Mashirika yaliyosajiliwa nchini kufikia 10,538. Aidha katika kipindi hicho jumla ya Mashirika 1,124 yamefuatiliwa usajili kwa sababu mbalimbali.

*Mheshimiwa Spika,* Wizara imeboresha Mfumo wa Kielektroniki wa Usajili na Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kwa kuongeza sehemu ya Ramani ya Utambuzi wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Kidigitali. Ramani ya utambuzi wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Kidigitali imelenga kuwezesha wadau, Taasisi za Serikali na Jamii kwa ujumla kupata taarifa za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kwa urahisi mahali popote walipo. Mfumo huu ulizinduliwa na Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Jukwaa la mwaka la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali lililofanyika jijini Dodoma tarehe 05 Oktoba, 2023. Mfumo huu umeanza kutumika ambapo hadi kufikia Aprili 2024 jumla ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali 10,538 yameshatambuliwa kwenye ramani, tayari yamewekewa taarifa kuanzia ngazi ya kata.

*Mheshimiwa Spika,* Wizara inaratibu na kuandaa taarifa ya mchango wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika Maendeleo ya Taifa. Kwa mwaka 2022 taarifa hiyo iliandaliwa na kusambazwa kwa wadau mbalimbali yakiwemo Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Wadau wa Maendeleo na Taasisi binafsi wakati wa Jukwaa la Mwaka la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali lililofanyika tarehe 03 – 05 Oktoba, 2023. Taarifa hiyo imebainisha kuwa, jumla ya Mashirika 1,257 yaliyowasilisha taarifa zao yalikuwa na mapato ya shilingi 2,249,244,846,280 kutoka vyanzo mbalimbali vya fedha kwa kipindi cha Januari hadi Desemba 2022. Kati ya fedha hizo Shilingi 1,959,334,118,380 zilitumika katika utekelezaji wa miradi kwenye afua za mazingira, afya, uwezeshaji jamii, ulinzi wa jamii, kilimo, elimu, utawala bora, maji, haki za binadamu na jinsia na shilingi 289,910,727,900 zilitumika katika posho na mishahara, kodi za ujuzi, kodi za mishahara, kuchangia kwenye mfuko wa Hifadhi ya Jamii na Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi. Vilevile, kazi na huduma za Mashirika hayo ziliwanufaisha watu 6,316,968. Halikadhalika, taarifa ilionesha kuwa, Mashirika yaliajiri jumla ya watu 9,974 ambapo kati ya hao Watanzania ni 9,818 na Wageni 156.

Mheshimiwa Spika, Naipongeza Bodi ya Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, katika kusimamia utekelezaji wa Sheria na Kanuni zinazosimamia Mashirika Yasiyo ya Kiserikali nchini. Naipongeza Mikoa na Halmashauri zote zilizojitokeza kuratibu kwa pamoja majukwaa ya Mashirika hayo katika maeneo yao. Natoa rai kwa Mikoa na Halmashauri kutoa ushirikiano katika majukwaa hayo na kufanya Uchaguzi wa wajumbe wa Baraza la Taifa la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kwa maendeleo ya taifa.

**ENEO LA 7: URATIBU WA MPANGO KAZI WA TAIFA WA KUTOKOMEZA UKATILI DHIDI YA WANAWAKE NA WATOTO (MTAKUWWA).**

*Mheshimiwa Spika,* Wizara kwa kushirikiana na wadau ilitekeleza na kufanya tathmini ya Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto (MTAKUWWA 2017/18 – 2021/22). Mpango ulilenga kupunguza vitendo vya ukatili dhidi ya wanawake na watoto, kuimarisha uchumi wa kaya pamoja na kuimarisha huduma za msaada wa waathirika wa vitendo vya ukatili. Tathmini ya utekelezaji wa mpango huu inaonesha kuwa, ukatili wa kimwili kwa wanawake umepungua kutoka 40% mwaka 2015 hadi 22% mwaka 2022, ukatili wa kingono umepungua kutoka 17% mwaka 2015 hadi 12% mwaka 2022 na vitendo vya ukeketaji vimepungua kutoka 10% mwaka 2015 hadi kufikia 8% mwaka 2022.



*Mheshimiwa Spika,* Wizara kwa kushirikiana na wadau imeandaa Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto awamu ya Pili (MTAKUWWA 2024/25 – 2028/29) ambapo Mpango huu umezinduliwa rasmi siku ya tarehe 15, Mei 2024. Utekelezaji wa Mpango huu ni shirikishi ukihusisha ushirikiano baina ya Serikali, Wadau wa Maendeleo, Asasi za Kiraia, Sekta Binafsi pamoja na Jamii yote kwa ujumla. Lengo la Mpango huu ni kupunguza vitendo vya ukatili dhidi ya wanawake na watoto kwa asilimia 50%. Kupitia Mpango huu, Serikali kwa kushirikiana na wadau imepanga kupunguza ukatili wa kimwili kutoka 27% hadi kufikia 14%, kupunguza ukatili wa kingono kutoka 12% hadi kufikia 6% na kupunguza vitendo vya ukeketaji kutoka 8% hadi kufikia 2% mwaka 2028/29. Aidha, kupitia Mpango huu, Serikali kwa kushirikiana na wadau itatekeleza afua za kuimarisha uchumi wa kaya ikiwemo kuendelea kutoa mikopo yenye masharti nafuu, itaendelea kutoa elimu kuhusiana na mila na desturi zenye madhara na kuimarisha mila zenye matokeo chanya, itaimarisha ulinzi wa mwanamke na mtoto katika maeneo ya umma na katika mitandao na itaongeza vituo vya kutolea huduma kwa wahanga wa ukatili kama vile nyumba salama na vituo vya mkono kwa mkono.

## D. UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA TAASISI ZILIZO CHINI YA WIZARA

*Mheshimiwa Spika,* Wizara ina jukumu la kusimamia utengaji wa Taasisi zilizo chini yake ambazo ni Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru na Taasisi ya Ustawi wa Jamii. Taasisi hizi zimeendelea kutoa mafunzo ya Taaluma ya Maendeleo ya Jamii katika ngazi ya Astashahada, Stashahada, Shahada na Shahada ya Uzamili. Vilevile, Taasisi zimeendelea kufanya tafiti na kutoa ushauri elekezi katika nyanja zinazo shabihiana na taaluma ya Maendeleo ya Jamii na taaluma ya Ustawi wa Jamii. Aidha, kumekuwepo na jitihada mbalimbali zinazofanywa na Taasisi hizi ili kuimarisha mifumo ya utoaji wa mafunzo, kufanya tafiti na kutoa ushauri elekezi kwa lengo kuongeza ukusanyaji wa mapato

## E. UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO.

*Mheshimiwa Spika,* katika kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia kwa wanafunzi, Wizara imeendelea kutekeleza afua mbalimbali za miradi ya maendeleo ikiwemo ujenzi na ukarabati wa majengo na miundombinu katika Taasisi na Vyuo vilivyo chini yake. Kwa kipindi cha Julai, 2023 hadi Aprili 2024, Wizara imepokea fedha za ndani za maendeleo kiasi cha **Shilingi Bilioni 4.88,** kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi wa Ukarabati wa Vyuo vya Maendeleo ya Jamii (**Shilingi Bilioni 2),** utekelezaji wa shughuli za programu ya kizazi chenye usawa **(Shilingi Bilioni 2.48)** na Mradi wa Huduma za Ustawi wa Jamii (**Shilingi Milioni 400)**.

## F. VIPAUMBELE VYA WIZARA NA BAJETI YA MAPATO, MATUMIZI YA KAWAIDA NA MIRADI YA MAENDELEO KWA MWAKA 2024/25

***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/25, Wizara kupitia Idara na Taasisi zilizo chini yake itatekeleza vipaumbele sita (6) ili kuboresha utoaji wa huduma za maendeleo na ustawi wa jamii. Vipaumbele hivyo ni kama vifuatavyo: -

i) Kukuza ari ya jamii kushiriki katika kupanga na kutekeleza miradi ya maendeleo iliyoibuliwa Ngazi ya Msingi;
ii) Kuratibu afua za kukuza usawa wa kijinsia na kutokomeza vitendo vya ukatili, uwezeshaji wanawake kiuchumi, upatikanaji wa haki, ulinzi na malezi chanya ya watoto;
iii) Kuratibu na kuimarisha utoaji wa huduma za msingi za ustawi wa jamii;
iv) Kutambua, kuratibu na kuendeleza Makundi Maalum wakiwemo wafanyabiashara ndogondogo;
v) Kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia katika Taasisi na Vyuo vya Ustawi na Maendeleo ya Jamii; na
vi) Kuimarisha ushiriki na mchango wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika Maendeleo ya Taifa.

***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza vipaumbele vilivyoainishwa, Wizara kwa mwaka 2024/25 imekadiria kutumia kiasi cha **Shilingi 67,905,259,000** kati ya hizo **shilingi 47,487,079,000** ni fedha za matumizi ya kawaida ambapo **Shilingi 21,650,426,000** ni Fedha za MIshahara na **Shillingi 25,836,653,000** ni fedha za uendesjaji wa ofisi, Aidha **Shilingi. 20,418,180,000** ni fedha za utekelezaji wa miradi ya maendeleo ambapo kati ya fedha hizo **Shillingi 18,025,673,000** ni fedha za ndani na **Shillingi 2,392.507,000** ni fedha za nje. Baadhi ya maeneo yaliyotengewa fedha kwa mwaka 2024/25 ni pamoja na: -

i) Katika eneo la kukuza usawa wa kijinsia na uwezeshaji wanawake kiuchumi (Generation Equality Forum - GEF), kiasi cha shillingi Bilioni 3.2 zimetengwa kwa ajili ya kuratibu shughuli za usawa wa kijinsia na uwezeshaji wanawake kiuchumi;
ii) Katika eneo la kutokomeza vitendo vya ukatili dhidi ya wanawake na watoto, kiasi cha Shilingi Bilioni 3.15 kimetengwa;
iii) Katika eneo la kutambua na kuratibu shughuli za kiuchumi za Makundi Maalum hususan wafanyabiashara ndogondogo wakiwemo machinga, mama/baba lishe, waendesha bodaboda na bajaji, kiasi cha **Shilingi Bilioni 10.5** kimetengwa kwa ajili ya kutoa mikopo yenye masharti nafuu ili kuongeza mitaji na kuboresha shughuli zao za kiuchumi;
iv) Kwenye eneo la huduma za ustawi wa jamii na watoto, kiasi cha **Shilingi Bilioni 1.2** kimetengwa kwa ajili ya kuwezesha utoaji wa huduma za marekebisho ya tabia kwa watoto waliokinzana na sheria; kufuatilia utoaji wa huduma katika Makao ya Watoto, Vituo vya Kulelea Watoto wadogo Mchana na Watoto Wachanga; Kukarabati Shule ya Maadilisho ya Upanga na Mtwara; na Kuendeleza ujenzi wa Mahabusu ya Watoto Mwanza;
v) Katika eneo la Wazee, **Shilingi Bilioni 1.06** zimetengwa kwa ajili ya kuwezesha utoaji wa huduma za ustawi kwa wazee wasiojiweza katika Makazi ya Wazee 13;
vi) Kwenye eneo la Taasisi na Vyuo, kiasi cha **Shilingi Bilioni 2** kimetengwa. Fedha hizo ni kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa majengo na miundombinu katika Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru, na Vyuo vitatu (3) vya Maendeleo ya Jamii vya Uyole, Rungemba na Buhare;
vii) Eneo la Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali limetengewa kiasi cha **Shilingi Bilioni 2.5** kwa ajili ya Kusajili na kufanya ufuatiliaji wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, kuandaa Taarifa ya Mchango wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kwa mwaka 2024, kuratibu utekelezaji wa Mkakati wa Kitaifa wa Uendelevu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (2022/2023 - 2025/2026), na kuratibu vikao vya Bodi na Jukwaa la Mwaka la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali;
viii) Eneo la maendeleo ya jamii limetengewa kiasi cha **Shilingi Milioni 826.1** kwa ajili ya kutekeleza Kampeni ya Kitaifa ya Kuamsha Ari ya Jamii kuhusu ujenzi wa nyumba bora za gharama nafuu kwa kutumia teknolojia rahisi na kutekeleza Mpango wa Taifa wa Kuhamasisha na Kusimamia Maendeleo Ngazi ya Msingi wa mwaka 2022/23 - 2025/26 (Bottom Up) katika Mikoa 26 ya Tanzania Bara; na
ix) Katika eneo la ufuatiliaji na tathmini, kiasi cha **Shilingi Milioni 150** kimetengwa. Fedha hizo ni kwa ajili ya kufuatilia utekelezaji wa mipango, programu na miradi ya maendeleo inayotekelezwa katika Taasisi, Vyuo na Vituo vya Ustawi wa Jamii vilivyo chini ya Wizara.

## G. SHUKRANI

***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imekuwa ikipata ushirikiano mkubwa kutoka nchi rafiki, Mashirika ya Kimataifa na Sekta mbalimbali zinazosaidia na kuchangia katika huduma za maendeleo na ustawi wa jamii. Aidha, Naomba nitumie fursa hii kuzishukuru Serikali za nchi rafiki zikiwemo Marekani, Japan, Ufalme wa Uingereza, Ufalme wa Sweden, Jamhuri ya Watu wa China, Ufalme wa Norway, Falme za Nchi za Kiarabu, Italia, Ujerumani, Ubelgiji, Ufaransa, Canada, Ufalme wa Denmark, Ireland, Jamhuri ya Uswisi, Bangladesh na nchi nyingine ambazo zimeendelea kuisaidia Wizara kwa njia mbalimbali.

***Mheshimiwa Spika,*** ninayashukuru Mashirika na Taasisi za Kimataifa kwa ushirikiano wao waliotoa kwa Wizara. Mashirika na Taasisi hizo ni pamoja na: - Mashirika ya Umoja wa Mataifa yakiwemo UNICEF, UNFPA, UN-Women, WHO, UNDP, ILO, IOM, WFP, FAO, UNESCO na UNHCR.
Vilevile, ninashukuru Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), Umoja wa Afrika (AU), Jumuiya ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC), na Jumuiya za Umoja wa Nchi za Ulaya (EU). Pia nayashukuru Mashirika ya Kimataifa ambayo ni: -Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Mfuko wa *Abbott Fund*, *Global Fund* na *Hilton Condrad Foundation*.

Aidha, nazishukuru Taasisi za Kifedha za hapa nchini zinazoshirikiana na Wizara ambapo ni pamoja na Benki za CRDB, NMB, Benki ya Biashara Tanzania (TCB), Stanbic, Azania, NBC, Equity, Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ), Akiba Commercial Bank (ACB) na Benki ya Mkombozi na Benki ya Biashara Tanzania.

***Mheshimiwa Spika,*** nayashukuru Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ya ndani ya nchi na Mashirika ya Dini kwa kuwa mstari wa mbele katika kuchangia uimarishaji wa huduma za maendeleo na ustawi wa jamii. Mashirika hayo ni pamoja na; *World Vision, PACT Tanzania, The Aga Khan Foundation, Foundation for Civil Society*, *HelpAge International, Compassion International*, *Responsible Organization Tanzania, Both Ends Believing* (BEB), *Safe Society Platform Tanzania*, *Children in Crossfire*, *Care International Tanzania, Railway Children Tanzania,* WiLDAF, ICS, TAWLA, TAYOA, LSF, *SOS Children's Village Tanzania*, BRAC Maendeleo Tanzania, *Plan International - Tanzania*, Kivulini, Uongozi wa Mgodi wa Geita, FSDT, WFT, TANLAP,*Save the Children, Equality for Growth (EfG)*, Landesa, CAMFED, CSEMA; REPPSI, *Amani Girls Home*, Pelum Tanzania, LHRC, Haki Elimu, TWCC, TECDEN, EGPAF,FAGDI, na MEWATA.

***Mheshimiwa Spika,*** nitoe pia shukrani zangu kwa Jumuiya za makundi mbalimbali ambazo zimekuwa zikifanya kazi na Wizara. Jumuiya hizo ni pamoja na:- Baraza la Wazee Tanzania, Chama cha Wazee Wanaume Tanzania, Chama cha Madereva na Wamiliki wa Pikipiki Tanzania (CHAMWAPITA), Machifu na Viongozi wa Kimila Tanzania, Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT), Chama Cha Wanawake Wajane Tanzania (CCWWT), Jukwaa la ULINGO, Jumuiya ya Wazazi CCM, Baraza la Watoto la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, TAWIA, Shirikisho la Umoja wa Machinga Tanzania (SHIUMA) na Umoja wa Mama na Baba Lishe Tanzania. Pia naomba nizishukuru Klabu za Mpira wa Miguu Tanzania hususan Yanga, Simba, AZAM na vikundi/kampeni za Kijamii kama (Shujaa wa Maendeleo na Ustawi wa Jamii (SMAUJATA), *Foundation for Ambassadors of Gender Development Initiatives* (FAGDI), Sauti ya Watoto Tanzania (SAWATA) NA MALEZI BORA NETWORK pamoja na vyombo vyote vya habari.

***Mheshimiwa Spika,*** nitoe shukrani zangu pia kwa viongozi na taasisi zetu za dini zikiwemo Baraza la Maaskofu wa Makanisa ya Kipentekoste Tanzania (CPCT), Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania (TEC), Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA), Jumuiya ya Kikristo Tanzania (CCT) na Kanisa la Waadventista Wasabato (SDA).

***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha utekelezaji wa majukumu yangu nikiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, nimepata ushirikiano mkubwa kutoka kwa viongozi na wafanyakazi wa Wizara. Naomba kumshukuru **Dkt. Seif Abdallah Shekalaghe,** Katibu Mkuu na **Bw. Amon A. Mpanju,** Naibu Katibu Mkuu kwa mchango na ushirikiano wao katika kuwezesha utekelezaji wa majukumu yangu. Aidha, nawashukuru Makamishna, Wasajili, Wakurugenzi, Wakuu wa Vitengo na Wataalam wote wa Wizara kwa utendaji wao mahiri uliowezesha kukamilisha maandalizi ya Hotuba yangu kwa wakati.

***Mheshimiwa Spika,*** kipekee naomba kuwashukuru Bodi na Menejimenti za Taasisi ya Ustawi wa Jamii na Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru. Pia, nawashukuru Wakuu wa Vyuo nane (8) vya Maendeleo ya Jamii kwa ushirikiano wao mzuri unaonirahisishia utekelezaji wa majukumu yangu. Natoa shukrani kwa sekta zote ambazo tunashirikiana nazo katika kutoa huduma za maendeleo na ustawi wa jamii pamoja na wananchi wote kwa ushirikiano wao.

***Mheshimiwa Spika,*** Vilevile, kupitia OR – TAMISEMI nawashukuru sana Wakuu wa Mikoa yote, Makatibu Tawala, Wakuu wa Wilaya na Wakurugenzi wa Halmashauri zote na Wataalam wote chini ya Ofisi zao na Wadau wote wa sekta mbalimbali wanao hudumia katika maeneo yao pamoja na wananchi mmoja mmoja na mitandao yote ya habari za kijamii ambao wamekuwa wakifuatilia na kutoa ushirikiano mkubwa kwenye utekelezaji wa majukumu ya wizara yangu hasa kupambana kutokomeza ukatili wa kijinsia.

***Mheshimiwa Spika,*** nichukue fursa hii pia kuishukuru familia yangu, hususan mume wangu **Wakili Msomi Methusela Gwajima** na watoto wetu pamoja na wote ambao wamekuwa sehemu ya familia yetu kwa uvumilivu wao wa kipekee kwa kunitia moyo katika kutekeleza majukumu yangu ya Kitaifa. Aidha, nawashukuru wananchi wote wa Tanzania kwa kuipatia ushirikiano Wizara ninayoisimamia wakati wote wa kutekeleza majukumu yangu na pia kwa wao binafsi kuendelea kupambana kuhakikisha maendeleo na ustawi wa jamii kwa usawa wa jinsia huku wakitumia **Simu Namba 116** na kituo cha huduma kwa mteja cha Wizara chenye namba za simu **0262160250, 0734986503, 0766400168** na **0769608130** kilichopo Mkoani Dodoma bila malipo kwa ajili ya kuripoti matukio au viashiria vya ukatili. Aidha, nawahimiza kuendelea kutumia simu zote kama tulivyotangaza kwenye vyombo vya habari na kuziweka kwenye tovuti yetu ya Wizara ambayo ni ***www.jamii.go.tz***.





## 'SMZ, SJMT zina dhamira ya kuwapa ajira, kipato wananchi'

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

NAIBU Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Khamis Hamza Chilo, amesema Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) pamoja na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SJMT), zina dhamira ya kuwawezesha wananchi kujikwamua kiuchumi, kujipatia ajira, kujiongezea kipato na kujiletea maendeleo.

Chilo alieleza hayo juzi katika ukumbi wa Shule ya Dunga, Wilaya ya Kati Unguja alipokuwa akifungua mkutano wa utambulisho wa Chama cha Mazingira na Ufugaji Tija Tanzania (CHAMAUTA).

Alisema SJMT na SMZ zinaunga mkono jitihada za wananchi katika suala la utunzaji wa mazingira na ufugaji wenye tija ili kuimarisha fikra zenye kuleta mapinduzi katika utunzaji wa mazingira pamoja na kufuga kwa kutulia eneo moja na kuwa na mabanda ya kisasa.

Aidha, alisema kuwa mazingira salama ni nidhamu ya ufugaji salama, hivyo alisisitiza kupanda miti ya kutosha kulingana na mazingira yaliyopo ili kuepusha mifugo isikumbane na mlipuko wa magonjwa kwa kuzingatia utunzaji wa mazingira.

Pia, aliwataka wanachama hao kutengeneza mazingira ya kijani yenye hewa salama itokanayo na miti na kufuga kisasa kwa kuzingatia chanjo, lishe bora na mabanda bora ya kisasa kwa ajili ya kujipatia tija iliyobora inayoendana na soko la ufugaji.

Mwenyekiti wa chama hicho, Jeremiah Wambura, alisema kuwa wamelenga kuunganisha nguvu za wadau wa utunzaji mazingira na wafugaji wote wa Tanzania Bara na Zanzibar ili kulinda na kutetea haki na maslahi yao.

Katibu Mkuu wa chama hicho, Makame Ali Makame, alisema CHAMAUTA kinaundwa na wadau mbalimbali wa utunzaji wa mazingira pamoja na ufugaji, wenye tija.

# ACT-Wazalendo bado walia na Sheria ya Uchaguzi

**Na Mwandishi Wetu**

MWENYEKITI wa Chama cha ACT-Wazalendo, Othman Masoud Othman, amesema Sheria ya Uchaguzi ya Kupiga Kura ya Mapema inapaswa kuondolewa kwa sababu ndiyo chanzo cha vurugu na mauaji katika Uchaguzi wa Zanzibar.

Aliyasema hayo alipokuwa akizungumza na viongozi wa mikoa miwili ya kichama Kaskazini A na B Unguja wa chama hicho, katika mkutano wa kukamilisha ziara, kuwashukuru wanachama kumaliza uchaguzi mkuu wa viongozi.

Alisema Sheria ya Tume ya Uchaguzi Zanzibar kuweka utaratibu wa askari wa ulinzi na usalama kupiga kura siku moja kabla ya uchaguzi mkuu ni sheria ambayo imeleta matatizo makubwa katika kufikia misingi ya uchaguzi huru na haki visiwani Zanzibar.

"Katika maridhiano ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa mambo mawili tumesema hayana mjadala la kwanza ni kura ya siku mbili hili lazima liondoke. Tulisema hatuwezi kupoteza muda kuja mezani kujadili iwepo au isiwepo kwa sababu imeletwa kwa nia ya kufanya dhuluma, kudanganya na kuiba uchaguzi," alisema.

Aliongeza: "Leo hatuwezi kujadili kwamba wizi huu uendelee au usiendelee na hili kama halijatekelezwa hatutokubali na ndiyo chanzo cha vurugu na kuua watu."

Alisema katika kuelekea Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025, kama sheria hiyo haitoondolewa, chama hicho hakitokubali kwa sababu imetungwa kwa misingi ya kuvuruga haki ya demokrasia na inaruhusu udanganyifu kufanyika katika matokeo ya Uchaguzi Mkuu wa Zanzibar.

Aidha, alisema kabla ya ACT kukubali kuunda Serikali ya Umoja wa Kitaifa kuna mambo ya msingi walikubaliana ikiwamo serikali kuhakikisha inafanya mabadiliko makubwa katika muundo wa Tume ya Uchaguzi Zanzibar ikiwamo mfumo wa upatikanaji wa makamishna na sekretarieti ya tume hiyo.

Alisema katika kuelekea Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025 lazima kila mwananchi mwenye haki apewe cheti cha kuzaliwa na gharama za kupata cheti hicho ziondolewe, ili kila mwananchi aweze kupata haki yake ikiwamo kitambulisho cha mzanzibari mkaazi, ambacho ndiyo msingi wa kuandikishwa katika daftari la wapigakura la Tume ya Uchaguzi Zanzibar.

Alisema mambo hayo ni haki kwa kila mwananchi na kwa mujibu wa makubaliano, yanapaswa kutekelezwa kwa muda mfupi ili kila mwananchi kupata fursa ya kuchagua au kuchaguliwa katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025.

Othman alisema kama hayo hayatatekelezwa, hawatokuwa na sababu ya kubaki kwenye Serikali ya Umoja wa Kitaifa kwa sababu dunia na taasisi za kimataifa itawashangaa kuendelea kuwamo katika serikali hiyo ambayo imeshindwa kuweka misingi ya haki na demokrasia.

Hata hivyo, alisema kamati ya uongozi ya ACT Wazalendo imeshawasilisha msimamo wake kwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Muungano juu ya mambo ya msingi yanayopaswa kuzingatiwa kabla ya ACT Wazalendo kuamua kuwamo au kujitoa katika SUK.

Alisema kutokana na kuendelea kusuasua kwa utekelezaji wa mambo waliyokubaliana kamati ya uongozi wa chama hicho unatarajiwa kukutana mwezi huu, kufanya tathmini kabla ya kutoa uamuzi wa kuendelea kuwemo katika serikali hiyo au kujiondoa.

Makamu Mwenyekiti wa chama hicho, Ismail Jussa, alisema chama kimeandaa mkakati wa kuhakiki wanachama na wafuasi nyumba kwa nyumba ili kujua idadi yao, ikiwemo walioandikishwa na ambao bado ili kuweka kumbukumbu sahihi kabla ya kuingia katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025, alisema mchakato huo utafanyika mwaka huu.



Msemaji wa Kampuni ya Tumbaku ya Alliance One, John Magoti (katikati), akifafanua jambo mbele ya Mkuu wa Mkoa wa Tabora (kushoto), Paul Chacha, wakati kiongozi huyo alipotembelea uwekezaji na maendeleo ya masoko ya ununuzi wa tumbaku mwaka huu. Kulia ni Mkurugenzi wa Uzalishaji Kampuni hiyo, David Mayunga. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Naibu Spika: Zanzibar ina uhaba wataalamu afya

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Spika wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Mgeni Hassan Juma, amesema Zanzibar inamahitaji makubwa ya wataalamu wa sekta ya afya.

Hivyo, ameiomba Global Education Link (GEL) kuwaunganisha wanafunzi wa visiwa hivyo na vyuo vikuu nje ya nchi, ili iweze kupata wataalamu wa kutosha.

Aliyasema hayo mwishoni mwa wiki wakati akizungumza na ujumbe wa Global Education Link ukiongozwa na Mkurugenzi Mkuu, Abdulmalik Mollel, uliotembelea Baraza la Wawakilishi kwa mwaliko wa Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Ali Abdulgulam Hussein.

Alisema maendeleo ya nchi yanahitaji vijana wenye ujuzi mbalimbali, hivyo mchango wa taasisi hiyo kwenye sekta ya elimu ni wa kuigwa.

"Nawapongeza mnafanyakazi kubwa na ngumu inayohitaji uvumilivu sana. Mimi nilishawahi kusema kwenye Baraza la Wawakilishi kuhusu wanafunzi kukosa nafasi za kazi wanazotaka hapa visiwani kwa hiyo kama kuna fursa ya kuwapeleka nje ya nchi ni jambo jema sana," alisema.

Alisema amefurahi kusikia Global imekuwa ikifanya kazi ya kuwabadili mitazamo vijana wa kitanzania na kuwajenga kwa ajili ya kujiajiri zaidi badala ya kuhangaika kutafuta ajira kila wanapohitimu masomo yao.

"Lazima tuwajenge vijana waweze kujitegemea, tumejisahau kidogo kwenye malezi vijana wengi hawawezi kazi kwa hiyo kuna haja ya kuwabadili fikra zao ili waweze kujitegemea na hata wakipata kazi wafanye kazi kwa bidii," alisema.

Alisema Zanzibar kuna vijana wengi wanaohitaji kupata ufadhili wa elimu ya juu, lakini wanakwama kwa kukosa maarifa ya sehemu wanayoweza kupata msaada, hivyo aliiomba Global iwe kiunganishi baina ya vijana hao na taasisi mbalimbali.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA RESULT SLIP



**ZAHIA ABDUL MMBAGA** anatangaza kupotea kwa Result slip ya kidato cha nne chenye index namba **S0499/0050** iliyotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **OLALENI SECONDARY SCHOOL** mwaka **2023**. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**POLISI TAARIFA: PHQ/KIL/MOS/10346/2024**

---

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**JUDICIARY**
**IN THE DISTRICT DELEGATE COURT OF MOROGORO**
**AT MOROGORO**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE No 11286 OF 2024**
**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE**
**PETER DEBO MWAKIOSA**
**AND**
**IN THE MATTER OF APPLICATION FOR A LETTER OF ADMINISTRATION BY:-**
**1: LINDA THOBIAS NGENDABANYIKWA**
**2: ____________________**

All persons claiming to have any interest in the estate of above-named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letter of administration) is made to the above - named petitioner.
Objection to the grant should be filed on or before the 13 day of 6.2024
DATED at MOROGORO this 17 day of MAY 2024

..... Resident Magistrate ....

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO**
**YA WILAYA YA MOROGORO**
**KITUO CHA MJINI**
**MKOA WA MOROGORO**
**Usimamizi wa Mirathi Na...27/2024**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU: MAJALIWA OMARY wa MAFIGA**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI**
**YALIYOLETWA NA KIJAKAZI SAID ABDALLAH.**
**TANGAZO**
**(kanuni ya 5 (2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 4 Mwezi 6 Mwaka 2024 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**
- Endapo kuna yeyote mwenye Wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
- Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani na waweza kukaguliwa
- Marehemu hakuacha wosia

Imetolewa leo Tarehe 15 mwezi 5 mwaka 2024

HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO
MOROGORO

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO KIHONDA**
**WILAYA YA MOROGORO**
**MKOA WA MOROGORO**
**Usimamizi wa Mirathi Na...14/2024**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU: RACHEL EDINGTON MOSHI**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI**
**YALIYOLETWA NA LULU HARSON NGOWI**
**TANGAZO**
**(kanuni ya 5 (2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo Tarehe 27 Mwezi 5 Mwaka 2024 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**
- Endapo kuna yoyote mwenye wosia wa marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
- Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani na waweza kukaguliwa
- Marehemu hakuacha wosia

Imetolewa leo tarehe 17 mwezi 05 mwaka 2024

HAKIMU

---

## TAYEBAT SISAL LIMITED

Namba ya Usajili. **158916088**
Inapenda kuwatangazia wadau wake rasmi kuwa kampuni ya **TAYEBAT SISAL LIMITED** inatarajia kufanya kikao cha kwanza cha kufunga kampuni cha tarehe 28/05/2024 hivyo basi kupitia taarifa hii kufungwa kwa kampuni, inakaribisha mwenye madai au lalamiko lolote afike ofisini kuwasilisha taarifa yake.

**Asante**
**Mkurugenzi wa Kampuni**

---

## TAYEBAT SISAL LIMITED

Namba ya Usajili. **158916088**
Inapenda kuwatangazia wadau wake rasmi kuwa kampuni ya **TAYEBAT SISAL LIMITED** inatarajia kufanya kikao cha mwisho cha kufunga kampuni cha tarehe **31/05/2024** hivyo basi kupitia taarifa hii kufungwa kwa kampuni, inakaribisha mwenye madai au lalamiko lolote afike ofisini kuwasilisha taarifa yake.

**Asante**
**Mkurugenzi wa Kampuni**

---

## TAYEBAT SISAL LIMITED

Namba ya Usajili. **158916088**
Inapenda kuwatangazia wadau wake rasmi kuwa kampuni ya **TAYEBAT SISAL LIMITED** imemteuwa Mfilisi wa Kampuni **LINDA ELIUD LUGANO** wa **S.L.P 2228** Tanga-Tanzania ambaye atakuwa anahusika na shughuli zote za Ufilisi wa Kampuni kwa kipindi cha taratibu za kufunga Kampuni.

**Asante**
**Mkurugenzi wa Kampuni**

---

## KUPOTEA KWA CHETI



**JACKSON ZAKARIA NANYARO** anatangaza kupotea kwa cheti cha kuhitimu kidato cha nne chenye index No. S5431/0101 Kilichotelewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia HARADANI WINNERS SECONDARY SCHOOL mwaka 2020, Cheti hiki kimepotea mkoani Dodoma. Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo cha polisi.

**Taarifa ya Polisi: PHQ/DOD/DOD/17680/2024**

---

## KUPOTEA KWA CHETI



**SHELLY SAMWEL OGOYA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kuhitimu kidato cha nne chenye index No. S0719/0033 Kilichotelewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **MASONGA SECONDARY SCHOOL** mwaka 2014, Cheti cha kidato cha sita chenye **No. S0668/0667** Kilchotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **DAKAWA SECONDARY SCHOOL** mwaka 2017. Vyeti vimepotea **RORYA (SHIRATI) -MARA.** Yeyote atakaeviona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**Taarifa ya Polisi: PHQ/DOD/DOD/18654/2024.**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA MWANZO [W] BOMANI**
**KATIKA WILAYA YA IRINGA**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**[MCA/84] R:E 2002**
**SHAURI LA MADAI 27/2024**
**MDAI......................BRAC FINANCE**
**MDAIWA...........................SUZAN MUSA**

**KWA: SUZAN MUSA**
Shauri la Madai tajwa hapo juu limefunguliwa katika Mahakama hii na BRAC FINANCELTD madai ya fedha kiasi cha 1,667,200/=, mdaiwa popote ulipo unaamuriwa kufika Kuhudhuria Mahakamani tarehe 30/05/2024 Saa 2:30 Asubuhi kujibu madai hayo na kwa Kua siku hiyo n siku ya kusikiliza shauri hilo ni lazima kuleta mashahidi wako kwa ajili ya Kujitetea bila kukosa. Usipofika bila taarifa shauri litasikilizwa upande mmoja na hukumu Kutolewa. Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahalam hii leo Tarehe 16/05/2024.

RESIDENT MAGISTRATE
HAKIMU MAHAKAMA YA MWANZO (W) BOMANI – IRINGA
MUHURI WA MAHAKAMA

---

**IN THE HIGH COURT OF TANZANIA**
**(IN THE SUB-REGISTRY OF ARUSHA)**
**AT ARUSHA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 19 OF 2023**
**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE**
**MICHAEL NGALEKU SHIRIMA ........................................ DECEASED**
**AND**
**IN THE MATTER OF AN APPLICATION FOR PROBATE BY:**
**CHRISTIAN CHARLES SHIRIMA ........................................ PETITIONER**

**NOTICE TO CREDITORS**
**(Rule 111)**

NOTICE is hereby given that all persons claiming debts or liabilities affecting the estate of the above-named MICHAEL NGALEKU SHIRIMA, deceased, who died at the Aga Khan Health Centre, Dar es Salaam, on the 9th day of June 2023, and probate of whose Will was granted to me by the Court on the 13th day of December 2023, are hereby required to send in their claims to me at the following address within two months from the date of the publication of this notice at the expiration of which time I shall proceed to hand over the assets to the persons entitled thereto having regard only to the claims of which I shall then have had notice.

Signed and dated this ..14th.. day of May, 2024.

.....................................
CHRISTIAN CHARLES SHIRIMA
(EXECUTOR)
OF: P. O. BOX 70770,
DAR ES SALAAM.
MOBILE: +255 784 563 274

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKMA YA WILAYA YA MWANGA**
**UTHIBITISHO NA USIMAMIZI WA MIRATHI**
**SHAURI LA MIRATHI NA 6184 YA MWAKA 2024**
**MAOMBI YA BARUA YA USIMAMIAJI WA MIRATHI YA**
**SILAS ENOCK MSANGI.....................MAREHEMU**
**ELIEWAHA URUBANO MSANGI............ MUOMBAJI**

**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(kanuni ya 75)**

Watu wote wanaodai kuwa na haki katika mirathi ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolwa kwa barua ya usimamiaji wa mirathi kwa muombaji aliyeomba hapo juu.
Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikwa mnamo au kabla ya tarehe 24 Mwezi MEI, Mwaka 2024.
Imewasilishwa Mwanga leo tarehe 24 Mwezi APRILI Mwaka 2024

HAKIMU MKAZI MKUU
MAHAKAMA YA WILAYA
MWANGA
Principal Resident Magistrate I/c
Mwanga

---

**IN THE HIGH COURT OF UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**(IN THE SUB REGISTRY OF KIGOMA)**
**AT KIGOMA**
**LAND CASE NO.32/2023**
**SYLIVANUS SEHEYE............APPELANT**
**(Administration of the Late SYLIVANUS SEHEYE KIKWAYA)**
**VERSUS**
**MWAYAYA VILLAGE COUNCIL.........1ST RESPONDENT**
**THE ATTORNEY GENERAL..............2ND RESPONDENT**
**OMARY KABHOHE..................3RD RESPONDENT**
**JOHN NDELEKA.....................4TH RESPONDENT**

**NOTICE OF DATE FOR MENTION/HEARING**

**TO:**
**OMARY KABHOHE**
**C/O VEO MWAYAYA VILLAGE**
**BUHIGWE**

**TAKE NOTICE** that the above case has been fixed for **HEARING** on 17th day of **MAY**, **2024** at **10:15 AM** before Hon. Rwizile, J.
**YOU ARE** required to appear in this court on the fixed date without fail.
**GIVEN UNDER MY HAND** and the **SEAL** of the court this 23rd day of APRIL, 2024.

DEPUTY REGISTRAR

---

**OFISI ZA MATANGAZO**
**Mikocheni Industrial Area, Po.Box 31042, Dar es Salaam.**
**Mob: +255 - 0677020701**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz,**
**Website: www.ippmedia.com**

**Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0677020701**

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Jeshi la DRC lazuia jaribio la mapinduzi

**KINSHASA,** DRC

MSEMAJI wa Jeshi la Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC), Bregedia Jenerali Sylvain Ekenge, amesema jeshi nchini humo limefanikiwa kuzuia jaribio la mapinduzi lililohusisha wapiganaji raia wa nchi hiyo na wa kigeni.

Akizungumza kupitia televisheni ya taifa, Ekenge alisema jaribio hilo lilifanyika asubuhi ya jana, na kwamba washukiwa kadhaa wamezuiliwa na hali sasa imedhibitiwa.

"Jaribio la kuipindua serikali limezuiwa na vikosi vya ulinzi. Jaribio hilo limehusisha Wakongomani na wageni. Watu hao akiwemo kiongozi wao, hawakupata nafasi ya kusababisha madhara," alisema Bregedia Jenerali Ekenge.

**Ijumaa, Rais Felix Tshisekedi alikutana na wabunge na viongozi wa chama tawala katika jaribio la kuutatua mzozo ndani ya chama hicho.**

Ilibainishwa kuwa taarifa hilo ilitolewa saa chache baada ya watu watatu wakiwemo walinzi wawili na mshambuliaji mmoja walipouawa katika shambulio kwenye makazi ya mwanasiasa Vital Kamerhe, mbunge anayewania kiti cha spika wa bunge la taifa hilo.

Mapigano yaliripotiwa kati ya watu wenye silaha waliovalia sare za jeshi na walinzi wa mwanasiasa huyo kwenye makaazi yake yaliyoko eneo la Tshatshi Boulevard, kilomita mbili karibu na Ikulu ya nchi hiyo na baadhi ya ofisi ya balozi za kigeni.

Msemaji wa Vital Kamerhe, Michel Muhim, aliandika kwenye mtandao wa kijamii wa X kuwa, mwanasiasa huyo na familia yake wako salama na kwamba ulinzi wao hivi sasa umeimarishwa.

Jaribio hilo la mapinduzi linatokea katikati ya mivutano ndani ya chama tawala cha Rais Felix Tshisekedi juu ya nafasi ya kiti cha spika wa bunge katika uchaguzi uliopangwa kufanyika Jumamosi na ambao umeahirishwa.

Vyombo vya habari vya ndani vilisema waliohusika na shambulio hilo ni wanajeshi wa Kongo. Licha ya kwamba haikuwa wazi iwapo watu hao waliovalia sare za jeshi walikuwa wakijaribu kumkamata Vital Kamerhe ama laa.

Picha za video, zilizoonekana kutoka eneo la tukio, zilionyesha malori ya kijeshi na watu wenye silaha wakipita karibu na makazi ya mwanasiasa huyo.

Ijumaa, Rais Felix Tshisekedi alikutana na wabunge na viongozi wa chama tawala katika jaribio la kuutatua mzozo ndani ya chama hicho.

Tshisekedi alikwenda mbali zaidi na kutishia kulivunja bunge na kumrudisha kila mtu nyumbani kwenye uchaguzi mpya iwapo kile alichokiita mazoea mabaya yataendelea.

Ubalozi wa Marekani nchini Kongo ulitoa tahadhari ya usalama na kuwahimiza watu kuwa macho kufuatia ripoti za kutokea makabiliano ya risasi.**DW**

## IFC, Standard zaipiga jeki sekta viwanda Tanzania

**KIGALI,** Rwanda

SHIRIKA la Fedha la Kimataifa (IFC) na Benki ya Standard ya Afrika Kusini wamesaidia ukuaji wa sekta ya viwanda nchini kwa kusaidia upanuzi wa kiwanda cha kutengeneza vioo cha Tanzania ili kukidhi ongezeko la mahitaji ya ndani na kikanda ya chupa za kioo na kontena.

Ilielezwa kuwa chini ya ushirikiano huo, IFC itatoa mkopo wa dola milioni 45 (Sh. bilioni 116.2) na Benki ya Standard itatoa dola milioni 15 (Sh. bilioni 38.7) kusaidia kioo kukuza uwezo wake wa utengenezaji na kuongeza soko la nje.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa juzi na taasisi hizo, mradi huo utazalisha maelfu ya ajira, pia kupitia mkopo huo Kioo itaongeza kiwango cha glasi iliyorejeshwa ambayo hutumia katika mchakato wake wa uzalishaji, na kusaidia kupunguza matumizi ya nishati.

Pia ilibainishwa kuwa Tanzania ni miongoni mwa nchi chache za Afrika Mashariki zenye uwezo wa muda mrefu wa kutengeneza glasi na kuuza nje ya nchi.

"Mradi pia utakuza ukuaji wa sekta ya vinywaji katika kubadilisha glasi iliyoagizwa kutoka nje na bidhaa zinazotengenezwa Tanzania na za gharama nafuu," ilisema sehemu ya taarifa hiyo.

Iliongeza kuwa Kioo itatumia malighafi na nishati zinazopatikana Tanzania na kuzalisha bidhaa iliyoongezwa thamani ya viwango vya dunia kwa ajili ya kusafirisha nje.

Akizungumza wakati wa hafla ya utiaji saini mkopo huo iliyofanyika Kigali Rwanda, Waziri wa Viwanda na Biashara wa Tanzania Ashatu Kijaji, aliishukuru IFC kwa kusaidia sekta ya biashara nchini, akieleza kuwa anatarajia ushirikiano zaidi katika sekta nyingine.




Waziri wa Viwanda na Biashara, Dk. Ashatu Kijaji (katikati), akiwa pamoja na viongozi wa Shirika la Kimataifa la Fedha (IFC) na uongozi wa KIOO Limited baada ya kusaini mkopo kwa kampuni hiyo juzi. **PICHA: MTANDAO**

# Mwandishi wa habari amrithi Jokate

**Na Elizabeth Zaya**

KAMATI Kuu ya Halmashauri Kuu ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), imemteua Mwandishi wa Habari, Suzan Kunambi, kuwa Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Wanawake Tanzania (UWT), ambaye amewahi kuwa Mkuu wa Wilaya ya Magharibi A, visiwani Zanzibar.

Suzan ameteuliwa kuongoza nafasi hiyo baada ya aliyekuwa akishikilia nafasi hiyo, Jokate Mwegelo kuteuliwa kwenda kuongoza kwenye Jumuiya ya Umoja wa Vijana (UVCCM) katika nafasi ya Katibu Mkuu.

Kamati hiyo ya Halmashauri Kuu ya CCM, katika kikao chake maalum kilichofanyika Ofisi Kuu ya chama hicho, Kisiwandui, Zanzibar chini ya Makamu Mwenyekiti wake na Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, pamoja na mambo mengine, ilimteua Khamis Yusuf Mussa (Pele), kuwa mgombea ubunge kwa tiketi ya chama hicho Jimbo la Kwahani, Wilaya ya Mjini, Mkoa wa Mjini Magharibi.

'Pele' atapeperusha bendera ya CCM katika uchaguzi mdogo wa ubunge unaotarajiwa kufanyika Juni 8, mwaka huu kutokana na kifo cha aliyekuwa mbunge wa jimbo hilo, Ahmada Yahya Shaa, aliyefariki Aprili 8, mwaka huu.

Kwa mujibu wa taarifa ya Katibu wa Halmashauri Kuu ya CCM Taifa, Itikadi na Uenezi, Amos Makalla, Kamati Kuu hiyo ilizipongeza serikali zote mbili kwa namna zinavyoendelea kuwatumikia wananchi kwa vitendo kupitia utekelezaji wa ilani ya uchaguzi ya chama hicho ya mwaka 2020-2025.

### MNEC AKABIDHI LESENI WANAWAKE

Wakati huo huo, Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa ya Chama Cha Mapinduzi (NEC) Mkoa wa Simiyu, Gungu Silanga, amekabidhi leseni kwa wachimbaji wa madini wanawake wa mkoa huo, kwa ajili ya kuwarahisishia kazi zao.

Silanga aliyasema hayo jana mbele ya Waziri wa Madini, Anthony Mavunde, wakati akikabidhi leseni kwa wachimbaji hao wanawake.

"Mimi ni MNEC wa Simiyu waliponifuata nikawaambia sawa lakini nendeni mkaunde kikundi kitakachokuwa na wawakilishi wa wilaya zote tano za mkoa huu. Kinamama hawa ni wasikivu walifanya hivyo."

Silanga alifafanua kuwa baada ya kukamilisha taratibu hizo aliwasiliana na ofisa madini aliyempa fomu na kuwakabidhi leseni Jumamosi.

Waziri Mavunde amemshukuru Silanga kwa moyo wake wa uelewa na kufuata maelekezo ya serikali na kwa hatua hiyo amewapa heshima kinamama wa Mkoa wa Simiyu.

"Umepandikiza mbegu kubwa sana, ulichokifanya kwa kinamama hawa kina maana kubwa katika uchumi, umekuwa muungwana, mstaarabu na msikivu kwa kuwajali wanawake wa Simiyu.

"Uchimbaji ni gharama kubwa sana, serikali inaangalia mipango mizuri ya kusaidia na kuwezesha kinamama na vijana kufanya uchimbaji na wizara itakusaidia MNEC," alisema Mavunde.

# MSHINDI PARIMATCH KITAA CUP KUPATA ZAWADI NONO

**Na Faustine Feliciane**

KAMPUNI ya michezo ya kubashiri ya Parimatch imezindua mashindano maalum ya mpira wa miguu ya "Kitaa Cup 2024' yenye lengo la kuinua na kuendeleza vipaji katika mchezo huo.

Mashindano haya yanashirikisha jumla ya timu nane kutoka maeneo mbalimbali ya Jiji la Dar es Salaam kwa mujibu wa Mkuu wa Masoko wa kampuni hiyo, Levis Paul.

Paul alizitaja timu hizo kuwa ni Faru Dume, Karume FC, Kawe UTD, Makubuli FC, Kauzu FC, Namanga FC, Mpakani FC pamoja na Rangi Tatu FC.

**Mshindi wa mashindano hayo ya siku mbili atazawadiwa fedha shilingi 1,000,000, mshindi wa pili shilingi 500,000 huku mshindi wa tatu atazawadiwa mipira miwili.**

Aidha, alisema pia kutakuwa na zawadi ya mfungaji bora, golikipa bora pamoja na mchezaji bora wa kila mchezo.

"Timu zote shiriki zimepewa jezi na mpira ambazo zitatumika katika mashindano haya , tumeona kila timu wachezaji wake wapo na morali ya juu, hii inaonyesha mashindano haya yatakuwa na ushindani mkubwa," alisema Paul.

Alisema kuwa kampuni ya Parimatch imedhamiria kuchangia maendeleo ya michezo nchini kwa vitendo na hasa kwa timu za mitaani ambapo kuna wachezaji wengi wanaoweza kuleta mafanikio kwa klabu mbalimbali na timu ya Taifa.

"Kutokana na hilo, ndiyo maana tumeandaa mashindano haya ya muda mfupi, kusaidia vifaa vya michezo na kuweka zawadi nono, hii itasaidia wachezaji kupambania timu zao ili kuibuka washindi.

Nawaomba mashabiki wa soka wa Dar es Salaam kujitokeza kwa wingi ili kupata burudani safi kutoka timu zetu za mitaani," alisema Paul.




Wachezaji wa Faru Dume na Karume United wakichuana jana katika mechi ya ufunguzi ya michuano ya 'Parimatch Kitaa Cup 2024' kwenye uwanja wa Zakhiem, Mbagala jijini Dar es Salaam. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## *Tembo Warriors kutupa karata ya kwanza leo*

**Na Saada Akida**

TIMU ya Taifa ya soka kwa watu wenye ulemavu 'Tembo Warriors', leo wanashuka dimbani kuperusha bendera ya Tanzania katika michuano ya Afrika (AAFCON) dhidi ya Sierra Leon.

Mashindano hayo yamefunguliwa rasmi juzi, Tembo Warriors itacheza mchezo wake wa kwanza kwenye uwanja wa Al Salaam, jijini Cairo, Misri ambapo Tanzania imepangwa kundi D ikiwa na timu za Angola, Rwanda na Sierra Leon.

Kundi A zipo timu za Cameroon, Misri, Burundi na Nigeria, Kundi B ina timu za Liberia, Morocco, Uganda na Senegal na Kundi C kuna timu za Ghana, Kenya, Gambia na Algeria.

Akizungumza na Nipashe jana, Kocha Mkuu wa Tembo Warriors, Salvatory Edward alisema wamefika salama nchini humo na wamefanya maandalizi mazuri kuelekea mchezo wao wa leo.

Aidha, alisema mchezo huo hautakuwa mwepesi kwa sababu hawajapata muda wa kuwaona wapinzani wao hivyo wanakutana nao wakiwa hawawafahamu.

"Ninaimani na vijana wangu, wengi wao wanauzoefu mkubwa kwa sababu wanacheza soka la kulipwa kwenye mataifa mbalimbali yanayofanya vizuri katika mchezo huu, watasaidiana na wale wanaocheza ndani kwa ajili ya kupata matokeo mazuri," alisema kocha huyo.

Aliongeza kuwa anamatumaini makubwa kwa vijana wake kufuata maelekezo aliyowapa katika uwanja na mazoezi na kuhamisha kwenye mechi na kutafuta matokeo chanya ya ushindi katika mechi hiyo ya kwanza.

## Waganda wang'aa mashindano netiboli Afrika Mashariki

**Na Shufaa Lyimo**

MASHINDANO ya klabu bingwa Afrika Mashariki ya mchezo wa netiboli yamemalizika juzi kwenye Uwanja wa Benjamini Mkapa jijini Dar es Salaam huku timu za Uganda, NIC na Wob zikiibuka mabingwa kwa upande wa wanaume na wanawake.

Nafasi ya pili katika mashindano hayo kwa upande wa wanawake ilichukuliwa na timu ya Prisons ya Uganda pia na nafasi ya tatu ikibaki nchi kwa timu ya Uhamiaji.

Kwa upande wa wanaume nafasi ya pili ilichukuliwa na timu ya KIUT ya Uganda na nafasi ya tatu ilichukuliwa na Smart Boys ya Dar es Salaam.

Akizungumza baada ya kumalizika kwa mashindano hayo Ofisa Michezo wa Baraza la Michezo la Tanzania (BMT), Charles Maguzu ambaye alimwakilisha Katibu Mtendaji, Neema Msitha aliwapongeza washiriki wote na kuwataka wale walioshindwa wasikate tamaa na badala yake wajipange kwa mashindano mengine.

"Ninawapongeza wale wote walioshinda na kupata zawadi ya makombe na medali, kwa wale ambao hamjafanikiwa kupata ushindi msikate tamaa nendeni mkajipange kwa ajili ya mashindano mengine," alisema Maguzu.

Aidha aliwataka wachezaji wa Tanzania kuongeza juhudi na kushirikiana na timu za Uganda ili na wao wawe na viwango kama vya kwao.

**Wakati huo huo**, nahodha wa timu ya Uhamiaji wanawake, Kulwa Asedy alisema amefurahi kushika nafasi ya tatu na kudai timu ya NIC iliwazidi uwezo kutokana na kuwa wachezaji wao wengi wenye uzoefu mkubwa.

"Licha ya Uganda kutuzidi hatujakata tamaa, tunajipanga kwa ajili ya mashindano mengine naamini tutafanya vizuri zaidi, alisema Asedy.

Kwa upande wake nahodha wa mabingwa, NIC, Namulema Fildaus, alisema siri ya ushindi wao huo umetokana na maandalizi ya muda mrefu waliyoyafanya, nidhamu pamoja na kufuata maelekezo waliyopewa na benchi lao la ufundi.

"Kabla mashindano haya hayajaanza tulikuwa tayari tumeshaanza mazoezi kwa lengo la kuendelea kutetea ubingwa wetu, vile vile timu zote ambazo tulikutana nazo zilikuwa na uwezo wa kawaida, Alisema Fildaus.

## ZISIKUPITE

### CASEMIRO ATAKIWA SAUDIA

KLABU za Ligi Kuu ya Saudia (Saudi Pro) zina nia ya kumsajili kiungo wa kati wa Manchester United na Brazil Casemiro, 32, na kiungo wa kati wa Ureno, Bruno Fernandes, 29. ***(Telegraph)***

### WALTERS AIKATALIA ARSENAL

ARSENAL inakaribia kumpoteza mlinzi Reuell Walters, 19, baada ya mchezaji huyo wa kimataifa wa England kukataa ofa ya mkataba mpya ili kutafuta nafasi kwingineko. ***(Athletic)***

### TRENT AWINDWA MADRID

REAL Madrid bado wana nia ya kumsajili mchezaji wa kimataifa wa England, Trent Alexander-Arnold, 25, kutoka Liverpool. ***(Fabrizio Romano kupitia Football365)***

### MBAPPE HAKUNA MZOZO

RIPOTI za kuibuka kwa mzozo mkubwa kati ya mshambuliaji wa Ufaransa Kylian Mbappe, 25 na Rais wa Paris St-Germain, Nasser Al-Khelaifi kabla ya mechi ya Ligue 1 dhidi ya Toulouse zimetupiliwa mbali na vyanzo vya mabingwa hao wa Ufaransa. ***(Marca)***

### ALONZO AZITAKA ZOTE

KOCHA wa Bayer Leverkusen, Xabi Alonso anatumaii kusimamia klabu zake zote tatu za zamani za Liverpool, Real Madrid na Bayern Munich lakini hana uhakika ni kwa utaratibu gani. ***(Abendzeitung)***

### BAYERN YABANIWA

NIA ya Bayern Munich kumnunua kocha wa Crystal Palace, Oliver Glasner ilififlia baada ya klabu hiyo ya Bundesliga kuambiwa itawagharimu pauni milioni 86. ***(Bild)***

### CONTE ANUKIA NAPOLI

NAPOLI imeanzisha tena mazungumzo na Antonio Conte kuhusu kuwa kocha wao baada ya Muitaliano huyo kupunguza mahitaji yake ya mshahara, huku AC Milan pia ikitaka kuzungumza na kocha huyo wa zamani wa Chelsea na Tottenham. ***(Il Mattino)***

### RAMOS KUHAMIA MAREKANI

MLINZI wa zamani wa Sevilla na timu ya taifa ya Hispania, Sergio Ramos, 38, amepiga hatua katika mazungumzo yake na klabu ya San Diego FC kuhusu kuhamia Ligi Kuu ya Soka ya Marekani. (MLS). ***(Athletic)***

### COLE ANYATIWA

BEKI wa zamani wa timu ya taifa ya England na klabu za Ligi Kuu ya England Arsenal na Chelsea, Ashley Cole, 43, ananyatiwa na klabu kadhaa za Championship ili kuchukua nafasi ya ukocha. ***(Mirror)***

### CHELSEA KUSAJILI MABEKI

KLABU ya Chelsea inatazamia kusajili mshambuliaji na mabeki wawili msimu huu wa majira ya joto huku Wakurugenzi wa michezo wa klabu hiyo, Paul Winstanley na Laurence Stewart wakitarajiwa kukabidhiwa tena majukumu yao ya uhamisho. ***(Telegraph?)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# MODRIC, KROOS MIKATABA MIPYA

**MADRID,** Hispania

**●●● Real Madrid imepanga kuwaongeza mkataba mwingine wa mwaka mmoja wakongwe...**

LUKA Modric anakaribia kungana na mkongwe mwenzake wa Real Madrid, Toni Kroos katika kuongeza mkataba wake na klabu hiyo kwa msimu mwingine, kwa mujibu wa ripoti.

**Kocha Carlo Ancelotti analeta kizazi kipya cha viungo wa kati Bernabeu akiwamo Jude Bellingham, Federico Valverde, Eduardo Camavinga na Aurelien Tchouameni.**

Kwa kuzingatia mustakabali, wote wawili Kroos na Modric walionekana kuwa na uwezekano wa kukamilisha misimu yao ya kubeba makombe katika mji mkuu wa Hispania mwishoni mwa msimu huu.

Hata hivyo, habari za Kroos kusalia kwa mwaka mwingine ziliibuka mwishoni mwa Machi ingawa bado sio rasmi na sasa, labda cha kushangaza zaidi, ripoti za kutaka kusalia kwa Modric zimeibuka.

AS na Marca zimedai Modric mshindi wa Ballon d'Or amekubali kupunguzwa kwa muda wake wa kucheza msimu huu ingawa bado amethibitisha kuwa kiungo muhimu katika hatua za mwisho za kampeni, haswa wakati wa kufuzu kwa fainali ya Ligi ya Mabingwa.

Ripoti zote mbili zinaangazia jukumu la rais wa klabu Florentino Perez katika kuwezesha kubaki kwao ndani ya timu hiyo.

Sasa kuna 'makubaliano ya kimsingi' kwa Modric kuendelea na Madrid, huku wakala wake Vladica Lemic pia ameviambia vyombo vya habari: "Jambo linalowezekana zaidi ni kwamba atakaa mwaka mmoja zaidi na kuendelea kuandika historia.

"Real Madrid ni klabu bora zaidi duniani na inaongozwa na rais bora katika historia ya soka. Luka Modric ni shabiki wa Real Madrid ambaye anaipenda klabu hiyo na anaichukulia kuwa nyumbani kwake."

Kroos na Modric wamecheza mechi 32 na 30 mtawalia La Liga msimu huu, ingawa Mjerumani huyo amecheza dakika 2,043 ikilinganishwa na nyota huyo wa zamani wa Tottenham Hotspur aliyecheza 1,590.

HABARI MICHEZO

# RAMSDALE ACHEKA KUSAJILIWA NEWCASTLE




**LONDON,** England

MLINDA mlango wa Arsenal, Aaron Ramsdale amecheka ripoti kwamba amekubali kujiunga na Newcastle United msimu huu wa majira ya joto.

Ramsdale alipoteza nafasi yake kuanzia wiki za mwanzoni mwa msimu baada ya kuwasili kwa David Raya, ambaye mkopo wake kutoka Brentford unatarajiwa kufanywa wa kudumu msimu huu.

Huku msimu mwingine kwenye benchi la Arsenal ukikaribia, klabu kadhaa zinadaiwa kutaka kumchukua Ramsdale katika miezi ijayo, huku Newcastle wakihusishwa mara kwa mara na saini ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26.

Iliripotiwa hata Ijumaa kwamba Ramsdale alikuwa amefikia makubaliano ya kuhamia St James' Park, lakini kipa huyo haraka aliingia kwenye mitandao ya kijamii na kuzima uvumi huo.

"Habari kwangu," aliandika kwenye X, zamani Twitter, akiweka picha yake akicheka.

Gazeti la Telegraph limesema kuwa Newcastle wanataka kumnunua Ramsdale kwa dau la pauni milioni 15, kwani hawezi kuvumilia kukaa nje kwa msimu mwingine.

Chelsea, ambao mara nyingi wanahusishwa kutaka kumnunua Ramsdale, hawatarajiwi kumfuatilia nyota huyo wa kimataifa wa England huku ikibakia kuonekana iwapo West Ham United itashughulikia nia yao baada ya David Moyes kuondoka mwishoni mwa msimu huu.

Uhakikisho wa dakika za kutosha kucheza utakuwa ufunguo wa uamuzi wa Ramsdale anapotafuta kutengeneza nafasi iliyopotea kwenye pambano lake la kugombania namba mwenye kikosi cha England na Jordan Pickford wa Everton.

# Chelsea kumnunua Willian

**LONDON,** England

CHELSEA imekubaliana na Palmeiras kwa ajili ya usajili wa winga Estêvão Willian mwenye umri wa miaka 17, kwa mujibu wa ESPN.

Klabu hiyo ya London Magharibi imeshinda ushindani kutoka kwa baadhi ya klabu kubwa za Ulaya ili kuafikiana makubaliano ambayo vyanzo vimeiambia ESPN kuwa ni ya awali ya Euro milioni 34 huku nyongeza zinazohusiana na uchezaji zinaweza kufikia jumla ya euro milioni 67.

Kijana huyo anachukuliwa kuwa mmoja wa wenye vipaji bora zaidi katika nchi yake ya kuzaliwa Brazil, lakini ikiwa uhamisho huo utakamilika, hatajiunga na klabu hiyo hadi 2025.

Chelsea imetanguliza kusajili vipaji vya vijana tangu Todd Boehly na Clearlake Capital walipokamilisha uchukuaji wa umiliki miaka miwili iliyopita huku wakiwekeza zaidi ya pauni milioni moja.

Wametekeleza mikataba kadhaa na klabu za Amerika Kusini katika muda wa madirisha machache yaliyopita.

Andrey Santos na Kendry Páez, walisajiliwa Chelsea mwaka jana, wakati Thiago Silva ataondoka katika klabu hiyo na kujiunga na klabu yake ya zamani ya Fluminense baada ya mechi ya mwisho ya msimu wao wa Ligi Kuu jana Jumapili.






# Reus awanunulia bia mashabiki

**DORTMUND,** Ujerumani

KIPENZI cha Borussia Dortmund, Marco Reus alinunua bia kwa takriban uwanja mzima kwa mashabiki wa timu hiyo kwenye mchezo wake wa mwisho wa nyumbani kwa klabu Jumamosi.

"Ilipangwa mapema," Reus alisema. "Ilikuwa kamili, ninashukuru sana kwa upendo wote ambao watu wamenionesha."

Kabla ya kuwanywesha kila mtu, aliwapa raha uwanjani kwa bao na kutengeneza jingine katika ushindi wa mabao 4-0 dhidi ya Darmstadt katika mchezo wa mwisho wa Bundesliga kwa Dortmund msimu huu.

Zaidi ya mashabiki 81,000 walihudhuria mechi hiyo, ingawa si wote walikuwa na umri wa kunywa bia, lakini wengi walikubali ofa ya nahodha huyo.

Dortmund ilichapisha kwenye ukurasa wake wa X barua iliyotiwa saini na Reus ambapo alisema, "Asante kwa kila kitu! Bia ya kuaga ni kwangu," ikifuatiwa na sura ya tabasamu na maneno "Marco wako."

Reus mwenye umri wa miaka 34 anaondoka Dortmund baada ya miaka 12 katika klabu hiyo. Alifunga kwa mkwaju wa faulo katika dakika ya 38 baada ya kumtengenezea, Ian Maatsen bao la kwanza.

"Huwezi kufikiria kuwa nzuri zaidi," alisema Mkurugenzi wa michezo wa Dortmund Sebastian Kehl.

"Ingekuwa kwaheri kamili ikiwa hatungetaka kumvika taji tena baada ya wiki mbili. Kwa hiyo lilikuwa ni tendo lake la mwisho hapa, lakini kuna jingine linakuja. Tunajisikia vizuri pamoja nasi hadi Wembley."

Dortmund itamenyana na Real Madrid katika fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya kwenye Uwanja wa Wembley jijini London Juni 1. Reus alisema anataka kuendelea kucheza, ingawa hakusema ni wapi.

"Nataka kucheza kwa sababu ninahisi vizuri na ninajiamini, lakini kwanza fainali ya Ligi ya Mabingwa iko kwenye umakini," alisema Reus.

## Yanga, Azam fainali ya kisasi Kombe la FA

INATOKA UKURASA 24

Dakika kumi kabla ya mechi kwenda mapumziko, beki wa kulia wa Yanga, Nickson Kibabage alianguka peke yake uwanjani, baada ya kufanyiwa matibabu akatolewa nje nafasi yake ikachukuliwa na Joyce Lomalisa.

Joseph Mahundi itabidi ajilaumu mwenyewe, alipokosa bao la wazi dakika za nyongeza kabla ya kwenda mapumziko, alipompora mpira, Mohamed Ibrahim 'Bacca', akakimbia nao mpaka ndani ya boksi huku kipa Diara akiwa ametokea, alipiga shuti la ovyo mpira ukatoka nje wakati goli likiwa tupu.

Mshambuliaji Rupia alikaribia kuifungia Ihefu goli lakini mpira wake wa kichwa ulipanguliwa kiufundi na Diarra.

Kipindi cha pili hakikuwa kizuri kama cha kwanza, kwani timu zote zilionekana kufunga njia na mpira kuchezwa kati zaidi, huku kukiwa na mashambulizi machache.

Pia dakika za mwisho, Ihefu ilionekana kupaki basi zaidi na kushambulia mara chache.

## Simba yatenga 'mpunga' wa maana kwa Fei Toto

INATOKA UKURASA 24

Kuhusu taarifa za beki wao Henock Inonga kuondoka kwenda kwenye mapumziko, Ahmed alisema beki huyo ameondoka kwa ruhusa maalum bado na ni mali ya Simba hadi msimu ujao mkataba wake unapomalizika.

"Hakuna ukweli kuwa kuna ofa imekuja kwetu, Inonga ni mchezaji wetu, watu wasimgombanishe mchezaji na mashabiki wa Simba, hivyo Inonga atarejea nchini kuitumikia timu yake endapo hakutakuwa na ofa kutoka kwenye timu nyingine," alisema Ahmed.

Katika hatua nyingine, Ahmed alisema kikosi cha timu hiyo kinaendelea na mazoezi kujiandaa na mchezo dhidi ya Geita Gold FC utakaochezwa kesho.

"Bado tunahitaji alama tisa katika michezo mitatu iliyosalia, hii ni muhimu sana kwetu kuzipata ili kujihakikishia nafasi ya pili na kucheza Ligi ya Mabingwa Afrika," alisema Ahmed.

Simba ipo nafasi ya tatu ikiwa na alama 60 wakilingana na Azam wanaoshika nafasi ya pili lakini wakiwa na uwiano mzuri wa magoli.

# FEI TOTO ASUBIRIA OFA

**Na Mwandishi Wetu**

KIUNGO mshambuliaji wa Azam FC, Feisal Salum, amesema anasubiria ofa zitakazokuja kutoka klabu yoyote inayomhitaji baada ya msimu huu kumalizika.

**Akizungumza jijini Mwanza juzi, Fei Toto, amesema anasikia maneno mbalimbali kuwa baadhi ya klabu za nje na hata za ndani zinamhitaji, anasubiri ofa hizo zije kwa mwajiri wake.**

Mchezaji huyo amevunja ukimya huo baada ya maneno mengi ya kutakiwa na baadhi ya klabu kutoka nje ya nchi, na ndani ya nchi ikitajwa Simba kumnyemelea.

Fei Toto amesema kwa sasa ana mkataba wa Azam FC, lakini hakuna klabu inayozuiliwa kwenda kwa uongozi wa klabu yake kama inamhitaji na yeye atakuwa tayari kama klabu hizo zitakubaliana.

"Kwanza kabisa kila mchezaji anatamani kwenda kucheza soka la kulipwa nje ya nchi, Mwenyezi Mungu akijaalia kama kwenda nje, basi nitaenda.

Pia uongozi wangu ndiyo unajua kuhusu ofa ambazo imepokea kutoka kwenye klabu za ndani au nje, tusubiri mwisho wa msimu itakuwaje, kama viongozi wana uhakika na hizo ofa basi wataniambia," alisema Fei Toto.

Siku moja kabla Fei Toto kusema hayo, Meneja Habari na Mawasiliano wa Klabu ya Simba, Ahmed Ally, alisema inamuhitaji kiungo huyo, lakini bado ana mkataba na Azam FC, hivyo inahitaji mazungumzo ya kina.

"Mipango yetu ni kufanya usajili mkubwa, wapo wachezaji hapa hapa nchini ambao wanamaliza mikataba na klabu zao kubwa, Fei Toto yeye bado ana mkataba na timu yake, inahitaji mazungumzo ya kuvunja, lakini hawa wengine hakutakuwa na tatizo la kuwasajili kwa sababu watakuwa huru," alisema bila kuwataja majina wachezaji hao wengine na klabu wanazochezea.

Wakati huo huo, mchezaji huyo amesema siri ya kuwa na kiwango cha juu msimu huu ni kujituma.

Alisema mchezaji ili aweze kucheza kwa kiwango cha juu anatakiwa autunze mwili wake kwa sababu ndiyo anaoutumia kufanyia kazi ya kusakata kabumbu.

"Hakuna kingine, ni kujitunza tu kwa mchezaji, na pia kumuweka Mungu karibu," alisema Feitoto.

Nyota huyo wa zamani wa klabu ya Yanga, mpaka sasa amepachika mabao 15 kwenye Ligi Kuu akiwa sawa na Stephane Aziz Ki wa Yanga, wote wakiwa na 'asisti' nane kila mmoja na kuongoza kwenye orodha ya wafungaji bora wa Ligi Kuu Tanzania Bara.



Mwanafunzi wa Shule ya Sekondari Ukonga, Ali Mohamed (kulia), akiruka juu kuupiga mpira dhidi ya wanafunzi wa Sekondari ya Ilala, katika mchezo wa mpira wa wavu wa mchujo wa kusaka timu ya Mkoa wa Ilala itakayoshiriki michuano ya UMISETA, kwenye viwanja vya Shule ya Sekondari Pugu Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## *Simba U20 yatinga nusu fainali bila kuruhusu bao*

**Na Adam Fungamwango**

TIMU ya vijana ya Simba chini ya miaka 20, imetinga hatua ya nusu fainali ya Ligi ya wachezaji wenye umri huo kwa timu za Ligi Kuu, bila kuruhusu bao lolote katika hatua ya nane bora.

Timu hiyo imekuwa moja kati ya timu nne ambazo zimetinga hatua ya nane bora ya ligi hiyo, timu nyingine ni Dodoma Jiji, ikitoka Kundi A pamoja na Simba, Azam FC ikiongoza Kundi B, pamoja na Kagera Sugar.

Vijana wa Simba, walianza hatua hiyo kwa kuichapa Ihefu mabao 2-0, na baadaye kuiadhibu Dodoma Jiji bao 1-0, kabla ya kutoka suluhu katika mechi yake ya mwisho dhidi ya JKT Tanzania.

Imemaliza mechi zake ikiwa na pointi saba, ikicheza mechi tatu, imeshinda mechi mbili na haijapoteza mchezo wowote, huku Dodoma Jiji ikisonga mbele kwa kuwa na pointi sita, ikicheza mechi tatu, kushinda mbili na kupoteza moja.

Kocha Mkuu wa timu hiyo, Mohamed Mrisho, alisema wanashukuru wachezaji wake kwa kujituma katika mechi zote hadi kufikia hatua hiyo, kwani haikuwa rahisi kutokana na ushindani mkali katika ligi hiyo.

"Nawapongeza wachezaji wangu, tumeandaa mpango na wao wamekwenda kutekeleza uwanjani, sasa tunajiandaa kucheza hatua ya nusu fainali, tunakwenda kurekebisha mapungufu tuliyoyaona katika mechi zilizopita," alisema Mrisho.

Kinara wa Kundi B, Azam FC yenyewe imecheza mechi tatu, imeshinda mbili, sare moja, ikifunga mabao manne, kufungwa mawili na kukusanya pointi saba.

Kagera Sugar nayo imetinga nusu fainali ikiwa na pointi saba baada ya kucheza mechi tatu, imeshinda mechi, imepata sare moja huku ikifunga mabao matatu na kuruhusu bao moja.

Simba itacheza nusu fainali dhidi ya Kagera Sugar, huku Azam FC ikitarajiwa kucheza dhidi ya Dodoma Jiji.

# Michezo

Jumatatu Mei 20, 2024

Nipashe




Ramsdale acheka kusajiliwa Newcastle UKURASA 22

# Yanga, Azam fainali ya kisasi Kombe la FA

## Ushindi wa jana wa Wanajangwani dhidi ya Ihefu unafanya timu hizo zikutane kwa mara ya pili mfululizo kwenye...

**Na Adam Fungamwango**

HATIMAYE fainali ya Kombe la Shirikisho la Mpira wa Miguu (TFF), iliyopangwa kufanyika Uwanja wa Tanzanite, Babati mkoani Manyara, utazikutanisha Azam FC na Mabingwa Watetezi, Yanga kama ilivyokuwa msimu uliopita.

**Hii ni baada ya Yanga jana kuibuka na ushindi wa bao 1-0 katika mechi ya nusu fainali iliyochezwa Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini Arusha.**

Ilibidi Yanga isubiri hadi dakika ya 100 ili kupata bao baada ya mechi hiyo kuingia kwenye dakika 120 kufuatia dakika 90 kumalizika bila kufungana.

Bao hilo lilifungwa na kiungo, Stephane Aziz Ki kwa shuti kali la mguu wa kushoto baada ya kupokea pasi ya Pacome Zouzoua aliyeingia kipindi cha pili kuchukua nafasi ya Maxi Nzengeli.

Mpira ulianzia kwa Khalid Aucho aliyemnyang'anya mchezaji mmoja wa Ihefu na kuipeleka wingi ya kulia ambako Pacome alikuwapo, akaingia ndani kidogo na kumtengea mfungaji wa bao.

Bao hilo limeipeleka Yanga fainali kwenda kuumana na Azam FC, ambayo ilitinga hatua hiyo juzi, ilipoifunga Coastal Union mabao 3-0, Uwanja wa CCM Kirumba, Mwanza.

Fainali hiyo itakuwa inajirudia tena kwani msimu uliopita timu hizo zilikutana Juni 12, mwaka jana, Uwanja wa Mkwakwani, Tanga na Yanga ilifanikiwa kutwaa ubingwa baada ya kuibuka na ushindi wa bao 1-0, lililowekwa wavuni na Kennedy Musonda.

Jana timu zote mbili zilianza kwa kucheza pasi ndefu kwenda kwenye wingi zao za kulia na kushoto, lakini mabeki wa pande zote walikaa imara.

Dakika ya 12, Yanga ilianza kulisalimia lango la Ihefu, pale mshambuliaji Clement Mzize alipoupata mpira akiwa ndani ya eneo la hatari, akiwa amebaki golikipa wa Ihefu, Khomein Aboubakar, shuti lake dhaifu liliishia mikononi mwa kipa huyo.

Dakika tano baadaye Ihefu ilijibu kwa shambulizi kupitia kwa mshambuliaji raia wa Togo, Marouf Tchakei, ambaye aliambaa na mpira kutoka katikati ya uwanja na kabla hajaingia ndani ya boksi, aliachia shuti kali lililompita kipa wa kimataifa wa Mali, Djugui Diarra, lakini badala ya kutinga wavuni ukatoka nje.

Yanga nayo ilikosa bao la wazi dakika ya 27, pale Aziz Ki alipounganisha vibaya krosi ya Mzize kutoka pembeni kidogo upande wa kulia.

INAENDELEA UKURASA 23



Kiungo wa Yanga, Aziz Ki aliyefunga bao pekee dhidi ya Ihefu na kuipeleka timu hiyo fainali ya Kombe la FA. **PICHA: MAKTABA**

## Simba yatenga 'mpunga' wa maana kwa Fei Toto

**Na Saada Akida**

IMEELEZWA uongozi wa klabu ya Simba umetenga fedha za kutosha kwa ajili ya kufanikisha usajili wa kiungo wa klabu ya Azam FC, Feisal Salum 'Fei toto' ili ajiunge na timu hiyo.

Mbali na Fei Toto, Simba pia inaangalia uwezekano wa kumsajili kiungo wa Yanga, Stephane Aziz Ki katika harakati zao za kujiimarisha na kurudisha heshima ya klabu hiyo.

Aziz Ki ni kinara wa mabao kwenye ligi ambapo mpaka sasa ana magoli 15 akilingana na Fei Toto, hata hivyo mkataba wa mchezaji huyo ndani ya Yanga unamalizika mwishoni mwa msimu huu.

Mbali na Simba, pia inaelezwa kuna timu kutoka Afrika Kusini ambazo zinafanya mchakato wa kumsajili kiungo huyo wa kimataifa wa Burkina Faso.

Akizungumza na Nipashe jana, Meneja wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, amesema klabu hiyo ipo makini katika usajili na mchezaji wanayemtaka hawatashindwa kumsajili.

Alisema wanafahamu kiungo huyo mkataba wake unaenda ukingoni ingawa kwa Feitoto mambo sio mepesi kutokana na nyota huyo kuwa na mkataba hai na Azam.

"Ni kweli hao wachezaji wawili wapo kwenye mipango yetu mmoja mkataba wake umefikia ukingoni na bado hajasaini mkataba mpya, kwa Fei Toto ni suala la kuweka fedha mezani ili kumchukua," alisema Ahmed na kuongeza,

"Pia kuna wachezaji wengine wapya tunawafuatilia sokoni kulingana na mapendekezo ya benchi la ufundi kwa ajili ya kuwasajili na kuimarisha kikosi chetu kwa ajili ya msimu ujao," alisema Ahmed.

Alisema uongozi wa klabu hiyo utawasilisha ofa yao kwa Azam kuangalia uwezekano wa kumchukua kiungo huyo wa timu ya taifa 'Taifa Stars' na Zanzibar.

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >